# TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR

## RIPOTI YA UTAFITI WA SHERIA YA LESENI NAMBA 3 YA MWAKA 1983 NA MAPENDEKEZO YA KUANZISHWA SHERIA YA USIMAMIZI WA MBEGU

**INAWASILISHWA KWA MHESHIMIWA WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA**

**JANUARI, 2022**

**MHESHIMIWA HAROUN ALI SULEIMAN,**

**WAZIRI WA NCHI, AFISI YA RAIS- KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA,**

**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA DKT. MWINYI TALIB HAJI,**
**MWANASHERIA MKUU WA ZANZIBAR,**
**ZANZIBAR.**

**MHESHIMIWA OMAR SAID SHAABAN,**
**WAZIRI WA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA,**
**ZANZIBAR.**

Kwa mujibu wa Kifungu cha 14 cha Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar, Nam. 16 ya Mwaka 1986, kwa heshima, Tume inawasilisha Ripoti ya Mapitio ya Sheria ya Leseni Nam. 03 ya mwaka 1983.

**…………………………**

**KHADIJA SHAMTE MZEE**
**MWENYEKITI,**
**TUME YA KUREKEBISHA SHERIA,**
**ZANZIBAR**

**05 Aprili, 2022.**

## MAKAMISHNA WA TUME YA KUREKEBISHA SHERIA ZANZIBAR



**BIBI. KHADIJA SHAMTE MZEE**

**MWENYEKITI**



**DKT.YAHYA KHAMIS HAMAD**
**KAMISHNA**



**ND. SALIM MOHAMED ABDALLA**
**KAMISHNA**



**ND. JUMA MSAFIRI KARIBONA**
**KAMISHNA**



**DKT. SIKUJUA OMAR HAMDAN**
**KAMISHNA**



**MHE. JAJI AZIZA IDDI SUWEDI**
**KAMISHNA**



**ND. MUSSA KOMBO BAKARI**
**KATIBU**

| | |
|---|---|
| Mhe. Khadija Shamte Mzee | Mwenyekiti |
| Mhe. Jaji Aziza Iddi Suwedi | Kamishna |
| Dr. Yahya Khamis Hamad | Kamishna |
| Dr. Sikujuwa Omar Hamdan | Kamishna |
| Nd. Salim Mohammed Abdalla | Kamishna |
| Nd. Juma Msafiri Karibona | Kamishna |
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu |

**WATAFITI**

| | |
|---|---|
| Nd. Mussa Kombo Bakari | Katibu wa Tume |
| Nd. Khamis Ali Jaku | Mtafiti wa Sheria |
| Nd. Mwanaid Juma Suleiman | Mtafiti wa Sheria |
| Nd, Rahma Salum Fundi | Mtafiti wa Sheria |

Tume ya Kurekebisha Sheria

Vuga, Zanzibar-

P.O BOX 2539,

Simu +255 24 2231143,

Nukushi +255 24 2231137,

barua pepe info@lrcz.go.tz.

tovuti www.lrcz.go.tz

## VIFUNGU VYA UTANGULIZI

**Makamishna……………………………………………………………………………..ii**

**Sheria zilizotumika……………………………………………………………………..viii**

**Shukrani…………………………………………………………………………………..xi**

**Vifupisho vya Maneno…………………………………………………………………..xii**

**Rejea……………………………………………………………………………………..xiii**

**Muhtasari………………………………………………………………………………..xviii**

**SURA YA KWANZA**

1.0 **UTANGULIZI**…………………………………………………………………………..1

1.1 **Mamlaka ya Tume**………………………………………………………………………1

1.2 Historia ya leseni za Biashara Zanzibar……………………………………………………2

1.3 Hadidu Rejea………………………………………………………………………………..5

1.4 Malengo ya Utafiti……………………………………………………………………………6

1.5 Tamko laTatizo la Utafiti……………………………………………………………………7

1.6 Njia za Utafiti…………………………………………………………………………………7

**SURA YA PILI**

2.0 **DHANA YA LESENI ZA BIASHARA**……………………………………………………8

**2.1 Utangulizi**……………………………………………………………………………………8

2.2 Maana ya Biashara……………………………………………………………………………9

2.3 Leseni ya Biashara…………………………………………………………………………10

2.4 Umuhimu wa Leseni…………………………………………………………………………11

2.5 Viwango vya leseni…………………………………………………………………………12

2.6 Muda wa Leseni……………………………………………………………………………12

2.7 Usimamizi wa Leseni………………………………………………………………………13

2.8 Kanuni ya usawa na Uwiano(equity and proportionality)…………………………………14

2.9 Vyombo vya kuto leseni……………………………………………………………………15

**SURA YA TATU**

3.0 **UCHAMBUZI WA SERA NA SHERIA……………………………………………………17**

**3.1 Sera……………………………………………………………………………………………17**
3.1.1 Dira ya Maendeleo ya 2050- 2050………………………………………………………17
3.1.2 ILANI YA CCM 2020- 2015……………………………………………………………18
3.1.3 Sera ya Biashara yam waka 2006………………………………………………………19
3.1.4 Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005……………………………………………………20
3.1.5 Sera ya Wajasiriamali Wadogo nawa kati Zanzibar ya mwaka 2005……………...21
3.1.6 Sera ya Ajira Zanzibar 2009……………………………………………………………22
3.1.7 Sera ya Serikaliz Mitaa Zanzibar ya mwaka 2012……………………………………22
3.1.8 Sera ya Mazingira ya mwaka 2014……………………………………………………23
3.1.9 Sera ya Mafuta na Gesi ya Zanzibar (Upstream) yam waka 2016………………….23
3.1.10 Sera ya Afya Zanzibar yam waka 2010……………………………………………...24
3.1.11 Sera ya Kilimo Zanzibar ya mwaka 2000……………………………………………24
3.1.12 Sera ya Uvuvi Zanzibar yam waka 2000……………………………………………..25
3.1.13 Sera ya Usalama wa Chakula Zanzibar ya mwaka 2008…………………………….25
3.1.14 Sera ya Usafiri Zanzibar ya mwaka 2008……………………………………………25
3.1.15 Sera ya Asasi ya Kiraia Zanzibar ya mwaka…………………………………………...26
3.1.16 Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006……………………………………………..26
3.1.17 Sera ya Habari na Mawasiliano yam waka 2013……………………………………...27
3.1.18 Sera ya Jinsia Zanzibar ya mwaka 2005……………………………………………27
3.1.19 Sera ya Usimamizi wa Maafa Zanzibar yam waka 2011……………………………...27
3.1.20 Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014…………………………………………...28
3.2 Sheria zinazohusiana na Leseni za Biashara Zanzibar……………………………..29
3.2.1 Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983…………………………………29
3.2.2 Sheria ya Biashara Nam. 14 ya mwaka 2013…………………………………………...33
3.2.3 Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya 2013…………35
3.2.4 Sheria ya Utalii Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2009……………………………………37
3.2.5 Sheria ya Misitu na mali zisizohamishika Nam. 10 ya 1996…………………………..38
3.2.6 Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar Nam. 7 ya 2014……………….40
3.2.7 Sheria ya Uvuvi Nam.7 ya mwaka 2010……………………………………………..41
3.2.8 Sheria ya Mamlaka yaBahari Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2009…………………..42
3.2.9 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za maji na Nishati Zanzibar Nam.7 ya 2013..43

3.2.10Sheria ya Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020……………………………………………………..44
3.2.11Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya mwaka 2006…………………...45
3.2.12Sheria ya Tume ya utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997……………………………46
3.2.13Kanuni ya Usafiri wa Bahari(Usajili na Leseni za Vyombo) ya mwaka 2007..46
3.2.14Zanzibar Industrial Property Act, Nam. 4 ya mwaka 2008…………………………47
3.2.15Sheria y Usajili wa Makandarasi Nam. 6 ya mwaka 2008…………………………..48
3.3 Sheria ya Muungano zinazotoa Leseni Zanzibar……………………………………...48
3.3.1 Sheria ya Benki ya Tanzania (BOT) Nam. 4 ya mwaka 2006……………………..48
3.3.2 Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi nyengine za Kifedha
Nam. 5 ya mwaka 2006……………………………………………………………………….49
3.3.3 Sheria ya Kusimamia Maendeleo ya Uvuvi wa bahari kuu Nam.5 ya 2020…50
3.3.4 Sheria ya Bima Nam. 10 ya mwaka 2009……………………………………………….51
3.3.5 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Nam. 12 ya mwaka 2003"TCRA"………..52

**SURA YA NNE**

4.0 **MAONI YA WADAU…………………………………………………………………………53**
4.1 Utangulizi…………………………………………………………………………………………..53
4.2 Maoni ya Sheria…………………………………………………………………………………..53
4.3 Maoni ya Kiutendaji……………………………………………………………………………..55

**SURA YA TANO**

**5 MIKATABA YA KIMATAIFA NA SHERIA ZA NCHI MBALI MBALI……………58**
**5.1 Mikataba ya Kimataifa……………………………………………………………………….58**
5.2 Mikataba ya Kikanda……………………………………………………………………………63
5.3 Sheria na uzoefu wa nchi mbali mbali…………………………………………………….65

**SURA YA SITA**

**6.0 MATOKEO YA UTAFITI……………………………………………………………………..79**
**6.1. Utangulizi……………………………………………………………………………………….79**
6.2 Njia zilizotumika katika Utafiti **………………………………………………………….79**
6.3 Upeo wa Utafiti……………………………………………………………………………………79
6.4Ukomo wa utafiti………………………………………………………………………………….80

6.5 Hadidu Rejea……………………………………………………………………………………80
6.6 Sampuli za Utafiti……………………………………………………………………………...81
6.7 Matokeo ya utafiti……………………………………………………………………………..84

**SURA YA SABA**

**1.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO……………………………………………93**

**1.1 Utangulizi………………………………………………………………………………………93**

1.2 Uchambuzi na Changamoto za Mfumo wa Leseni za Biashara Zanzibar………93

**1.3** Mapendekezo ya Tume **…………………………………………………………………97**

1.3.1 Mapendekezo ya Jumla……………………………………………………………...97

1.3.2 Kisera………………………………………………………………………………………...98

1.3.3 Mapendekezo ya Kisheria……………………………………………………………..100

1.3.4 Mapendekezo ya Kikanuni……………………………………………………………..106

1.3.5 Mapendekezo ya kiutendaji…………………………………………………………...106

**7.4 Hitimisho** ………………………………………………………………………………………107

**SHERIA ZILIZOTUMIKA**

## SHERIA

Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar namba 16 ya mwaka1986

Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983

Sheria ya Biashara Nam. 14 ya mwaka 2013

Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya 2013

Sheria ya Utalii Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2009

Sheria ya Misitu na Mali zisizohamishika Nam. 10 ya 1996.

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar Nam. 7 ya 2014

Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya mwaka 2010

Sheria ya Mamlaka ya Bahari Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2009.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar Nam. 7 ya 2013.

Sheria ya Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020

Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya mwaka 2006

Sheria Ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997

Kanuni ya Usafiri wa Baharini (Usajili na Leseni za Vyombo) ya mwaka 2007

Zanzibar Industrial Property Act, Nam. 4 ya mwaka 2008

Sheria ya Usajili wa Makandarasi Nam. 6 ya mwaka 2008

Sheria ya Benki ya Tanzania (BOT) Nam. 4 ya mwaka 2006

Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi nyengine za Kifedha Nam. 5 ya mwaka 2006

Sheria ya Kusimamia Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari kuu Nam. 5 ya mwaka 2020

Sheria ya Bima Nam. 10 ya mwaka 2009

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Nam. 12 ya mwaka 2003 “TCRA”

Sheria ya Leseni ya Tanzania Bara Sheria Nam, 25 ya mwaka 1972, Sura ya 208 Sheria za Tanzania

Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 249 ya mwaka 1998 Vanuatu

Sheria ya biashara ya Seychelles Sura ya 113 ya mwaka 2010

Sheria ya Biashara Sura ya 43:02 ya mwaka 2008 Botswana

Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 40:02 ya mwaka 2016Tonga

**MIPANGO YA NCHI**

Dira ya Maendeleo ya 2050- 2050

ILANI YA CCM 2020-2015

**SERA**

Sera ya Biashara ya mwaka 2006

Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005

Sera ya Wajasiriamali Wadogo na wa kati Zanzibar ya mwaka 2005

Sera ya Ajira Zanzibar 2009

Sera ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2012

Sera ya Mazingira ya mwaka 2014

Sera ya Mafuta na Gesi Zanzibar (Upstream) ya mwaka 2016

Sera ya Afya Zanzibar ya mwaka 2010

Sera ya Kilimo Zanzibar ya mwaka 2000

Sera ya Uvuvi Zanzibar ya mwaka 2000

Sera ya Usalama wa Chakula Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Usafiri Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Asasi za Kiraia Zanzibar ya mwaka  2008

Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006

Sera ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2013

Sera ya Jinsia Zanzibar ya mwaka 2005

Sera ya Usimamizi wa Maafa Zanzibar ya mwaka 2011

Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014

## SHUKRAN

Tume inatoa shukrani kwa Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda,kwa ushirikiano wao katika utafiti huu kupitia vikao vya wadau na kubainisha maeneo yenye mapungufu usimamizi na utoaji wa leseni Zanzibar. Shukrani za pekee kwa Katibu wa Wizara na Baraza la Usimamizi wa Leseni Zanzibar kwa ushirikiano katika kukamilisha utafiti huu.

Shukran kwa taasisi na Mamlaka za Leseni za Zanzibar na Mamlaka za leseni za Muungano zilizopo Zanzibar ambazo zimeshiriki katika vikao vya Tume na kutoa michango yao na uzoefu katika kutoa na kusimamia leseni.

Tume inawashukuru wafanyabiashara wa Zanzibar kupitia Jumuiya ya Wafanyabiashara kwa kushiriki na kutoa maoni yao katika matayarisho ya Ripoti hii pamoja na Mapendekezo.

Shukrani za pekee ziende kwa Makamishna wa Tume, Katibu wa Tume Nd. Mussa Kombo Bakari na wafanyakazi wa Tume ya Kurekebisha Sheria kwa kuongoza zoezi la utafiti huu na kufanya uchambuzi yakinifu na uandishi wa ripoti.

Uzoefu na changamoto zilizoelezwa kuikumba sekta hii vimeisaidia sana Tume kuweka misingi na Mapendekezo ya Tume, na kuhakikisha changamoto zilizopo katika utoaji na usimamizi wa leseni Zanzibar zinazingatiwa katika mapendekezo ya Tume.

**VIFUPISHO VYA MANENO**

| | |
|---|---|
| AG | Antony General |
| BRELA | Business Registration and Licensing Agency |
| CCM | Chama cha Mapinduzi |
| EAC | East Africa Community |
| FDI | Foreign Direct Investment |
| GATT | General Agreement on Tariff and Trade |
| GATS | General Agreement on Trade in Services |
| SMEs | Small and Medium Enterprises |
| MKUZA | Mkakati wa Kuondoa Umasikini Zanzibar |
| MSMEs | Micro and Small and Medium Enterprises. |
| MTN | the Multilateral Trade Negotiations |
| ITO | International Trade Organisation |
| ICT | Information and Communication Technology |
| NGO | Non Governmental Organisation |
| PPP | Public Private Pertnership |
| SLA | Seychelles Licensing Authority |
| RIA | Regulatory Impact Assessment |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| EPZ | Economic Processing Zone |
| TZS | Tanzanian Shilling |
| WTO | World Trade Organization |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Agency |
| ZPRP | Zanzibar Poverty Reduction Plan |
| TCRA | Tanzania Communication Regulatory Authority |
| JITAP | The Joint Integrated Trade Assistance Programme |
| ZMCL | Zanzibar Media Corporation Ltd |
| ZEXA | Zanzibar Exporter Association |

## REJEA

### VITABU NA MAKALA

Abdul Sheriff, "The Peasantry Under Imperialism, 1873 - 1963" in Abdul Sheriff and Ed Ferguson (eds.) Zanzibar Under Colonial Rule (London: James Currey, 1991), p.112 and Abdul Sheriff, "The Spatial Dichotomy of Swahili Towns: The Case of Zanzibar in the nineteenth Century" in AZANIA: Journal of the British institute in Eastern Africa, Volume XXXVI-XXXVII 2001-2002, (Nairobi: The British Institute in Eastern Africa), 2002

Akman Pinar, *The Concept of Abuse in EU Competition Law: Law and Economic Approaches*, 2012, Hart Publishing, Oxford

Antoniak M (1995). 21st Century Entrepreneur: How to Start a Home Business. New York: Avon

Anderman, Steven & Schmidt Hedvig, *EU Competition Law and Intellectual Property Rights: The Regulation of Innovation, 2011*, 2nd edition, Oxford University Press, Oxford.

Baldwin R. (2000) '*Regulatory Protectionism, Developing Nations and a Two –Tier World Trade System,*' International Trade and Regional Economic

Bheenick, R.M., 2003. "The EAC Customs Union Protocol: The Application of the Principle of Asymmetry." Study prepared for the East African Community Secretariat. Imani Development Consultants, Pretoria.

Booth, D., Cooksey, B., Golooba-Mutebi, F., & Kanyinga, K. (2014). East African prospects: an update on the political economy of Kenya, Rwanda, Tanzania, and Uganda. Overseas Development Institute. https://www.odi.org/publications/8383-east-african-prospectsupdate-political-economy-kenya-rwanda-tanzania-and-uga

Braithwaite J. & Drahos P. (2000) 'Global Business Regulation', Cambridge University

Cichocki KM, "Unlocking the Future of Public Libraries: Digital Licensing that Preserves Access" (2007-2008) 16 University of Baltimore Intellectual Property Law Journal

Cross W M, (2012) "Restoring the Public Library Ethos: Copyright, E-Licensing, and the Future of Librarianship," Law Library Journal 104:2

David McKitterick (1992) *A History of Cambridge University Press*: Volume 1, Printing and the Book Trade in Cambridge, 1534 -1698 printed by the Syndicate of the University of Cambridge

Dreschle B (2001). Small-Scale Mining and Sustainable Development within the SADC Region, MMSD project of IIED, International Institute for Environment and development. Available at: https://www.scribd.com/document/91701845/Small-Scale-Miningand-Sustainable-Development-Within-the-SADC-Region

Fred H. Cate, (2002). "The commodification of information and the control of expression," *Amicus Curiae* (Journal of the Institute of Advanced Legal Studies, School of Advanced Studies, University of London), volume 43, pp.. 3–7.

Gellhorn W (1956) "Individual Freedom and Governmental Restraints."Baton Rouge: Louisiana State University Press

Gervais D, Maurushat A, "Fragmented Copyright, Fragmented Management: Proposals to Defrag Copyright Management" (2003) Canadian Journal of Law and Technology 2, 15

Hills C. A. (2007), '*How the WTO Fight Protectionism'* The International Trade Law Newsletter, Vol. 2 issue 1, March, 2009

Hinkes, 2007:709 Hinkes E M, "Access Controls in the Digital Era and the Fair Use/First Sale Doctrines" (2006-2007) 23 Santa Clara High Technology Law Journal 685

Hildebrand, Doris, *The Role of Economic Analysis in the EC Competition Rules, 2009*, 3rd edition, Kluwer Law International

John Willey & Sons Australia Ltd, *Mohan Dhall (contributing author)*; *Business Studies in Action, Preliminary Course*; Stephen Chapman, Natalie Devenish 3rd Edition

Kampala Capital City Authority (KCCA) (2017), Trading Licence (Assessment, Payment & Issuance). Available at: https://www.kcca.go.ug/uDocs/Trade_Licence_FAQs.pdf

Khadija Shamte Mzee "Setting up A Business in Zanzibar: The Legal Requirements," LYBL Volume 8 -2018

Paul Dobson and Rob Stokes: (2012) *Commercial Law*, Sweet and Maxwell London,

*Protecting Your Trademark; Enhancing Your Rights through Federal Registration*, BASIC Facts About Trade mark, United States Patent ND Trademark Office; available at https://www.uspto.gov/sites/default/files/documents/BasicFacts.pdf

Pedro A. De Miguel Asensio: *The Law Governing International Intellectual Property Licensing Agreements (A Conflict of Laws Analysis)*, Research Handbook on Intellectual Property Licensing Cheltenham, Edward Elgar Publishing, 2013

Peter Stimpson and Alex Smith *Business Management for the IB Diploma 978-1-107-46437-7*, Second Edition, Cambridge University Press 2015

Peter Walkenhorst "Trade Policy Developments in Tanzania: The Challenge of Global and Regional Integratio" February 2005, https://mpra.ub.uni-muenchen.de/23399/1/MPRA_paper_23399.pdf

Robert B. Mabele The Challenges of the Economic Partnership Agreements in Tanzania March 2007: https://library.fes.de/pdf-files/bueros/tanzania/04756.pdf

Sander H. and András I. (1996) "World Trade After the Uruguay Round: Prospects and Policy Options for the Twenty-first Century" Routledge

Robert Goldscheider and Alan H. Gordon Editors, (2006) *Licensing Best Practices, Strategic, Territorial, and Technology Issues*, John Wiley & Sons, Inc, Wiley

Squitieri, Mauro (2012) *Refusals to License Under European Union Competition Law After Microsoft*, Journal of International Business and Law: Vol. 11: Issue. 1, Article 4.

Steve Suranovic (2010): *International Trade: Theory and Policy*; George Washington University Saylor Foundation

Tilley, H. (2014). The political economy of aid and accountability: the rise and fall of budget support in Tanzania. New York: Routledge

UNCTAD-ICTSD, Cambridge University Press, International Centre for Trade and Sustainable Development Cambridge University Press, 2005

World Bank (2010) "Doing Business in Zanzibar 2010" A Co publication of the World Bank and the International Finance Corporation, inapatikana https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/13439/74678.pdf?sequence=1&isAllowed=y

*World Bank "Doing Business 2016 Measuring Regulatory Quality and Efficiency*, 3th edition," World Bank Group Comparing Business Regulation for Domestic Firms in 189 Economies

World Bank Group *Doing Business 2016 Measuring Regulatory Quality and Efficiency*, 13th edition, Comparing Business Regulation for Domestic Firms in 189 Economies, World Bank Group

World Bank '*Policy Response to Global Financial Crisis: Swimming against the Tide; How Developing Countries are coping with the Global Crisis*', World Bank Background paper prepared by World Bank Staff for the G20 Finance Ministers and Central Bank Governors meeting, Horsham, UK 13-14 March, 2009

**TOVUTI**

https://ij.org/activism/legislation/model-legislation/model-economic-liberty-law-1/

https://www.andrewsarbenz.com/business-attorney-tacoma-business-licsense

https://www.investopedia.com/terms/t/trade.asp

https://www.dictionary.com/browse/trade

Trade License- Category, Eligibility, Registration, FAQs (taxguru.in)

https://www.lendingkart.com/blog/trade-licens

https://mn.gov/deed/business/starting-business/legal-regulatory/

https://en.wikipedia.org/wiki/Essential_facilities_doctrine

https://www.britannica.com/topic/General-Agreement-on-Tariffs-and-Trade

https://www.eac.int/resources/11-document/472-710-653-manual-on-the-application-of-the-east-african-community-rules-of-origin

https://www.wto.org/english/tratop_e/tpr_e/tp128_e.htm

**KESI**

MCI v. AT&T, 708 F.2d1081, 1132 (7th Cir. 1983);

Hecht v. Pro-Football, Inc., 570 F.2d 982, 992-93 (D.C. Cir. 1977),

CommissionDecision 92/213/EEC, 1992 O.J. (L 96) 34 (British Midland v. Aer Lingus

*Inc. v.Trinko*, 124 Ct. 872, 881 (2004)

*In the Heart ofAtlanta Motel v. United Sates* 379 U.S. 241, 85 S.Ct.348 13 L.Ed.2d 258 (1964)

**MIKATABA NA RIPOTI**

UNCTAD/DITC/TNCD/7 4 October 2002 Original: United Nations Conference on Trade and Development Multilateral Trading System Impact on National Economy And External Trade Policy Adaptation United Republic Of Tanzania Report prepared by UNCTAD in the framework of the Joint ITC/UNCTAD/WTO Integrated Technical Assistance Programme to Selected Least Developed Countries and other African Countries (JITAP) Under cluster 9: MTS impact on national economy and trade policy adaptation inapatikana https://unctad.org/system/files/official-document/ditctncd7_en.pdf

Understanding on the Interpretation of Article XXIV of the General Agreement on Tariffs and Trade 1994 (on regional agreements) Trade 1994

A Simplified Guide for Micro and Small-Scale Women Cross Border Traders and Service Providers within the East African Community (EAC)

Programme Management Unit, 'Property and Business Formalisation Programme, Vol. 5, Business Formalisation Reform Packages and Outline for Zanzibar'.

Report Analysis of the Business Licensing Regime in Zanzibar Project 6036 Revolutionary Government of Zanzibar April 2011, Maxwell Stamp PLC : Phase 1

General Agreement on Tariff and Trade) ulioanzishwa (GATT) mwaka 1947.

**MUHTASARI**

Uchambuzi wa taratibu zilizopo katika utoaji wa leseni za biashara ni sehemu muhimu kwa maendeleo ya nchi na utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Zanzibar. Ili kutathmini utaratibu wa utoaji leseni, kutambua shughuli muhimu zinazohitaji leseni, kuondoa hatua zisizo za lazima na kuchukua muda katika kupata leseni au vibali Tume imeona kuna haja ya kuifanyia mapitio Sheria ya Leseni Nam. 3 ya 1983.

Utoaji wa leseni za Zanzibar, kama ule wa nchi nyingi za Afrika Mashariki na nchi nyengine zinazoendelea, unatajwa kuwa na changamoto zinazokwamisha biashara binafsi na uwekezaji wa moja kwa moja na hivyo kurudisha nyuma maendeleo ya nchi. Vikwazo vya kiutawala na udhibiti vinazuia uwekezaji, wafanya biashara na biashara ndogo na za kati (SME) na kufanya utaratibu maalum wa usimamizi wa biashara kukosa usimamizi au utaratibu maalum.

Kupunguza taratibu za utoaji leseni na mzigo wa ada za leseni kwa wafanyabiashara ni mkakati muhimu wa Serikali kupitia Wizara ya Biashara na Viwanda, mkakati ambao unalenga kuweka mifumo shirikishi ambayo inaweza kupelekea mazingira bora ya biashara na uwekezaji na pia kuhimiza biashara za ndani na uwekezaji wa kigeni (FDI).

Utafiti huu unakusudia kutathmini taratibu za utoaji wa leseni, mamlaka zinazohusika, athari za mchakato wa mageuzi ya leseni na biashara Zanzibar na matokeo ya utafiti yataisaidia Serikali katika kurahisisha taratibu za utoaji leseni na utaimarisha mazingira ya biashara na kukuza urahisi wa kufanya biashara.

Utafiti huu pia unalenga kurekebisha na kuimarisha mifumo ya sheria, sera, taratibu za kiutawala na hatua zinazoathiri utoaji wa leseni za biashara ili kusaidia ukuaji wa biashara na kuongeza ushindani kama sehemu kuu ya biashara shirikishi.

Mbinu mbalimbali katika utafiti huu zimezingatiwa ikiwemo uzoefu wa Kimataifa na nchi mbalimbali katika mageuzi ya utoaji leseni na kutathmini utaratibu wa utoaji leseni za biashara na mchakato wa mageuzi ili kuimarisha mazingira mazuri ya biashara. Tathmini hiyo pia inaeleza mifano ya mageuzi ya udhibiti wa utoaji leseni na uzoefu wa mageuzi ya nchi nyengine kama Tanzania Bara, Seychelles, Jamhuri ya Vanuatu, Botswana, na Tonga.

Aidha wadau kutoka taasisi mbalimbali na wafanyabiashara wa sekta binafsi katika sekta mbalimbali wameshirikishwa ili kukusanya taarifa kuhusiana na leseni za biashara.

Mwsisho, utafiti umebainisha maeneo mbalimbali ya kuimarishwa katika utoaji leseni ikiwemo uwepo wa taasisi nyingi za leseni ambazo haizna mwongozo unaohusiana na utoaji wa leseni.

## SURA YA KWANZA

## 1.0 UTANGULIZI

### 1.1 Mamlaka ya Tume

Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar imeundwa na Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria ya mwaka 1986.[1] Sheria hiyo inaipa uwezo Tume ya Kurekebisha Sheria kuzifanyia mapitio sheria zote za Zanzibar kwa nia ya kuzirekebisha ili ziende sambamba na maendeleo na mabadiliko ya kimfumo.[2]

Tume ya Kurekebisha Sheria katika kufanya mapitio ya sheria inaweza kufanya mapitio kwa kutumia njia tatu zilizoainishwa katika sheria. Njia ya kwanza, Tume inaweza kufanya mapitio ya Sheria ikiona ipo haja ya kufanya hivyo,[3] njia ya pili ni kwa maelekezo ya Waziri anaehusika na mambo ya sheria,[4] na njia ya tatu ni kwa maelekezo ya Mwanasheria Mkuu wa Zanzibar (AG).[5]

Kutokana na uwezo iliyopewa kwenye Sheria, na katika kutekeleza majukumu yake ya msingi, Tume imefanyia mapitio Sheria ya Leseni za Biashara[6] kwa ajili ya kuainisha mapungufu ya sheria hiyo na kupendekeza Serikalini marekebisho yake.

[1] Nam. 16 ya mwaka 1986
[2] Kifungu cha 4(1) cha sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar Nam. 16 ya mwaka1986
[3] Kifungu cha 4(2)
[4] Kifungu cha 7
[5] Kifungu cha 8
[6] Nam. 3 ya mwaka 1983

Tume ya Kurekebisha Sheria ya Zanzibar, inafanya mapitio ya Mfumo wa leseni na Sheria ya Leseni ya mwaka 1983 kwa madhumuni ya kutambua mapungufu na kupendekeza Marekebisho yake ili kwenda sambamba na nia ya Serikali katika kuwajibika kwa wananchi, kuboresha huduma kwa wananchi, kuboresha huduma kwa taasisi za Serikali na kupunguza urasimu Serikalini.

## 1.2 Historia ya leseni za biashara Zanzibar

Suala la biashara kwa Zanzibar lilijitokeza katika miaka ya 1800 pamoja na kuongezeka kwa mapato kati ya 1804 mpaka 1819 na kuongeza mtaji unaopatikana kwa wafanyabiashara wa Zanzibar. Seyyid Said alijihusisha katika majaribio ya mazao ya biashara, kama vile karafuu, nazi, sukari na kahawa.[7]

Katika mwaka 1933 kulipitishwa Sheria ya Leseni, Decree Nam. 5 ya mwaka 1933. Sura ya Sheria hii ilitungwa kipindi cha utawala wa kikoloni wa Muingereza ambapo ilitungwa ili kudhibiti leseni zote za biashara.

Baada ya Mapinduzi, kulikuwa na uhusiano usio rasmi kwa wafanyabiashara wa Zanzibar na biashara hiyo ilifahamika kama biashara za Waafrika wa Mashariki na wa Asia Kusini kwa mazao ya kilimo,[8] biashara ambayo

---

[7] Abdul Sheriff, "The Peasantry Under Imperialism, 1873 - 1963" in Abdul Sheriff and Ed Ferguson (eds.) Zanzibar Under Colonial Rule (London: James Currey, 1991), p.112 and Abdul Sheriff, "The Spatial Dichotomy of Swahili Towns: The Case of Zanzibar in the nineteenth Century" in AZANIA: Journal of the British institute in Eastern Africa, Volume XXXVI-XXXVII 2001-2002, (Nairobi: The British Institute in Eastern Africa), 2002, pp. 66 -68

[8] Booth, D., Cooksey, B., Golooba-Mutebi, F., & Kanyinga, K. (2014). East African prospects: an update on the political economy of Kenya, Rwanda, Tanzania, and Uganda. Overseas Development Institute. https://www.odi.org/publications/8383-east-african-prospectsupdate-political-economy-kenya-rwanda-tanzania-and-uga

ilianzishwa kwa mara ya kwanza mwanzoni mwa miaka ya 1960 na kudumu hadi leo.[9]

Katika kipindi cha miaka ya 1980, Sheria Nam. 5 ya mwaka 1933 ilifutwa na kutungwa Sheria mpya ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983 ili kukuza uchumi wa nchi na kuweka mfumo wa uchumi na biashara huria (market economy). Mageuzi hayo ya kiuchumi yalipelekea kuongezeka kwa ushiriki wa sekta binafsi na kukua kwa shughuli za kiuchumi katika nchi.

Mwishoni mwa miaka ya 1980 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ilipitisha sera ya biashara huria hali iliyopelekea wafanyabiashara binafsi kuanzisha biashara mbalimbali Zanzibar. Tangu katikati ya miaka ya 1980, Zanzibar imekuwa na mipango ya mageuzi makubwa ya kiuchumi ambapo kipengele kikuu cha mageuzi haya ni ukombozi wa biashara, kukuza uwekezaji na ukuaji wa uchumi. Kwa kufanya biashara huria, uwekezaji kwa kutoa motisha kwa wawekezaji, Serikali ililenga kuongeza ufanisi wa kiuchumi na kuwaondoa wakazi wake kutoka kwenye umaskini na kuongeza kiwango cha maisha.[10]

Mipango na mipango mikuu ya mageuzi ya kiuchumi iliyopitishwa na kutekelezwa Zanzibar ilikuwa ni kutungwa kwa Sheria ya Ukuzaji na Ulinzi wa Uwekezaji Binafsi 1986 kama ilivyorekebishwa mwaka wa 1991, kupitishwa kwa Mipango ya Kufufua Uchumi 1988 na 1989, kuundwa kwa Wakala wa Kukuza Vitega Uchumi Zanzibar (ZIPA) mwaka 1991, kuanzishwa kwa

[9] Tilley, H. (2014). The political economy of aid and accountability: the rise and fall of budget support in Tanzania. New York: Routledge
[10] Report Analysis of the Business Licensing Regime in Zanzibar Project 6036 Revolutionary Government of Zanzibar April 2011, Maxwell Stamp PLC : Phase 1

Kamisheni ya Utalii mwaka 1992, kupitishwa kwa Mamlaka ya Maeneo Huria ya Kiuchumi mwaka wa 1992, kuanzishwa kwa Mamlaka za Bandari Huria na Bandari mwaka 2000, Dira ya Sera za Kitaifa na Kisekta 2020, Mpango wa Kupunguza Umasikini Zanzibar (ZPRP) 2002, Sera ya Zanzibar ya Viwanda (1998-2008), Sera ya Uwekezaji Zanzibar, na Sera ya Biashara ya Zanzibar.[11]

Utaratibu wa utoaji wa leseni ulionekana kuwa sio rafiki, wa gharama kubwa, mzito na unatumia muda mwingi. Michakato ya utoaji leseni inahusisha hatua nyingi sana za usimamizi zisizo za lazima na mara nyingi huhitaji miingiliano mingi na maafisa wa Serikali. Pia ilibainika kuwa leseni ilitumika kama chanzo cha mapato badala ya chombo cha kudhibiti biashara.

Ripoti ya Benki ya Dunia kuhusu "Easy of Doing Business 2010" kwa Zanzibar ilikuwa ni ripoti ya kwanza inayohusu udhibiti wa mazingira ya biashara na leseni katika uchumi wa visiwa vidogo. Ripoti ya "Doing Business" ya mwaka 2010 iliiweka Zanzibar namba 155 kati ya nchi 183 kwa urahisi wa kufanya biashara kwa kuzingatia mfumo wa udhibiti ulioainishwa na viashiria mbalimbali. Kwa urahisi wa kuanzisha biashara, kulinda wawekezaji, kupata mikopo, na kufunga biashara.[12]

Aidha, Wizara ya Biashara na Viwanda imekuwa ikifanya marekebisho ya usajili wa biashara na kurahisisha utaratibu wa utoaji leseni Zanzibar tangu mwaka

[11] Programme Management Unit, 'Property and Business Formalisation Programme, Vol. 5, Business Formalisation Reform Packages and Outline for Zanzibar'.
[12]World Bank (2010) "Doing Business in Zanzibar 2010" A Co publication of the World Bank and the International Finance Corporation, inapatikana https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/13439/74678.pdf?sequence=1&isAllowed=y

2013. Katika kufanya marekebisho ya leseni Serikali ilifanya utafiti kuhusu "Uchambuzi wa Udhibiti wa Leseni za Biashara 2011". Utafiti huo umebaini kuwa mfumo wa kisheria wa utoaji leseni unasababisha wingi wa leseni na tozo kutokana na idadi ya sheria, kanuni na sheria. Baadhi ya sheria zimepitwa na wakati na haziakisi hali ya sasa ya kudhibiti biashara.

Mbali ya marekebisho yaliyofanywa, mageuzi hayo hayakuweza kupunguza kwa kiasi kikubwa tatizo la usimamizi, kutokana na wafanyabiashara wengi kufanya kazi nje ya uchumi rasmi ambapo bila ya kuwa na misingi mizuri ya kisheria.[13]

Jitihada za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuimarisha biashara na kutilia mkazo katika sekta ya biashara katika Serikali ya Awamu ya 8 zinaendelea na dhamira njema ya kukuza Sekta za Biashara na Viwanda hapa Zanzibar inaimarishwa ili kuwaletea wananchi maendeleo zaidi ya kiuchumi.[14]

### 1.3 Hadidu rejea

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeandaa ripoti hii kwa kufuata hadidu rejea zifuatazo ambazo zitaweka muelekeo mzuri wa usimamizi wa leseni:

(a) Kufanya tathmini ya utaratibu uliowekwa katika sheria Nam. 3 ya mwaka 1983 katika utoaji wa leseni za biashara.

[13] Programme Management Unit, 'Property and Business Formalisation Programme, Vol. 5, Business Formalisation Reform Packages and Outline for Zanzibar'

[14] Rais wa Zanzibar na mwenyekiti wa Baraza La Mapinduzi Dr. Hussein Ali Mwinyi, katika uzinduzi wa Baraza la kumi la Wawakilishi tarehe 11 Novemba, 2020.

(b) Kuangalia uzoefu wa nchi mbalimbali kuhusiana na masuala ya usimamizi wa leseni za biashara na kwa namna gani uzoefu huo unaweza kuisaidia Zanzibar.

(c) Kuangalia Sera na sheria mbalimbali za Zanzibar zinazohusiana na usimamizi au utoaji wa leseni za biashara.

(d) Kupitia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo inahusiana na leseni za biashara na kuona ni kwa namna gani zinaweza kusaidia katika marekebisho ya sheria hii.

(e) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisera na kisheria kwa lengo la kupunguza au kuondosha kabisa changamoto zilizopo katika utoaji na upatikanaji wa leseni za biashara.

## 1.4 Malengo ya Utafiti

Lengo la kufanya utafiti huu ni kuangalia mapungufu ya Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983 na kupendekeza marekebisho yake Serikalini. Mapendekezo hayo yatazingatia:

(a) Kupendekeza utaratibu wa kisheria ili kuziwezesha taasisi za Serikali ziweze kusimamia shughuli za utoaji wa leseni kwa ufanisi zaidi;

(b) Kupendekeza utaratibu utakaowawezesha wafanyabiashara waweze kufanya biashara kwa haraka na ufanisi;

(c) Kusaidia upatikanaji wa huduma na bidhaa kwa wananchi;

(d) Kuwezesha Serikali kufanya mawasiliano ya kibiashara kuzingatia misingi ya utawala bora.

## 1.5 Tamko la Tatizo la Utafiti

Suala la usimamizi wa leseni za biashara ni eneo muhimu linalosaidia kuendeleza uchumi na kupunguza umasikini kwa wananchi. Eneo la leseni lina haja ya kuratibiwa na kusimamiwa vizuri zaidi ili kutambua leseni halisi zinazotolewa, vigezo na masharti ya leseni, mchango wa wafanyabiashara wa sekta mbalimbali katika Pato la Taifa, umiliki wa biashara zilizopo kwa mujibu wa sekta zilizowekwa kiuchumi. Utaratibu huu unatakiwa kutambua mamlaka za leseni na kurahisisha utaratibu ili utoaji wa leseni usikwaze maendeleo na malengo ya Serikali.

## 1.6 Njia za Utafiti

Katika utafiti huu njia zifuatazo zilitumika kukusanya maoni na kupata taarifa zilizoweza kufanikisha malengo yaliyokusudiwa katika utafiti.

(a) Kufanya mikutano na wadau walioainishwa kwa ajili ya kutoa maoni.

(b) Kuhoji baadhi ya wadau mbali mbali wakiwemo wataalam wa sekta zinazotoa leseni, ruhusa na vibali vya biashara.

(c) Kupitia Sheria mbalimbali na rejea ambazo zinazungumzia masuala ya leseni za biashara.

## SURA YA PILI

## 2.0 DHANA YA LESENI ZA BIASHARA

### 2.1 Utangulizi

Mabadiliko katika mazingira ya kijamii na kiuchumi na masuala yanayoendelea kwa kasi ya kiteknolojia na kijamii yanahitaji sheria sahihi za kudhibiti biashara; kutokana na ukweli kwamba biashara kulingana na taarifa ambayo inaweza kupatikana na kutumika. [15]

Kwa upande mwengine, kwa wamiliki wa biashara na wateja wengine wasiwasi mkubwa unabakia umuhimu wa leseni za biashara na kiungo chao cha usajili na urasimishaji wa biashara, hata hivyo kuna umuhimu kwa Serikali wa kutambua iwapo biashara inaendeshwa kisheria.

Suala la leseni linahusisha pia makubaliano, au mkataba, na baadhi kuruhusu matumizi ya alama ya biashara, hakimiliki, au siri ya biashara kwa madhumuni fulani. Leseni inashughulikia shughuli zote halali zinazofanywa wakati wa biashara iwe leseni ya binafsi au watu wengine kwa niaba yake. [16]

Kwa upande mwengine, kwa wamiliki wa biashara na wateja wengine wasiwasi mkubwa unabakia umuhimu wa leseni za biashara na kiungo chao cha usajili

[15] *Doing Business 2016 Measuring Regulatory Quality and Efficiency*, 3th edition," p. 9, World Bank Group Comparing Business Regulation for Domestic Firms in 189 Economies
[16] https://ij.org/activism/legislation/model-legislation/model-economic-liberty-law-1/

na urasimishaji wa biashara.[17] Wachuuzi, wakandarasi na muhimu zaidi Serikali inahitaji kujua kwamba biashara inaendeshwa kisheria.[18]

Katika suala hili leseni inaweza kuwa makubaliano, au mkataba, kuruhusu matumizi ya alama ya biashara, hakimiliki, hataza, au siri ya biashara kwa madhumuni fulani.[19]

### 2.2 Maana ya biashara

Biashara ni dhana ya msingi ya kiuchumi inayohusisha ununuzi na uuzaji wa bidhaa na huduma, pamoja na fidia inayolipwa na mnunuzi kwa muuzaji, au kubadilishana bidhaa au huduma kati ya wahusika.[20] Biashara ni kitendo au mchakato wa kununua, kuuza, au kubadilishana bidhaa, ama kwa jumla au rejareja, ndani ya nchi au kati ya nchi.[21]

Biashara kwa ujumla inamaanisha ubadilishanaji wa bidhaa na huduma, mara nyingi kwa malipo ya pesa. Biashara inaweza kufanyika ndani ya nchi, au kati ya taifa moja na jengine. Kwa biashara ya kimataifa, nadharia ya faida linganishi inatabiri kuwa biashara ni ya manufaa kwa pande zote.

Biashara ya kimataifa inaruhusu watumiaji na nchi kuoneshwa bidhaa na huduma ambazo hazipatikani katika nchi zao. Takriban kila aina ya bidhaa

---

[17] John Willey & Sons Australia Ltd, *Mohan Dhall (contributing author)*; *Business Studies in Action, Preliminary Course*; Stephen Chapman, Natalie Devenish 3rd Edition, p. 68

[18] https://www.andrewsarbenz.com/business-attorney-tacoma-business-licsense

[19] Peter Stimpson and Alex Smith *Business Management for the IB Diploma 978-1-107-46437-7*, Second Edition, Cambridge University Press 2015, p.3.

[20]https://www.investopedia.com/terms/t/trade.asp

[21]https://www.dictionary.com/browse/trade

inaweza kupatikana kwenye soko la kimataifa: bidhaa kama vile chakula, nguo, vipuri, mafuta, vito, divai, akiba, sarafu na maji. Huduma pia zinauzwa: utalii, benki, ushauri, na usafirishaji. Bidhaa ambayo inauzwa katika soko la kimataifa ni mauzo ya nje, na bidhaa inayonunuliwa kutoka soko la kimataifa ni ya kuagiza kutoka nje. Biashara yoyote inahitaji leseni ili iweze kufanyika katika sehemu fulani. Leseni ya biashara ni leseni tu au cheti kinachohitajika kwa biashara au mtu binafsi kufanya shughuli fulani. Biashara pia inatumia rasilimali kukidhi mahitaji ya wateja kwa kutoa bidhaa au huduma wanayodai.[22]

## 2.3 Leseni ya biashara

Leseni ya biashara ni hati au cheti ambacho hutoa ruhusa kwa mwombaji (mtu anayetaka kufungua biashara) kuanza biashara fulani katika eneo fulani.[23] Leseni ni mkataba unaofungwa kisheria ambao unamruhusu mtu kufanya, kumiliki, kutekeleza jambo au kutumia huduma kulingana na masharti yaliyotolewa. Leseni hutolewa kwa watu na mamlaka husika. Leseni ni muhimu katika kutoa ufahamu wa udhibiti wa shughuli mbalimbali, na kusaidia jamii kushiriki katika shughuli hizo.

Leseni ya biashara ni cheti kilichotolewa kwa mwombaji anayetaka kufungua biashara inayomruhusu kuanza biashara, leseni hii inaruhusu mwombaji kuanza na kuendesha biashara kwa kuzingatia taratibu zilizowekwa. Ikiwa mwombaji anataka kuanza biashara nyengine tofauti na ile iliyotajwa katika

---

[22] Peter Stimpson and Alex Smith *Business Management for the IB Diploma 978-1-107-46437-7*, Second Edition, Cambridge University Press 2015, p.3.
[23] Trade License- Category, Eligibility, Registration, FAQs (taxguru.in)

maombi ya leseni ya biashara, atalazimika kuitenganisha kwa kuiombea leseni yake. Leseni ya biashara ina maana tu kama idhini au ruhusa iliyotolewa kwa mwombaji kuanza biashara iliyotajwa.[24]

## 2.4 Umuhimu wa leseni

Lengo la leseni ni kutoa umiliki kisheria,[25] leseni inatoa tu haki fulani kwa maudhui, kwa mujibu wa masharti fulani, ambapo uuzaji halisi unaelezwa, na kuweka ukomo wa haki za mwenye kumiliki biashara hiyo.[26]

Mbali na umuhimu wa leseni kama ilivyoainishwa katika sehemu ya utangulizi; malengo ya leseni za biashara yameundwa ili kupunguza au kuzuia matumizi ya soko na kulinda maslahi ya umma; hata hivyo malengo mapana ni pamoja na; kulinda au kuimarisha usalama wa taifa, na sera ya biashara.[27]

Leseni huthibitisha uwezo wa watu binafsi katika biashara, biashara na taaluma; kuhakikisha usalama na ufanisi wa bidhaa na taratibu; kuhimiza au kuzuia ushindani katika sekta maalum; kuzuia udanganyifu na kuhakikisha utulivu wa kifedha katika shughuli za biashara; kudhibiti upatikanaji wa soko au maendeleo au utekelezaji wa teknolojia mpya; kukuza utumiaji wa uwajibikaji wa bidhaa za asili na kusaidia katika ukusanyaji wa mapato[28] Leseni

[24] https://www.lendingkart.com/blog/trade-licens

[25] Cross W M, "Restoring the Public Library Ethos: Copyright, E-Licensing, and the Future of Librarianship," Law Library Journal (2012) 104:2

[26] Cichocki KM, "Unlocking the Future of Public Libraries: Digital Licensing that Preserves Access" (2007-2008) 16 University of Baltimore Intellectual Property Law Journal 29 ukurasa wa 38.

[27] Steve Suranovic (2010): *International Trade: Theory and Policy*; George Washington University Saylor Foundation; p.493

[28] https://mn.gov/deed/business/starting-business/legal-regulatory/

husaidia katika kuweka mfumo wa kisheria, na kujumuisha utendaji na mawasiliano kwa umma.[29]

## 2.5 Viwango vya leseni

Kimsingi viwango vya leseni vinatafautiana, kuna leseni zenye masharti maalum na zenye masharti ya jumla kulingana na ukubwa au unyeti wa biashara inayofanywa,[30] tofauti hii inaoneshwa kwa viwango kadhaa.

Maudhui ya kidijitali kwa mfano yanapopewa leseni, mtoa leseni anakuwa na udhibiti kamili wa kisheria kuyahusu.[31] Maudhui ya kidijitali kwa ujumla hayahifadhiwi kikawaida, na hubeba hatari kwamba maudhui yaliyoidhinishwa yanaweza kukosa kupatikana kwa wateja wao kutokana na masuala ya kiufundi au mengine kwa upande wa mtoa leseni.[32]

## 2.6 Muda wa leseni

Tafiti kadhaa zinaonyesha kuwa leseni nyingi zinatolewa kwa muda mfupi na muda mrefu na hivyo hazihakikishi usalama wa muda mrefu wa ufikiaji wa makusanyo yaliyopatikana katika mfumo wa kidigitali.[33]

---

[29] Gervais D, Maurushat A, "Fragmented Copyright, Fragmented Management: Proposals to Defrag Copyright Management" (2003) Canadian Journal of Law and Technology 2, 15 ukurasa wa 10

[30] Robert Goldscheider and Alan H. Gordon Editors, (2006) *Licensing Best Practices, Strategic, Territorial, and Technology Issues*, John Wiley & Sons, Inc, Wiley

[31] Hinkes, 2007:709 Hinkes E M, "Access Controls in the Digital Era and the Fair Use/First Sale Doctrines" (2006-2007) 23 Santa Clara High Technology Law Journal 685

[32] Squitieri, Mauro (2012) *Refusals to License Under European Union Competition Law After Microsoft*, Journal of International Business and Law: Vol. 11: Issue. 1, Article 4.

[33] Fred H. Cate, 2002. "The commodification of information and the control of expression," *Amicus Curiae* (Journal of the Institute of Advanced Legal Studies, School of Advanced Studies, University of London), volume 43, pp. 3–7.

Ili biashara ifanye kazi katika nchi yoyote linahitaji leseni iliyotolewa na mamlaka ya Serikali. Leseni ni ruhusa inayotolewa kwa mtu baada ya maombi kwa mamlaka inayosimamia kufanya shughuli fulani kwa taratibu zilizowekwa, kwa kawaida baada ya kukidhi masharti fulani ikijumuisha malipo ya ada iliyowekwa.[34]

Kwa kawaida muda pia hutegemea mwenye leseni kutoa kwake maelezo ya shughuli zake na eneo la biashara, vipengele vyengine vinaweza kujumuisha idadi ya wafanyakazi, mfumo wa biashara, wanachama na hisa zilizopo kama wapo.[35]

## 2.7 Usimamizi wa leseni

Serikali zinategemea leseni ili kudhibiti shughuli mbalimbali za binadamu, kuanzia taasisi za kibiashara na shughuli za kitaalamu pamoja na kufahamu biashara hatarishi na nyeti kwa mazingira ya nchi na eneo husika.[36] Kabla ya kutoa leseni, mwombaji analazimika kukidhi vigezo fulani, na amelipa gharama za leseni zilizoainishwa.[37]

Kuna aina mbalimbali za biashara zinazohitaji umiliki kuwa na leseni maalum, kwa mfano, unahitaji leseni ili kuhakikisha kuwa biashara imesajiliwa na kupewa leseni ipasavyo; unahitaji leseni ya biashara ili kuhakikisha kuwa

[34] Gellhorn W (1956). Individual Freedom and Governmental Restraints. B aton Rouge: Louisiana State University Press
[35] Antoniak M (1995). 21st Century Entrepreneur: How to Start a Home Business. New York: Avon
[36] Dreschle B (2001). Small-Scale Mining and Sustainable Development within the SADC Region, MMSD project of IIED, International Institute for Environment and development. Available at: https://www.scribd.com/document/91701845/Small-Scale-Miningand-Sustainable-Development-Within-the-SADC-Region
[37] Kampala Capital City Authority (KCCA) (2017), Trading Licence (Assessment, Payment & Issuance). Available at: https://www.kcca.go.ug/uDocs/Trade_Licence_FAQs.pdf

biashara yako kifedha ipo katika hadhi nzuri. Leseni pia inatoa utekelezaji wa masuala muhimu ya sera za nchi.[38]

## 2.8 Kanuni ya Usawa na Uwiano (equity and proportionality)

Usawa na uwiano katika utoaji wa leseni ni dhana ya msingi na inahakikisha vipengele vya usawa ndani ya muundo wa soko, na uwiano wa biashara na kuondoa tafauti za kibaguzi. [39]

Hivyo sheria za leseni zinatakiwa kuhakikisha na kuanzisha kanuni tofauti zinazotumika kwa biashara; taratibu za maombi; kanuni ya usawa na uwiano; uanzishwaji wa mfumo wa uwazi; na hatimaye tahadhari itachukuliwa ili kuhakikisha kuwa mamlaka inafikia maamuzi.[40] Kwa msingi huu, sheria za ushindani huanzishwa kudumisha miundombinu ya soko shindani. [41]

Katika suala hili, mambo muhimu yanazingatiwa na kutumika;[42] ikiwemo madai ya kushughulikia utoaji leseni,[43] kuhakikishiwa kwamba hakuna kizuizi kwa mmiliki wa leseni, [44] ili kuondoa ubaguzi katika biashara na kuwafanya wenye leseni kutimiza malengo yanayotakiwa.[45]

---

[38] Khadija Shamte Mzee "Setting up A Business in Zanzibar: The Legal Requirements," LYBL Volume 8 -2018

[39] Anderman, Steven & Schmidt Hedvig, *EU Competition Law and Intellectual Property Rights: The Regulation of Innovation, 2011*, 2nd edition, Oxford University Press, Oxford; p. 25-26

[40] World Bank Group *Doing Business 2016 Measuring Regulatory Quality and Efficiency*, 13th edition, Comparing Business Regulation for Domestic Firms in 189 Economies, World Bank Group

[41] Hildebrand, Doris, *The Role of Economic Analysis in the EC Competition Rules, 2009*, 3rd edition, Kluwer Law International

[42] A legal doctrine which describes a particular type of claim of monopolization made under competition laws. In general, it refers to a type of anti-competitive behavior in which a firm with market power uses a "bottleneck" in a market to deny competitors entry into the market

[43] https://en.wikipedia.org/wiki/Essential_facilities_doctrine

[44] MCI v. AT&T, 708 F.2d1081, 1132 (7th Cir. 1983); Hecht v. Pro-Football, Inc., 570 F.2d 982, 992-93 (D.C. Cir. 1977), (see, e.g. Commission Decision 92/213/EEC, 1992 O.J. (L 96) 34 (British Midland v. Aer Lingus

[45] *Inc. v.Trinko*, 124 Ct. 872, 881 (2004)

## 2.9 Vyombo vya kutoa leseni

Vyombo vya kutoa leseni ni eneo jengine muhimu ambalo linahitaji kuwekwa wazi katika sheria. Muundo na wajumbe ni muhimu sana kiasi kwamba kuna makundi mengi ya biashara na wakati mwengine, kuwepo kwa maoni yanayopingana kuhusu sifa ya utendaji katika biashara hizo na kupoteza umuhimu wake.[46]

Vyombo hivi vinatakiwa kuhakikisha biashara inaimarika kwa maslahi ya taifa, kulinda haki miliki na biashara za kitaaluma. Vyombo vya kutoa leseni au mabaraza yanatakiwa kuwa na wajumbe wenye sifa stahiki ili kubaini kama mwombaji anafaa kwa taaluma au biashara husika.[47]

Vyombo hivi na Mabaraza yatakuwa na uwezo wa kuweka vigezo mbalimbali ambavyo waombaji wanapaswa kukidhi au kudumisha wakati wa kuomba leseni. Baraza kwa kawaida huhitajika kutoa notisi kwa wakati unaofaa ya kukataliwa leseni, au kusimamishwa au kufutwa kwa leseni.[48] Katika baadhi ya matukio, Baraza linaweza kupitia taratibu na taratibu za mamlaka ya utoaji leseni.[49]

Baraza lina mamlaka ya kuhitaji mamlaka yoyote ya leseni au mtu kutoa taarifa, kutoa maagizo kwa mamlaka yoyote ya kutoa leseni kuhusu sera, kufanya

---

[46] Akman Pinar, *The Concept of Abuse in EU Competition Law: Law and Economic Approaches*, 2012, Hart Publishing, Oxford ukurasa wa 53

[47] *In the Heart of Atlanta Motel v. United Sates* 379 U.S. 241, 85 S.Ct.348 13 L.Ed.2d 258 (1964) the supreme Court has interpreted the commerce clause to mean that the national government has the exclusive authority to regulate business

[48] Pedro A. De Miguel Asensio: *The Law Governing International Intellectual Property Licensing Agreements (A Conflict of Laws Analysis)*, Research Handbook on Intellectual Property Licensing Cheltenham, Edward Elgar Publishing, 2013, pp. 312-336

[49] Paul Dobson and Rob Stokes: (2012) *Commercial Law*, Sweet and Maxwell London, p. 374

mapitio ya sheria, na kupitia upya masuala ya sera.[50] Baraza lina mamlaka ya kipekee ya kudhibiti biashara ambayo inaathiri kwa kiasi kikubwa biashara na biashara miongoni mwa mataifa kupitia sheria inayowekwa.[51]

Baraza lina uwezo wa kupitia na kupendekeza marekebisho ya ada zinazolipwa kwa ajili ya leseni, kuandaa hatua na njia za kutathmini utendakazi wake na kuweka rejista za leseni, vibali na idhini zinazohitajika kwa ajili ya biashara zinazoweza kufikiwa na umma.[52]

Kwa kuzingatia mamlaka ya Baraza; Sheria inatakiwa kuweka masharti kulingana na mfumo wa leseni unasimamiwa; lakini pia kuweka mamlaka ya uchunguzi kila sekta ya biashara.

---

[50] David McKitterick (1992) *A History of Cambridge University Press*: Volume 1, Printing and the Book Trade in Cambridge, 1534 -1698 printed by the Syndicate of the University of Cambridge

[51] Paul Dobson and Rob Stokes: (2012) *Commercial Law*, Sweet and Maxwell London, p. 374

[52] *Protecting Your Trademark; Enhancing Your Rights through Federal Registration*; p.8, BASIC Facts About Trade mark, United States Patent ND Trademark Office; available at https://www.uspto.gov/sites/default/files/documents/BasicFacts.pdf

## SURA YA TATU

## 3.0 UCHAMBUZI WA SERA NA SHERIA

### 3.1 Sera

Sera inayosimamia Sheria ya leseni za biashara Zanzibar ni Sera ya biashara ya Zanzibar ya mwaka 2006 (Trade Policy). Sera hii ina lengo la kuweka mazingira bora ya biashara ambayo yatapelekea urahisi wa ufanyaji biashara na kuondoa urasimu wakati wa upatikanaji wa huduma. Mbali ya Sera za biashara zipo sera nyengine mbalimbali ambazo zimezingatia uwepo wa biashara na kuweka mazingira mazuri ya ukuzaji wa uchumi wa Zanzibar.

#### 3.1.1 Dira ya Maendeleo ya 2050- 2050

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imeanzisha taasisi kadhaa za kusaidia maendeleo ya biashara na uanzishaji wa viwanda kupitia biashara ndogo ndogo, ndogo na za kati (MSMEs), zinazohusu ubora wa bidhaa na ulinzi wa watumiaji. Ingawa viwanda ni chanzo muhimu kwa biashara, uhusiano kati ya sekta hizi mbili unahitaji kuboreshwa zaidi. Zanzibar ina uwezo wa kuharakisha ukuaji wa uchumi, kukuza wafanyakazi wenye ujuzi na ujuzi wa kati na kupanua vyanzo mbalimbali vya mapato kwa kubadilisha faida yake ya kulinganisha katika rasilimali za bahari na kilimo kuwa faida yakatika viwango vya ushindani.

Kuna nafasi ya kuongeza thamani na kuboresha uwiano wa kibiashara wa Zanzibar kwa kufanya biashara ya karafuu, uvuvi, mafuta, mwani na maziwa kwa njia ya makopo, kukausha, kusafisha. Sekta nyengine muhimu zenye uwezo wa kuuza nje ni pamoja na kusafisha chumvi, vito, bidhaa za mbao, vifaa vya

elektroniki na kazi za mikono, zikitumia kwa pamoja kati ya utalii, kilimo na biashara.

Miongoni mwa matarajio ya Dira ya mwaka 2050 kwa upande wa biashara ni kama yafuatayo:

(i) Kuwa na viwanda vilivyostawi vyema na vinavyoweza kuingia katika ushindani katika masoko ya ndani na nje ya nchi kupitia uingizwaji wa bidhaa na mwelekeo wa mauzo;

(ii) Mpango endelevu wa uendelezaji viwanda unaolenga katika kuongeza kiasi cha mauzo ya nje na ongezeko la thamani ya utengenezaji kupitia mchanganyiko wa mtaji na tasnia inayohitaji nguvu kazi kubwa kulingana na faida linganishi kama ifuatavyo: Mbinu ya kimkakati ya utengenezaji wa bidhaa nyepesi katika usindikaji wa kilimo unaoendana na mauzo ya nje.

(iii) Mfumo madhubuti wa sera ya viwanda na biashara ambayo hupitia mara kwa mara viwanda vinavyolengwa pamoja na mauzo ya nje na vivutio vyake vya uwekezaji kulingana na sekta zinazoibuka, mwelekeo wa soko la kimataifa na mabadiliko ya faida linganishi;

(iv) Kuratibu taratibu za biashara ndani ya Zanzibar, kati ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya muungano ya Tanzania, katika Afrika Mashariki na Eneo Huria la Biashara, kupitia Shirika la Biashara Duniani na mengineyo.

### 3.1.2 ILANI YA CCM 2020-2015

Ilani ya CCM fungu 156, imeelekeza kutekelezwa Sera mpya ya Biashara, sera ya uendelezaji viwanda vidogo na vya kati na kuwapatia mafunzo ya mitaji na

huduma za kiufundi wajasiriamali wadogo na wakati (SMEs).[53] Ilani katika imeeleza katika fungu 156 (h) kufanya utafiti wa utoaji wa leseni na kuandaa misingi, vigezo, miongozo, taratibu fupi kwa ajili ya kurahisisha upatikanaji wa leseni.[54]

### 3.1.3 Sera ya Biashara ya mwaka 2006

Sera ya sasa ya Biashara, ingawa imetangulia, imezingatia malengo ya Dira ya Maendeleo ya Zanzibar 2020. Sera hii inalenga kuwezesha uendeshaji mzuri wa shughuli zote zinazohusiana na biashara Zanzibar, kuimarisha ushiriki wa sekta binafsi katika biashara ya bidhaa na huduma na kuhakikisha kwamba mipango na hatua zinazohusiana na biashara chini ya sera tofauti za kijamii na kiuchumi za Serikali zinawiana na kutekelezwa kwa pamoja. Sheria, kanuni na taratibu zinazohusiana na biashara zitawekwa vizuri zaidi ili kutimiza madhumuni yaliyokusudiwa na kuafiki mwelekeo mpya wa shughuli za biashara.[55]

Sera hii inatambua na imejumuisha sekta muhimu ikiwemo biashara huru na inayozingatia viwango, sekta za afya, elimu, na kusisitiza uwepo wa usawa katika biashara.[56] Aidha Sera imeeleza kuzingatiwa masuala ya mazingira na utawala Bora katika usimamizi wa biashara,[57] usimamizi wa sekta za viwanda, kilimo, na miundombinu ikiwemo mawasiliano, usafiri, maji safi na ardhi.[58]

[53] Ukurasa wa 210-211
[54] Ukurasa wa 211
[55] Kifungu cha 44, mstari wa 94
[56] Ukurasa wa 4-6
[57] Kifungu cha 1.6.4 na 1.6.5 ukurasa wa 7-8
[58] Kifungu cha 1.7-1.9 cha Sera

Aidha masuala ya kusimamia utalii na sekta za fedha yametambuliwa na kuwekewa mwongozo maalum.[59]

Sera imetambua na kubainisha leseni za uingizaji na usafirishaji bidhaa,[60] biashara ya EPZ na Maeneo Huru ya Biashara.[61] Sera ya biashara inaendana na malengo ya Biashara ya Shirika la Biashara Duniani (WTO) na kubainisha masuala muhimu ya kuunganishwa katika uundaji wa biashara ya kitaifa. Masuala haya ni pamoja na huduma za biashara za kitaalamu na ICT; ujenzi na uhandisi; huduma za usambazaji; elimu; mazingira; huduma za Kifedha; utalii na huduma za Usafiri; na huduma ya Burudani. Aidha Sera imeweka wazi kutambuliwa na utumikaji wa Mikataba ya Kimataifa na Kikanda katika biashara.[62] Kwa kumalizia Sera hii imetoa mwongozo wa majukumu ya taasisi mbali, ikiwemo sekta binafsi na taasisi za Serikali na jukumu lao katika usimamizi na uendelezaji wa biashara nchini.[63]

### 3.1.4 Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005

Sera ya uwekezaji ya Zanzibar ni Sera ya mwaka 2005 ambayo miongoni mwa malengo yake makuu ni kuimarisha ushiriki wa Zanzibar katika makubaliano ya kibiashara ya kikanda na kimataifa. Sera hii imeeleza nia ya kukuza masoko ya mauzo yake nje na kuhamasisha uwekezaji unaolenga kuuza bidhaa nje ya Zanzibar na kwa thamani kubwa. Vile vile kuwezesha ushiriki wa sekta binafsi ya kitaifa katika biashara kupitia ubia.

[59] Ukurasa wa 15 wa Sera
[60] Kifungu 5.3.3 paragraph 113
[61] Kifungu 5.5.2 paragraph 142
[62] Kifungu 5.6-5.6.1 (paragraph 151-153)
[63] Kifungu 7 na 7.1 (paragraph 169-179)

Sera hiyo iliundwa ili kuvutia uwekezaji wa moja kwa moja wa kigeni (FDI) ndani ya Zanzibar na kufanya mkakati makini wa utangazaji na mabadiliko makubwa ya sera na mfumo wa uendeshaji wa FDI kulingana na viwango vya kimataifa. Sera imeeleza haja ya kuvutia uwekezaji katika sekta muhimu kama vile kilimo, uvuvi, SMEs, viwanda, biashara na Utalii.

Baadhi ya mikakati muhimu ya Sera ya uwekezaji ni pamoja na uwazi, uwajibikaji na utawala wa sheria, mfumo wa usimamizi unaohakikisha ufanisi, mwitikio na uadilifu, na kuhakikisha kuwa Wizara, taasisi na sekta binafsi zinafanya kazi kwa karibu na wawekezaji kwa ajili ya kuchochea uchumi.

Sera hiyo inahitaji kuanzishwa kwa mfumo wa fedha wenye ufanisi unaowezesha, kuvutia, kuimarisha na kupanua makampuni ya mitaji ya ubia, makampuni ya fedha na makampuni ya bima, miongoni mwa mengine, kupitia uwekezaji na uwekezaji wa umma, binafsi wa ndani na nje, na inatoa wito wa kuweka vivutio vinavyofaa katika kukuza biashara nje ya nchi na masoko ya mitaji.

### 3.1.5 Sera ya Wajasiriamali Wadogo na wa kati Zanzibar ya mwaka 2005

Sera hii inagusa lengo la kutoa fursa za ajira, mapato na uzalishaji mali na kupunguza umasikini. Sera ya SME inatambua kwamba maendeleo ya sekta ya SME inahitaji uingiliaji kati mahususi katika nyanja mbalimbali za Serikali na ukuzaji wa uwezo kwa sekta binafsi na ya umma kwa mujibu wa ilivyoelezwa sera na malengo ya kitaifa.

Sera inatetea mazingira mazuri ya biashara, utunzaji na uendelezaji wa biashara ndogo ndogo ili kuleta tija kwa wananchi. Sera inatoa kipaumbele maalum cha utekelezaji wa hatua za udhibiti na matumizi ya mbinu mbadala. Hatua zinazohusiana na kuongezeka kwa uhamasishaji juu ya uzalishaji safi, ufanisi na usimamizi wa teknolojia mbadala kwa SMEs.

### 3.1.6 Sera ya Ajira Zanzibar 2009

Lengo kuu la Sera ya ajira ya Zanzibar inaelekeza katika kuongeza tija na kupata ajira zenye tija, faida na zilizochaguliwa kwa hiari ili kupunguza kasi ya ukosefu wa ajira na viwango vya chini vya utendaji kazi,[64] kuongeza tija katika uzalishaji na kupunguza kiwango cha umasikini kama ilivyoainishwa katika MKUZA.

Sera hii ina malengo ya kuongeza kasi ya ukuaji ya uchumi na uwekezaji makini wa rasilimali katika sekta kuu za utoaji wa ajira kama vile viwanda vidogo na vya kati katika sekta za kilimo, utalii, utamaduni, michezo, ubaharia, miundombinu, uzalishaji na sekta za huduma za jamii na uchumi. Aidha lengo jengine ni kujenga mazingira bora yatakayowezesha mabadiliko ya sekta ya uchumi isiyo rasmi ili kuweza kuwa sekta rasmi yenye tija na yenye kuhimili ushindani.

### 3.1.7 Sera ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2012

Sera inakuza huduma bora na zenye ufanisi katika kufikia malengo ya utawala bora. Kwa hiyo, lengo la Sera ni kuhakikisha kwamba uanzishwaji wa Serikali ya mitaa inayowajibika ambayo ina uwezo wa kutoa huduma bora za msingi

[64] Sera ya Ajira ya mwaka 2009

kwa wananchi na kulinda riziki zao, ambazo ni uti wa mgongo wa maendeleo ikiwemo biashara.

Mfumo wa sera unatoa msingi wa sekta ya umma na ya kibinafsi na ushirikiano unaosaidia kuwepo ushindani na ufanisi wa huduma na kuunda mazingira mazuri zaidi kwa miradi ya PPP ambayo pia ni muhimu kwa maendeleo ya Zanzibar. Lengo la jumla la sera ni kufikia ubora wa maisha na kiwango cha maisha kwa Wazanzibari wote kupitia usimamizi na maendeleo ambayo lazima yawe na mfumo mzuri wa biashara.

### 3.1.8 Sera ya Mazingira ya mwaka 2014

Sera ya Mazingira ya mwaka 2014 inasimamia mazingira hapa Zanzibar. Masuala ya mazingira ni ya msingi kwa Serikali yoyote na yanapaswa kujengwa katika mfumo wa Sera ya maendeleo ili kuhakikisha kuwa mazingira yanalindwa na maendeleo ya kiuchumi yanafanyika kwa njia endelevu ya mazingira. Malengo ya Sera hiyo kwa malengo ya biashara ni uondoaji wa vizuizi vya kibiashara juu ya uagizaji wa teknolojia safi, isiyochafua mazingira, na teknolojia ya kijani kibichi.

### 3.1.9 Sera ya Mafuta na Gesi Zanzibar (Upstream) ya mwaka 2016

Zanzibar hadi sasa, haina utawala wake wa mafuta na gesi na kwa hiyo hakuna utaratibu wowote wa maamuzi la Utoaji wa Leseni na Mikataba. Sera hii inaelleza kwamba Serikali inapaswa kuhakikisha kuwa haki za kipekee za utafiti, maendeleo na uzalishaji wa mafuta ya petroli zinatolewa kwa wawekezaji wakubwa na wa kuaminika wenye manufaa ya pande zote mbili na kwa maslahi ya nchi, pamoja na uanzishwaji wa ukubwa kamili wa vitalu vya

mafuta na gesi kwa ajili ya kupata leseni utakuwa kipaumbele kuleta ufanisi wa kiutendaji katika eneo hili.

Sera imeainisha mambo muhimu yafuatayo ya kipaumbelem ikiwemo umiliki wa Rasilimali ya Mafuta na Gesi kwa Wananchi wa Zanzibar, uhakikisho wa matumizi endelevu ya mapato ya mafuta na gesi kwa wananchi wa Zanzibar; ushiriki kamili wa Serikali katika mnyororo wa thamani wa mafuta na gesi, uwazi kamili katika kusimamia masuala ya mafuta na gesi chini ya mfumo mpana wa utawala wa sheria, kuzuia hatua dhidi ya changamoto zinazotokana na masuala ya mafuta na gesi kulingana na kanuni bora ndani ya majukumu ya kisheria ya Kitaifa na Kimataifa na uundaji wa mfumo wa kisheria na udhibiti unaosimamia shughuli za mafuta ya petroli.[65]

### 3.1.10 Sera ya Afya Zanzibar ya mwaka 2010

Dira ya Sera ni kuwa na idadi ya watu wenye afya njema, yenye huduma za afya zinazotegemewa, zinazofikiwa na zinazolingana. Dhamira ya sera ni kuhakikisha kwamba Wazanzibari wote wanapata haki yao ya kupata huduma bora za afya na kutokuathiriwa na bidhaa au huduma mbalimbali. Mbali ya mambo mengine, Sera hii imejikita katika mambo makuu yafuatayo: utoaji wa huduma za afya, huduma bora katika ngazi ya afya ya msingi; uwekezaji katika miundombinu ya afya; teknolojia mpya, aina mpya za utaalamu, na mikakati mengine.

### 3.1.11 Sera ya Kilimo Zanzibar ya mwaka 2000

[65] Kifungu cha 2.3 ukurasa wa 11 wa Sera

Sera ya Sekta ya Kilimo inataja umuhimu wa bidhaa za kilimo na biashara ya bidhaa hizo kama eneo muhimu katika uchumi wa Zanzibar.

Kutokana na kuongezeka kwa mahitaji, Sekta hii imekuwa muhimu sana, na ina athari hasi katika sekta ya kilimo. Mwelekeo wa sera ni jinsi ya kukuza unafuu na kimazingira ya kukuza uchumi na kuinua maisha ya Wazanzibari.

### 3.1.12 Sera ya Uvuvi Zanzibar ya mwaka 2000

Sera inatoa wito wa kukuza na kuendeleza ikolojia Kwa maendeleo ya uvuvi Zanzibar. Kuna leseni za uvui zimeainishwa na udhibiti wake ili kupunguza matumizi ya mbinu haribifu za uvuvi kama vile baruti ambayo pia inaharibu mfumo ikolojia wa baharini na kutishia uwezo wa kupata mazao ya kutosha ya baharini. Sera inataja masuala yanayohusiana na uhifadhi wa mazingira wa mifumo ya ikolojia ya baharini na wito kwa ongezeko la programu za elimu na uhamasishaji juu ya uhifadhi wa bahari na utekelezaji wa malengo ya Jumuishi. Biashara na Uvuvi wa viwanda pia umeangaziwa katika sera.

### 3.1.13 Sera ya Usalama wa Chakula Zanzibar ya mwaka 2008

Sera inatambua utekelezaji wa Mpango wa Matumizi ya Ardhi unachangia kwa kiasi kikubwa katika kushughulikia upatikanaji wa chakula na kuhakikisha biashara zinakuwa salama kwa mlaji. Sera imeipa jukumu Wizara kuhakikisha uwepo wa wa huduma na bidhaa safi kwa matumizi ya binadamu, na mifugo, na kuchangia katika utekelezaji bora wa sera katika kukuza maisha na kuhakikisha chakula na maji usalama.

### 3.1.14 Sera ya Usafiri Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Taifa ya Usafiri ya Zanzibar inaeleza hatua ya kuchukua kwa maendeleo ya sekta ndogo za usafiri wa baharini, anga na nchi kavu. Sera inashughulikia utaratibu wa leseni na mahitaji ya usafiri,vifaa vya kutoa huduma za usafiri, na usimamizi wa sekta ya usafiri ikiwa ni pamoja na kuendeleza mifumo ya usafiri na miundombinu. Sera inatambua haja ya kuhamasisha uwekezaji binafsi kupitia ubia kati ya sekta ya umma na binafsi katika ujenzi, uendeshaji na matengenezo ya bandari na miundombinu inayohusiana. Sera inakuza huduma za leseni na usajili wa wazi ndani ya bandari ya Zanzibar na kuruhusu raia wa kigeni kusajili meli zao Zanzibar.

Kuhusu masuala yanayohusiana na sekta ndogo ya usafiri wa anga, sera inasisitiza hitaji la kukuza viwanja vya ndege vya kibinafsi ili kusaidiana upanuzi uliopo wa miundombinu ya viwanja vya ndege vikubwa na huduma zikiwemo biashara mbalimbali.

### 3.1.15 Sera ya Asasi za Kiraia Zanzibar ya mwaka 2008

Mashirika ya Kiraia, hasa (NGOs) yanatambuliwa na Serikali kama chombo muhimu katika kuimarisha maendeleo ya kiuchumi na kijamii, na kukuza pato la Taifa na kupunguza umasikini.

### 3.1.16 Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006

Sera ya Elimu imeibuka ili kutekeleza malengo ya maendeleo ya kiuchumi ya kijamii katika sekta ya elimu. Maono ya Sera ni kuwa na elimu bora kwa jamii, kujitolea kujifunza na kukabiliana na changamoto za maendeleo. Sera inaelezea changamoto mpya ambazo mfumo wa elimu unakabiliwa hasa kutokana na ukombozi unaoendelea, utandawazi na mchakato wa ubinafsishaji na uchumi

hivyo kuna haja ya kuzingatia utolewaji wa leseni kwa taasisi ambazo zinalenga mikakati na mwelekeo wa Serikali.

### 3.1.17 Sera ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2013

Lengo la jumla la sera hii ni kutoa marejeleo mfumo wa maendeleo yenye usawa na endelevu wa sekta ya TEHAMA Zanzibar na kuwa msingi mkuu kwa sheria, mipango ya maendeleo na utekelezaji katika siku zijazo. Malengo mahususi ya Sera ya TEHAMA ya Zanzibar ni kuleta mabadiliko Zanzibar katika jamii inayotegemea habari, usawa na nafuu wa ICT; kuhakikisha kwamba ICT ni sehemu Ya programu za elimu ya kitaifa. Hii ni muhimu sana kwa maslahi ya Wazanzibari na taasisi za leseni zina haja ya kudhibiti na kuweka utaratibu mzuri katika usimamizi wa TEHAMA.

### 3.1.18 Sera ya Jinsia Zanzibar ya mwaka 2005

Kama ilivyoelezwa katika Sera ya Biashara, Sera hii inasisitiza usawa kati ya jinsia katika kijamii, nyanja za kisiasa na kiuchumi katika ngazi zote. Lengo la jumla ya Sera ni kutoa mfumo wa kitaifa wa kupanga, kutekeleza, kuratibu, kufuatilia na tathmini ya mikakati ya ujumuishaji wa jinsia, mipango yao ya utekelezaji na bajeti. Aidha, sera inatambua jukumu kubwa zaidi linalotekelezwa na wanawake katika eneo la biashara katika sekta zote na wana umakini mkubwa katika mapambano dhidi ya umasikini na utoaji wa huduma za msingi za kijamii.

### 3.1.19 Sera ya Usimamizi wa Maafa Zanzibar ya mwaka 2011

Sera ya Kukabiliana na Maafa Zanzibar inaweka utawala na taratibu za uendeshaji ili kujenga jumuiya zinazostahimili na kuimarisha matumizi na kupunguza maafa.

Katika kuzuia maafa, kupunguza, kujiandaa, na kukabiliana katika ngazi zote, Sera inazingatia viwango katika maeneo ya biashara ili kuondoa usumbufu wakati wa maafa na kusaidia maendeleo ya kijamii na kiuchumi. Sera pia inasisitiza juu ya ulinzi wa maeneo yanayotumika kwa huduma mbalimbali ikiwemo biashara, na kupunguza hatari na ajali. Umuhimu wa Sera unatakiwa kuzingatiwa wakati wa kutoa leseni za biashara.

### 3.1.20 Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014

Madhumuni ya jumla ya Sera ya Hifadhi ya Jamii ya Zanzibar ni kuanzisha mfumo mpana wa ulinzi wa kijamii unaokutana mahitaji ya usalama wa mapato, usimamizi wa huduma za kimsingi kwa Wazanzibari wote. Sera inazingatia ulinzi wa kijamii ambao utaboresha hali ya maisha Zanzibar kwa kupunguza umasikini, mazingira magumu na kunyimwa, kutoa ulinzi dhidi ya mshtuko, kuimarisha upatikanaji wa huduma muhimu, kuimarisha ushirikishwaji wa kijamii,na kukuza haki na fursa sawa kwa wote.

Sera inakubali kwamba Zanzibar imeendeleza nguvu Katika ukuaji wa uchumi, lakini faida hazijawafikia Zanzibar wote. Baadhi ya vikundi, kama vile wakulima wadogo na wavuvi wameachwa nyuma, huku makundi mengine hatarishi, kama vile wazee na watu wenye ulemavu, hawawezi kutumia fursa za kiuchumi. Hivyo katika utoaji wa leseni kuna haja ya kuzingaia mazingira

ambayo kila mmoja atafaidika nayo hasa katika maeneo ya huduma muhimu za biashara na kutoa elimu ya leseni kwa lengo la kuhamasisha makundi maalum.

## 3.2 Sheria zinazohusiana na Leseni za Biashara Zanzibar

### 3.2.1 Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983[66]

Sheria hii (Trade Licencing Act) ilikuja kwa lengo la kuziweka pamoja baadhi ya sheria zinazohusiana na mambo ya leseni za biashara na mambo mengine yanayohusiana nayo, aidha sheria ya leseni za biashara ya mwaka 1933 (The Trade Licencing Decree).

Sheria katika kifungu chake cha 2 imetafsiri biashara kuwa ni kufanya biashara za kibenki, Biashara za jumla, biashara za rejareja au fundi wa kazi za mikono kwa faida ya kibinafsi sehemu ya biashara Sheria imeweka wazi kwamba hakuna mtu atakayefanya biashara katika visiwa vya Zanzibar bila ya kuwa na leseni halali ya kufanya biashara hiyo. Leseni hiyo itaeleza kwa undani aina ya biashara itakayofanyika katika sehemu hiyo.[67]

Sheria hii katika kifungu chake cha 5 imetoa nafasi kwa baadhi ya biashara kufanyika bila ya leseni za biashara zikiwemo bidhaa za kilimo, biashara za mikono na mtu mwengine ambaye anasimamiwa na sheria nyengine kufanya biashara yake na mtu mwengine yeyote ambaye Waziri ataona inafaa kumtoa katika kukata leseni katika biashara yake anayofanya.

[66] Sheria Nam. 3 ya mwaka 1983
[67] katika kifungu cha 3

Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi anaweza chini ya Sheria hii kuanzisha Bodi ya leseni ya biashara[68] kwa madhumini ya kusimamia leseni za biashara. Bodi hiyo itaundwa na wajumbe wasiozidi 10 kama Raisi atakavyoona inafaa. Kazi kuu za Bodi hiyo ni kutoa maelekezo ya jumla au maalum kwa maafisa leseni[69](wanateuliwa na Waziri[70]) juu ya utekelezaji wa kazi zao. Vilevile Bodi itakuwa ni chombo cha rufaa kwa yeyote ambaye hataridhishwa na maamuzi ya afisa leseni au Kamati ya Mapinduzi ya Mkoa. Maamuzi au maelekezo ya Bodi yatatekelezwa na afisa leseni ingawa takuwa ya lazima kwa mahakama yoyote.

Sheria hii inatoa leseni za aina tatu za biashara kama zilivyoainishwa katika jadweli la kwanza la sheria. Leseni za mfanyabiashara za jumla, mfanyabiashara wa rejareja na leseni za benki ambazo kila moja imewekewa ada yake, malipo ya ada hizo yamewekewa muda maalum na pindi mfanyabiashara akichelewa kulipa atapambana na adhaabu ambayo imewekwa chini ya Sheria hii.

Utaratibu wa maombi ya leseni[71] utaanzia kwa maafisa wa leseni wa wilaya na miji baada ya kukamilika taratibu zilizowekwa na katika maombi hayo. Afisa leseni atawasilisha maombi na ada kama itakuwa imewekewa katika Kamati za Mapinduzi za Wilaya ambayo muombaji anaishi. Baada ya hapo maombi yaliyokubaliwa yatapelekwa kwa kamati za Mapinduzi za Mkoa kwa kuidhinishwa yote au kuidhinishwa baadhi na kufutwa baadhi yao.

---

[68] Kifungu cha 6 cha sheria Nam. 3 ya mwaka 1983
[69] kifungu cha 7
[70] kifungu cha 8
[71] Kifungu cha 10 cha sheria Nam. 3 ya mwaka 1983

Maombi yaliyopitishwa na kamati ya Mapinduzi ya Mkoa yatapelekwa kwa afisa leseni ambaye atamkabidhi muombaji huyo leseni yake ya biashara kama ilivyoelezwa katika sheria hii. Aidha utaratibu wa utoaji wa leseni za biashara kwa mujibu wa sheria hii ni kama ifuatavyo:

(a) maombi ya leseni yatapelekwa kwa Afisa leseni wa Mji au wilaya ambayo biashara inafanyika.

(b) Baada ya kupokea maombi ya leseni Afisa leseni wa Wilaya au Mji atapeleka maombi hayo kwa kamati ya mapinduzi ya Wilaya kwa mapitio.Ambapo baada ya mapito hayo kamati ya mapinduzi ya Wilaya itapeleka orodha ya waombaji wanaostahili kwa Kamati ya mapinduzi ya Mkoa kwa kuidhinishwa.

(c) Maombi yaliyoidhinishwa na Kamati ya Mapinduzi ya Mkoa yatapelekwa Bodi ya leseni kwa kuidhinishwa.

(d) Baada ya maombi kuidhinishwa na Bodi ya leseni ndio Afisa leseni atatoa leseni ya biashara kwa muombaji.

(e) sheria imeweka fomu maalum za maombi ya leseni za biashara pamoja leseni za biashara zenyewe.

Sheria hii pia imekataza kutolewa leseni kwa leseni mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18[72] na mtu ambaye imezuiwa leseni yake ya biashara na mahakama chini ya kifungu cha 20 cha sheria hii. Mmiliki wa leseni ya biashara anatakiwa kuiweka leseni yake katika eneo lake la biashara na itakapohitajika na afisa leseni au mtu mwengine yoyote kwa niaba ya afisa leseni kwa ajili ya uchunguzi

[72] kifungu cha 14

atalazimika kumuonesha.[73] Na ikitokea leseni ya biashara imepotea au kuharibika, afisa leseni atampatia mwenye leseni hiyo nakala ya leseni hiyo baada ya kukamilisha malipo.[74]

Kifungu cha 21 cha sheria kimetoa adhabu kwa makosa mbalimbali ikiwemo kufanya biashara bila ya kuwa na leseni inayofaa au vyenginevyo, ikiwa atavunja au atajaribu kuvunja masharti ya sheria hii, pamoja na adhabu ya kifungu cha 20 cha sheria hii kwa kosa la kwanza faini isiyozidi elfu moja na akishindwa kulipa atapelekwa chuo cha mafunzo kwa muda usiozidi mwaka mmoja. Kwa kosa la pili au zaidi adhabu isiyopungua elfu mbili na isiyozidi elfu tano akishindwa kulipa atatumikia chuo cha mafunzo kwa muda usiopungua mwaka mmoja na usiozidi miaka miwili.

Sheria pia katika kifungu cha 22 kimetoa uwezo kwa Waziri kubatilisha leseni yoyote ya biashara iliyotolewa kwa mtu au kumtoa mtu yeyote kufanya biashara au aina fulani ya biashara ambayo ataitaja katika amri yake hiyo, ikiwa ataona ni kwa maslahi mapana ya umma. Waziri atakapofanya hivyo atashauriana na Mwanasheria Mkuu na kwa kupata ridhaa ya Rais.

Hata hivyo mbali ya uwepo wa baadhi ya vifungu vya Sheria hii, sheria hiyo kwa sasa haitoshelezi mahitaji na imeshindwa kwenda sambamba na mabadiliko ya uchumi na biashara duniani. Kuna baadhi ya masharti yanapaswa kuzingatiwa pamoja na aina za biashara ambazo hazina udhibiti na usimamizi maalum.

[73] kifungu cha 18
[74] kifungu cha 19

Usimamizi na Mamlaka za leseni hazijaelezwa wazi na Kamati ya Mapinduzi iliyoanzishwa kisheria  kwa sasa haiwezi kufanyakazi  kutokana na kubadilika kwa Mfumo wa Serikali na usimamizi katika Serikali za Mitaa. Uundwaji wa chombo cha kuzisimamia Mamlaka za zinazotoa leseni unapaswa kutambuliwa na sheria hii ili malengo na majukumu ya taasisi hizo yasiingiliane katika usimamizi wa leseni Zanzibar.

Aidha sehemu ya adhabu imejumuisha maeneo machache hivyo kuna haja ya kuangaliwa tena sehemu hiyo, pamoja na kuweka utaratibu wa kumaliza makosa kwa makossa ya kawaida.

### 3.2.2 Sheria ya Biashara Nam. 14 ya mwaka 2013

Sheria ya Biashara Nam. 14 ya mwaka 2013 ina lengo la kuhuisha/kuboresha mfumo wa biashara Zanzibar. Sheria hii imetafsiri neno mamlaka ya leseni kuwa ni mamlaka zote zilizo pewa nguvu na sheria kutoa leseni hapa Zanzibar. Sheria hii inasimamia biashara na ufanyaji wa biashara ndani ya Zanzibar. Sheria hii ndio inayoweka sera na misingi ya usimamizi wa biashara na masharti kuhusiana uendeshaji wa biashara ndani ya Zanzibar.

Sheria katika kifungu cha 16 kimeeleza kwamba mtu yeyote atakayefanya biashara atawajibika kuwa na leseni ya biashara hiyo ambayo itatolewa na mamlaka inayosimamia biashara husika baada ya kutimiza masharti iliyowekewa. Sheria pia imewekea mamlaka za kutoa leseni majukumu mengine mbali na yale ambayo yamewekwa katika sheria maalum zinazowaongoza kwa zile mamlaka ambazo zinatoa leseni,

(a) kutoa leseni baada ya kuridhika kwamba masharti muhimu yametimizwa kwa mfanyabiashara kuwa na leseni inayomruhusu kufanya aina fulani ya biashara au biashara.

(b) Mamlaka baada ya kutoa leseni kuagiza masharti yoyote muhimu kwa mfanyabiashara kuyatimiza katika kufanya biashara yake.

(c) kadiri inavyowezekana, mamlaka ifanye ukaguzi mahali ambapo biashara itafanyika na ijiridhishe kuwa eneo la biashara linakidhi mahitaji yaliyoainishwa au ambayo ni muhimu kwa uendeshaji sahihi wa aina husika ya biashara.

Kifungu cha 6 kimeanzisha Kamati ya Ushauri wa masuala ya biashara iliyoanzishwa chini ya kifungu cha 6, na utaratibu na kazi za Kamati umetajwa katika kifungu cha 6 hadi cha 11. Kifungu cha 12(2) kimeainisha mamlaka ambazo kwa kushirikiana na Idara ya Biashara itateua maafisa wa kusimamia utekelezaji wa sheria hii. Majukumu ya wasimamizi watakaoteuliwa yameelezwa katika kifungu cha 13(1) na 14(1) ikiwemo kutoa amri ya kuzuia kufanywa biashara ikiwa mfanyabiashara hana nyaraka zinazohitajika, sehemu ya biashara haijafuata masharti yanayotakiwa, ikiwa mfanya biashara hana usajili n.k.

Kwa mujibu wa kifungu cha 16 cha Sheria hiyo mtu au wakala yeyote anayefanya biashara ni lazima awe na leseni ya biashara iliyotolewa na mamlaka ya leseni inayohusika baada ya kutimiza masharti kwa mujibu wa sheria husika. Kwa mujibu wa Sheria hiyo, anayehusika na kutoa leseni za biashara ni Mamlaka za leseni iliyopewa uwezo na Sheria kutoza leseni za biashara katika kifungu cha 17 na kifungu cha 18 kinaeleza kuwa maombi ya

usajili na leseni yawe katika fomu maalum na kifungu cha 18 kinaeleza kazi za mamlaka ya leseni ikiwa ni pamoja na kuainisha masharti yaliyoelezwa katika sheria kabla ya kutoa leseni (19(b)). Sehemu ya VII ya Sheria inaeleza kuwa Sheria hii ina mamlaka kwa bidhaa zinazoingizwa na kutolewa nje ya nchi. Aidha kifungu cha 30 kimeeleza biashara ambazo hazitatolewa leseni.

### 3.2.3Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya 2013

Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya mwaka 2013 ni miongoni mwa sheria muhimu sana katika kusimamia leseni za biashara Zanzibar. Pia imeanzishwa kwa lengo la kudhibiti mfumo wa leseni za biashara pamoja na mambo mengine yanayohusiana na hayo. Sheria hii ndiyo sheria inayosimamia mfumo mzima wa utoaji wa leseni za biashara. Mamlaka zote za leseni za biashara zinasimamiwa na sheria hii katika utoaji wa leseni. Aidha mamlaka yoyote ya leseni za biashara inawajibika kufuata na kuzingatia masharti yaliyomo katika sheria hii katika utozaji wa leseni za biashara.

Sheria hii pia imeainisha misingi ambayo inapaswa kuzingatiwa na mamlaka za leseni katika utozaji wa leseni, vibali au ruhusa za biashara. Miongoni mwa misingi hiyo ni kama ulioainishwa katika kifungu cha 20(1) (h) (i) kwamba mahitaji ya mtu kuwa na leseni ya biashara, kibali au ruhusa yatakua ni kwa ajili ya kudhibiti biashara tu.

Mantiki iliyopo katika Sheria hiyo kwamba mamlaka ya leseni itatoza leseni ya biashara kwa lengo la kusimamia na kudhibiti biashara pekee. Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya 2013 chini ya kifungu cha 4 kimeanzisha chombo maalum cha kusimamia mfumo wa leseni za biashara

ambalo ni Baraza la usimamizi wa leseni za biashara. Baraza hilo limepewa kazi muhimu katika leseni za biashara zikiwemo:

(a) kutekeleza kwa ufanisi mfumo wa kitaifa wa utoaji leseni

(b) kuendeleza sera kuhusu leseni na kusimamia mfumo wa leseni, vibali na ruhusa

(c) kupitia mahitaji yote ya kushikilia leseni, vibali au ruhusa ya kuanzisha au kuendelea katika biashara au kufanya shughuli zozote za kibiashara na kutoa maagizo kwa mamlaka husika kwa kuondolewa kwa mahitaji yoyote ambayo hayafikii kiini chini ya kifungu 20(1) na (2) cha sheria hii.[75]

(d) kushirikiana na chombo chochote kinachopitia mfumo wa leseni ya kitaifa au mfumo wa udhibiti wa biashara au nyanja yoyote.

(e) kukagua na kurekebisha ada inayolipwa kwa leseni, vibali au ruhusa zilizoidhinishwa chini ya sheria hii.

Aidha Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya 2013 imeweka wazi kuwa Baraza ndio litakalotoa orodha ya mamlaka zilizoruhusiwa kutoa leseni au vibali kupitia kwenye Gazeti rasmi la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. Mamlaka isiyoorodheshwa haitaruhusiwa kutoa leseni, vibali au ruhusa ya biashara.[76] Baraza pia ndio lililopewa mamlaka ya kuweka kumbukumbu za kitaifa za mahitaji muhimu ya mtu kuweza kupata leseni, kibali au ruhusa ili kuweza kufanya biashara.

[75] ibid

[76] ibid

### 3.2.4 Sheria ya Utalii Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2009[77]

Sheria ya Utalii Zanzibar imetafsiri neno leseni kama ni leseni zinazotolewa chini ya sheria hii kwa lengo la kufanya biashara ya utalii. Kifungu cha 3 cha sheria kimeanzisha kamisheni ya utalii Zanzibar ambayo miongoni mwa kazi zake ni kama zifuatazo:

(a) kusajili, kutoa leseni na kusimamia biashara za utalii;
(b) kubadili, kusitisha matumizi, kufanya marekebisho ya leseni zilizotolewa chini ya sheria hii;
(c) kusikiliza na kufanya uchunguzi juu ya malalamiko yanayohusu biashara ya utalii.

Sheria ya Utalii katika sehemu ya Nne imeelezea kuhusu leseni za biashara ya utalii na kifungu cha 15 kimeweka wazi kuwa hakuna mtu atakayeruhusiwa kuendesha biashara ya utalii bila ya kuwa na leseni iliyotolewa na Kamisheni ya Utalii.

Mkurugenzi Mkuu atatoa leseni kwa mtu anayefanya biashara baada ya kukamilisha matakwa ya kisheria yaliyowekwa chini ya sheria hii, leseni hiyo itakuwa katika fomu maalum, leseni hiyo uhalali wake utakuwa ni wa muda wa mwaka mmoja na itatolewa baada ya kukamilisha malipo yaliyowekwa.

Sheria ya Utalii imeweka kifungu 28 cha makosa na adhabu. Katika kifungu hicho kimeeleza mtu ambaye anafanya biashara ya utalii bila ya leseni halali atakuwa ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyozidi dola elfu kumi za kimarekani au kifungo kisichopungua miezi mitatu na

[77] Sheria Nam. 6 ya mwaka 2009

kichozidi miezi mitano au adhabu zote mbili kwa pamoja, akiendelea kufanya kosa hilo kwa mara nyengine atawajibika kulipa faini ya dola hamsini kwa kila siku moja ya kutenda kosa hilo au kifungo cha mwezi kwa kila siku moja ya kutenda kosa hilo.

### 3.2.5 Sheria ya Misitu na Mali zisizohamishika Nam. 10 ya 1996.

Sheria ya Misitu na Mali zisizohamishika Nam. 10 ya 1996 ina lengo la kulinda, kuhifadhi na kuendeleza rasilimali za misitu kwa faida ya kijamii, kiuchumi na kimazingira kwa vizazi vya sasa na vijavyo vya wazanzibari.

Sheria inahusika na usimamizi wa misitu, Mipango ya Kitaifa ya Rasilimali za Misitu, misitu ya Akiba na Hifadhi za Misitu ya Asili. Sehemu ya VI ya sheria inazungumzia leseni ambayo inaweza kutolewa ikimruhusu mmiliki kufanya moja au zaidi ya yafuatayo katika hifadhi ya msitu:

(a) Kukata miti kwa matumizi ya mbao,
(b) kuchukua mazao mengine ya misitu,
(c) Kujenga majengo au maboma ya mifugo,
(d) kupanda mazao au miti,
(e) Kujenga barabara, njia au njia za maji,
(f) Kuwinda au kufuga samaki maeneo ya misitu;
(g) Shughuli nyengine.

Leseni inaweza kutolewa ikimruhusu mmiliki kufanya moja au zaidi ya yafuatayo kwa namna fulani ikiwemo kuchambua miti iliyokufa, kuvuna mazao ya misitu yasiyo ya mbao na shughuli nyengine. Leseni inaweza kutolewa

kumruhusu mmiliki kuangusha au kung'oa miti au shughuli nyengine. Hata hivyo, afisa wa leseni anaweza kutoa leseni kuruhusu shughuli hizo.

Hakuna leseni inayoweza kutolewa isipokuwa shughuli inayohusika inaambatana na Mpango wa usimamizi wa eneo la misitu, Mpango wa usimamizi wa mazingira, Mpango wa matumizi ya ardhi. Hakuna leseni inayohitajika kwa shughuli ambazo zimeruhusiwa wazi na mpango wa usimamizi wa eneo la msitu.

Sheria ya Misitu na Mali zisizohamishika katika kifungu cha 7 kinampa Mamlaka ya Usimamizi wa misitu anateuliwa na Rais kwa kushauriana na Waziri. Msimamizi wa misitu anaweza kumchagua Afisa yeyote kuwa ni Afisa wa leseni ambaye atakua na uwezo wa kutoa aina yoyote ya leseni zilizoainishwa chini ya sehemu ya saba ya sheria hii.

Sehemu ya Saba ya Sheria ya Misitu na Mali zimetaja aina mbalimbali za leseni ambazo Afisa leseni atazitoa zikiwemo kukata mbao katika hifadhi ya msitu, kuchukua mazao mengine ya misitu, kuruhusu kuingiza wanyama, kuwinda au kuvua samaki, kupanda miti au mazao, kujenga njia za kupitia watu au njia za maji. Vilevile leseni za kuruhusu uchukuaji wa miti iliyokufa, kuchukua miti isiyokua ya mbao.

Waziri anaweza kutangaza katika Gazeti rasmi la Serikali aina ya miti ambayo itaingia katika miti inayotunzwa na baada ya kutangazwa miti hiyo hakuna mti utakaokatwa au kufanya kitu chengine chochote bila ya kuomba leseni. Sheria imeweka adhabu kwa mtu yeyote ambaye hana mamlaka chini ya sheria hii akafanya bila leseni, shughuli yoyote ambayo inahitaji leseni, atakua ametenda kosa na atakapotiwa hatiani atatumikia kifungo kisichopungua miezi sita au atalipa faini iliyowekwa katika Jadweli la pili.[78]

Sheria hii imetoa mamlaka makubwa ya kukasimu kwa maafisa na wananchi mbalimbali, kusimamia utoaji wa leseni, ruhusa na vibali bila kuweka miongozo maalum.

### 3.2.6 Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar Nam. 7 ya 2014

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar Nam. 7 ya mwaka 2014, Kifungu cha 21 kinatoa kazi za Baraza la Manispaa ambapo miongoni mwa kazi zake ni kutoa, kusimamia na kudhibiti leseni za biashara katika eneo lake.

Vile vile Sheria katika kifungu cha 23, imeweka kazi za Baraza la Mji ambapo pia miongoni mwa kazi zake ni kutoa, kusimamia na kudhibiti leseni za biashara katika eneo lake. Aidha Sheria katika kifungu 82(1)(d) cha makosa na adhabu kimeweka wazi kwamba, mtu yeyote atakayefanya biashara wakati leseni yake, usajili au ruhusa yake vimefutwa chini ya sheria hii atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa kulipa faini isiyopungua laki moja, au kifungo kisichopungua miezi miwili au adhabu zote mbili kwa pamoja.

[78] ibid

### 3.2.7 Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya mwaka 2010

Sheria ya Uvuvi imeanzisha kitengo maalum cha uvuvi kitakachokuwa na kazi maalum zikiwemo kujenga uwezo katika kusimamia masuala ya uvuvi na mambo mengine yanayohusiana nayo. Kifungu 14 cha Sheria kimeweka wazi matakwa ya sheria hii kwamba vyombo vyote vitakavyofanya kazi ya uvuvi katika maeneo ya bahari "territorial", "internal water" au maeneo maalum ya kiuchumi ya Zanzibar ni lazima awe na leseni.[79]

Leseni hizo zinaweza kuwekwa na Waziri kwenye viwango tofauti vya malipo kutegemea na aina ya samaki unaovua, ukubwa na nguvu ya chombo na mambo mengine na leseni chini ya sheria hii zitakua katika fomu maalum. Sheria katika Sehemu ya II inaanzisha Idara ya Uvuvi, Kifungu cha 9 kinaweka masharti ya leseni, na Mkurugenzi wa Idara anaweza kuweka masharti ya leseni kwa kuzingatia maeneo yaliyopigwa marufuku kwa uvuvi, kizuizi cha mbinu na zana za uvuvi, kuzuia kuvua aina za samaki, kuzuia uchafuzi wa maji ya ndani au ya eneo.

Kila meli ya uvuvi inayofanya kazi katika maji ya ndani, maji ya eneo au Ukanda wa Kipekee wa Kiuchumi Zanzibar (EEZ) inahitaji leseni. Waziri anaweza kuanzisha aina za leseni na ada zinazolipwa. Kuna fomu iliyowekwa kwa ajili ya maombi na ada na leseni ni halali kwa mwaka 1. Kifungu cha 15 kina masharti ya jumla ya leseni ikiwemo fomu zilizowekwa na Kanuni, mamlaka ya Waziri kuweka sheria na masharti katika Kanuni, wajibu wa kumpa Mkurugenzi takwimu na taarifa inapohitajika. Leseni inaweza kusimamishwa

[79] ibid

au kufutwa kwa ukiukaji wa masharti, inagwa muhusika anaweza kukata rufaa dhidi ya uamuzi wa Mkurugenzi lakini uamuzi wa Waziri ni wa mwisho.

Sheria imempa mamlaka Mkurugenzi kutunza Daftari la Leseni, na Waziri anaweza, kwa pendekezo la Mkurugenzi, kuanzisha leseni nyengine za kuvua kwa zana bila kutumia chombo, kusindika samaki au viumbe vyengine vya baharini.

Ukiukaji wa masharti ya leseni na vibali adhabu yake ni faini isiyopungua TZS 100,000 na si zaidi ya TZS 5,000,000 na au isiyopungua kifungo cha miezi 3 na kifungo kisichozidi miaka 2. Sheria katika kifungu 28 cha makosa na adhabu imeeleza mtu yeyote atayekwenda kinyume na vifungu vinavyoeleza kuhusu leseni atakua ametenda kosa na akitiwa hatiani atawajibika kulipa faini isiyopungua laki moja na isiyozidi milioni tano au kifungo kisichopungua miezi mitatu na kisichozidi miaka miwili au adhabu zote kwa pamoja.

### 3.2.8 Sheria ya Mamlaka ya Bahari Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2009.

Sheria ya Mamlaka ya Bahari imeeleza kazi za mamlaka ya vyombo vya usafiri kimeweka wazi kuwa miongoni mwa kazi zake ni kama zifuatazo:

(a) kusajili na kutoa leseni za meli za biashara kwa madhumuni ya kufikia matakwa ya kitaifa na kimataifa, kutoa utaifa, kuthibitisha umiliki na hatimiliki, kusajili rehani na kuanzisha utambulisho wa chombo.

(b) kutoa leseni na kudhibiti meli ndogo, meli, boti ndogondogo na kuhakikisha usalama wa vyombo vya uvuvi.

Makosa na adhabu yameelezwa katika sehemu sita ya sheria hii, ambapo kifungu cha 28 kinatoa adhabu kwa mtu yeyote ataanzisha, kuweka au kuendesha huduma za baharini bila ya kuwa na idhini au leseni iliyotolewa na Mamlaka atakuwa amefanya kosa.[80]

### 3.2.9 Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar Nam. 7 ya 2013.

Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar namba 7 ya 2013, imeanzisha mamlaka ya usimamizi wa huduma wa Maji na Nishati ambayo inaongozwa na Mkurugenzi Mkuu katika kusimamia shuhuli zake za kila siku. Sheria ya Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar namba 7 ya 2013, Kifungu cha 12 kinaonesha kwamba Mamlaka itatoa leseni kwa huduma za umma zinazodhibitiwa kama ifuatavyo:

(a) umeme – uzalishaji, usambazaji, usafirishaji na uuzaji.[81]
(b) Maji – usambazaji na kuendeleza vyanzo vya maji.[82]
(c) Petroli–usambazaji, uingizaji, uuzaji wa jumla na rejareja na mengineyo.[83]

Mamlaka katika sheria hii imepewa uwezo wa kupokea, kutoa, kurekebisha na kuibatilisha leseni yoyote na vilevile kuweka vigezo na masharti ya kutoa leseni chini ya sheria hii.

[80] ibid
[81] Kifungu cha 10
[82] Kifungu cha 9
[83] Kifungu cha 8

### 3.2.10 Sheria ya Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020

Sheria ya Vileo inasimamia leseni na kudhibiti vileo kwa kuzingatia uagizaji, uhifadhi, uuzaji, usambazaji na utumiaji wa vileo. Vilevile sheria hii imeweka marufuku kwa kuuza au kuweka kwenye ghala vileo vya aina yoyote bila leseni.[84]

Serikali katika sheria hii imeanzisha Bodi ya ushauri ya vileo kwa lengo la kudhibiti vileo Zanzibar ambayo miongoni mwa kazi zake zikiwemo:[85]

(a) Kuweka masharti ya utunzaji wa majengo yaliyopewa leseni ya vileo na kudhibiti utunzaji na usambazaji kutoka katika maeneo hayo;
(b) Kusimamia maombi, utoaji, ulipaji upya wa leseni na vibali na kumalizika kwa leseni na vibali.

Kifungu cha 25 cha sheria hii kimetaja leseni na vibali vyote ambavyo vinatolewa chini ya sheria hii ikiwemo leseni ya hoteli; leseni ya baa; leseni ya duka la vileo; leseni ya ghala; kibali cha kuagiza vileo; kibali cha usambazaji vileo; na kibali cha hafla maalum.

Sheria katika kifungu cha 45, sehemu ya sita ya makosa na adhabu, imeelezea kuhusiana na makosa ya tofauti ya leseni likiwemo kuuza au kuweka kwenye ghala vileo vinavyo lewesha bila kuwa na leseni na kufanya hivyo kumewekewa adhabu ya faini isiyopungua TZS 1, 000,000 na kifungo kisichopungua miezi sita.

[84] ibid
[85] ibid

Ukaguzi utakapofanyika mkaguzi au afisa yeyote aliyeidhinishwa na bodi atakua na uwezo wa kumuagiza mwenye leseni wa eneo hilo kutoa taarifa, kumbukumbu au kitu chochote ambacho mwenye leseni anapaswa kuweka chini ya sheria hii.

Sheria imeweka katazo juu ya maafisa kutumia vibaya mamlaka yao. Sheria katika kifungu chake cha 38. Afisa yeyote akila njama za kuzuia au kusambaza vifaa au akikubali, kula rushwa au akikubali hidaya au malipo ya fadhila na kupanga au kula njama na mtu yeyote kufanya jambo ambalo ni kinyume na sheria hii atakua ametenda kosa.

### 3.2.11 Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya mwaka 2006

Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi imeainisha kazi za Bodi ya chakula, madawa na vipodozi ambayo imeanzishwa chini ya kifungu cha 3 cha sheria hii, zimeelezwa katika kifungu cha 4.

(a) kudhibiti masuala yote yanayohusiana na ubora, usalama wa chakula, dawa, dawa za mitishamba, vifaa vya matibabu, sumu na vipodozi;

(b) kwa mujibu wa Sheria hii, uagizaji, kutengeneza, kuweka lebo, kuweka alama au kitambulisho, kuhifadhi, kukuza, kuuza na usambazaji wa chakula, madawa ya kulevya, vipodozi, dawa za mitishamba na vifaa tiba au nyenzo yoyote au vitu vinavyotumika katika utengenezaji wa bidhaa zilizodhibitiwa chini ya Sheria hii;

(c) kuchunguza, kutoa, kusimamisha kwa muda, kufuta na kubatilisha vyeti na leseni au vibali vilivyotolewa chini ya Sheria hii.

### 3.2.12 Sheria Ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997

Sheria ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997 katika kifungu cha 5 imeanzisha Kamisheni ya Utangazaji Zanzibar ambapo miongoni mwa kazi zake za msingi ni:

(a) Kutoa leseni za utangazaji;

(b) Kusimamia shughuli za utangazaji ikiwa ni pamoja na lakini sio tu urushaji wa matangazo ya redio, televisheni na video kutoka nje ya Zanzibar kwa nia ya kuwa matangazo hayo yatapatikana mara kwa mara Zanzibar;

(c) Kutunza kumbukumbu ya watu wote waliopewa leseni ya kuwa watangazaji, wauzaji katika vituo vya utangazaji.

(d) Udhibiti wa shughuli za watangazaji na wafanyabiashara.

(e) Ukaguzi wa taasisi za utangazaji.

Mtu hawezi kuwa na leseni ya utangazaji ya redio na TV kwa wakati mmoja. Kamisheni itafanya kuchapisha orodha ya maombi ili kuwapa watu nafasi ya kupinga utoaji wa leseni. Leseni hutolewa kwa kujaza fomu na kwa malipo ya ada yaliyowekwa.

### 3.2.12 Kanuni ya Usafiri wa Baharini (Usajili na Leseni za Vyombo) ya mwaka 2007

Kanuni za 67 -76 zinasimamia utoaji wa leseni kwa meli ambazo hazijasajiliwa na hizi zinahusika na maombi ya leseni, maelezo ya kusajiliwa, kuweka alama, muda wa leseni, taarifa ya mabadiliko ya mmiliki na kusitishwa kwa leseni.

Kanuni ya 84 inatoa masharti ya meli ndogo na kuwa wamiliki wa meli ndogo wameorodheshwa, na Kanuni ya 85 imeweka sifa za kupata leseni ikiwemo kuwa Mtanzania, wananchi wa EAC, watu binafsi au mashirika ya kigeni katika uhusiano wa biashara ya ubia wa ubia wa meli na raia wa Tanzania.[86]

Sheria zinazosimamia meli katika Kanuni za 96-108 na hizi zinahusika na Mahitaji ya kusajiliwa au kupewa leseni, usajili wa meli za asili zaidi ya 50 GT, kutoa leseni kwa vyombo vingine vya asili, mahitaji ya uchunguzi. mahitaji ya kupewa leseni meli ndogo zimo katika Kanuni za 109-120 na mikataba.

### 3.2.13 Zanzibar Industrial Property Act, Nam. 4 ya mwaka 2008

Sheria hii inahusiana na umiliki wa alama na hati miliki za biashara katika neno lolote, jina, ishara, au kifaa, au mchanganyiko wowote, kutumika au inayokusudiwa kutumika, katika biashara kutambua na kutofautisha bidhaa za mtengenezaji mmoja au muuzaji kutoka kwa bidhaa zinazotengenezwa au kuuzwa na wengine, na kuonesha chanzo cha bidhaa.

Kifungu cha 14 kinampa Waziri mamlaka, katika hali ya kipekee kutoa leseni kwa matumizi ya hati miliki. Mazingira yanayozingatiwa ni pamoja na usalama wa Taifa, dharura ya kitaifa, masuala ya lishe, masuala ya afya, maendeleo ya sekta nyengine muhimu za uchumi yanahitaji hivyo.[87] Leseni inaweza kubadilishwa kwa ombi la mmiliki, na inaweza tu kutolewa kwa misingi isiyo ya kipekee.[88]

---

[86] kanuni ya 99(3).

[87] Kifungu cha 14(1)(a)

[88] Kifungu cha 14

### 3.2.14 Sheria ya Usajili wa Makandarasi Nam. 6 ya mwaka 2008

Sheria hii inatoa leseni kwa wakandarasi wanaofanya kazi Zanzibar. Sheria imeeleza aina tofauti za wakandarasi wanaoweza kupewa leseni[89] kama wakandarasi wa kazi za ujenzi, wakandarasi wa umeme, wakandarasi wa mitambo, kazi za maji na wakandarasi wa maji taka na wakandarasi wataalam.

Daftari la Usajili (register) la wakandarasi limenazishwa na linatunzwa na Msajili. Sheria inaruhusu kuweka Daftari na orodha ya wakandarasi na uchapishaji wa jina katika orodha ni ushahidi wa kusajiliwa kisheria.

Kifungu cha 20 kinaweka sifa za kusajiliwa mkandarasi ikiwemo maombi lazima yawe kwenye fomu inayotakiwa na kuambatanishwa na malipo yaliyowekwa, mwombaji lazima awe na kiwango cha chini zaidi cha sifa za kiufundi na utaalam uliowekwa na Bodi ya aina na daraja la mkandarasi ambaye usajili unaoombwa; na leseni zinatolewa kila mwaka na Bodi inaweza kufuta, au kusimamisha usajili.

## 3.3 Sheria za Muungano zinazotoa Leseni Zanzibar

### 3.3.1 Sheria ya Benki ya Tanzania (BOT) Nam. 4 ya mwaka 2006

Sheria ya Benki ya Tanzania (BOT) ya mwaka 2006 katika kifungu cha 5 (1) imetaja majukumu makuu Benki Kuu ambayo ni kutekeleza kazi za benki kuu na, bila kuathiri ujumla wailiyotangulia, kutunga, kutekeleza na kuwajibika kwa sera ya fedha, ikiwa ni pamoja na sera ya viwango vya ubadilishaji fedha, kutoa sarafu, kudhibiti na kusimamia benki na taasisi za fedha ikiwa ni pamoja na

[89] Kifungu cha 23

ufadhili wa mikopo ya nyumba, ufadhili wa rehani, ufadhili wa kukodisha, leseni na ubatilishaji wa leseni na kushughulikia, kumiliki na kusimamia akiba ya dhahabu na fedha za kigeni za Tanzania.

### 3.3.2 Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi nyengine za Kifedha Nam. 5 ya mwaka 2006

Sheria ya mambo ya Kibenki na Taasisi nyengine za Kifedha ni Sheria ya Muungano na katika kifungu cha 4 kimeipa mamlaka Benki Kuu kutoa leseni, kudhibiti na kusimamia benki zote na Taasisi za fedha zilizomo ndani ya Jamhuri ya Muungano na ambazo zinasimamiwa na Sheria hii.

Vile vile Benki, mbali ya kazi ya kutoa leseni hii ina uwezo wa kufanya ukaguzi wa uendeshaji wa benki zote au taasisi za fedha kwa mujibu wa sheria hili, kuhitaji benki yoyote au taasisi ya fedha kutoa taarifa yoyote au kuzingatia amri, maagizo au uamuzi uliotolewa au kufanywa na Benki kwa mujibu wa mamlaka iliyopewa benki chini ya sheria hii.

Sheria inaendelea kutoa mkazo katika kuonesha umuhimu wa leseni katika biashara za kibenki kwa kutoa katazo chini ya kifungu cha 6 kwamba mtu hawezi kufanya biashara ya benki au kukubali kuweka fedha za watu amana isipokuwa mtu huyo ana leseni iliyotolewa na Benki kwa mujibu wa masharti ya Sehemu ya tatu ya sheria hii.

Maombi ya leseni yanatakiwa yawe katika maandishi na maombi hayo yatazingatia uwepo wa “Memorandum na Articles of Association,” taarifa za anuani ya eneo la biashara, taarifa za anuani za kila mteja, mbia, bodi

wakurugenzi, Afisa Mtendaji Mkuu na afisa yeyote ambaye moja kwa moja anawajibika Afisa Mtendaji Mkuu, taarifa ambazo zinaweza kuagizwa na Benki kwa madhumuni ya kutathmini uwezo na uaminifu wa kila mbia na taarifa za fedha, mipango ya biashara na nyaraka nyinginezo ambazo Benki inaweza kuhitaji ili kuendesha uchunguzi wakati wa kukagua maombi.

Kutolewa au kukataliwa kwa leseni ndani ya sheria hii kunafanyika ndani ya siku tisini baada ya kupokelewa kwa maombi au, pale ambapo taarifa zaidi zimehitajika, baada ya kuzipokea taarifa hizo. Benki itatoa leseni pale tu itakaporidhika kwamba mwombaji amekidhi vigezo vya leseni chini ya Sheria hii na sheria nyengine yoyote iliyoainishwa na Benki.

### 3.3.3 Sheria ya Kusimamia Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari kuu Nam. 5 ya mwaka 2020

Sheria ya Kusimamia Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari kuu namba 5 ya mwaka 2020 inafanya kazi katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar). Kifungu cha 6 cha sheria kimetaja kazi za Mamlaka zikiwemo:

(a) kuunda, kutekeleza na kufuatilia utekelezaji wa sera na mikakati ya taifa kuhusu uhifadhi, usimamizi, maendeleo na matumizi endelevu ya rasilimali za uvuvi katika Ukanda Maalum wa Kiuchumi;

(b) kuendeleza, kusimamia na kudhibiti shughuli zote zinazohusiana na uvuvi, ikiwa ni pamoja na uvuvi na shughuli zinazohusiana, katika Ukanda Maalum wa Kiuchumi na mengine yote, watu na shughuli zinazosimamiwa na Sheria hii, ikijumuisha kudhibiti na kusimamia utoaji wa leseni, ruhusa na vibali vyengine vinavyohitajika kwa shughuli zilizo chini ya Sheria hii;

(c) kuamua ada, malipo, vyanzo vya kodi au mrabaha;

Kifungu cha 16 cha sheria hii kimeweka kazi na uwezo wa Mkurugenzi Mkuu wa mamlaka, ikiwemo utoaji, kukataa, kusimamishwa na kufutwa kwa leseni, idhini na aina nyengine za ruhusa zinazotolewa chini ya Sheria hii.

Kifungu cha 35 cha sheria kimeweka wazi kwamba mtu hataweza kuendesha chombo cha uvuvi, au kushiriki katika shughuli zozote za uvuvi isipokuwa awe anayo leseni, ruhusa au idhini iliyotolewa kwa mujibu wa Sheria hii.

Mwenye leseni, idhini au ruhusa nyengine iliyotolewa chini ya Sheria hii atafuata masharti na vigezo vya leseni, idhini au ruhusa nyengine; kutii Sheria hii, na sheria nyengine yoyote iliyoandikwa na hatua zozote zinazotumika za uhifadhi na usimamizi wa kimataifa; na kuzingatia masharti yote muhimu ya sheria za Jamhuri ya Muungano zinazohusiana na viwango vya urambazaji, usalama wa baharini na usalama wa meli baharini.

### 3.3.4 Sheria ya Bima Nam. 10 ya mwaka 2009

Sheria ya Bima inatumika kwa biashara zote za bima katika Jamhuri ya Muungano ya Tanzania (Tanzania Bara na Tanzania Zanzibar), chini ya kifungu cha 5 cha sheria ya Bima kumeanzishwa Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania. Mamlaka hii ilipewa jukumu la kuweka kanuni za maadili kwa wanachama wa sekta ya bima, usimamizi na ufuatiliaji wa Bima, madalali na mawakala, kuandaa viwango vya uendeshaji wa biashara ya bima ambavyo vitazingatiwa na wenye bima, madalali na mawakala. kuhakikisha uzingatiaji ipasavyo wa kanuni za maadili na utendaji kazi na bima, madalali na mawakala;

kulinda maslahi ya mwenye sera, kubainisha sifa zinazohitajika kwa wanachama wa sekta ya bima na kuweka tozo za malipo na kamisheni.

Kwa mujibu wa sheria hii kifungu cha 21 hakuna mtu anayeishi Tanzania atafanya biashara ya bima, isipokuwa awe amesajiliwa kama bima. Maombi yote ya bima yataombwa kwa Kamishna katika fomu maalum iliyowekwa.
Sheria inaeleza kwamba ndani ya miezi mitatu baada ya kupokea ombi au kama alihitaji taarifa zaidi, mara baada ya kupokea taarifa hizo, Kamishna anaweza kutoa usajili kwa mwombaji na ikiwa maombi yamekataliwa, atampa mwombaji sababu ambayo ni ya msingi ya kukataliwa ombi lake hilo.

### 3.3.5 Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Nam. 12 ya mwaka 2003 "TCRA"

Sheria ya mamlaka ya mawasiliano Tanzania "TCRA" ni sheria inayosimamia masuala ya Mawasiliano. Katika kifungu cha 4(1) imeanzisha Mamlaka ya Udhibiti wa Mawasiliano Tanzania pia inajulikana kwa kifupi chake "TCRA".
Kifungu cha 6. (1) kimeeleza kazi za Mamlaka ikiwemo kutekeleza majukumu iliyopewa Mamlaka na sekta sheria; kutoa, kuhuisha na kufuta leseni; kuanzisha viwango vya bidhaa na huduma zinazodhibitiwa; na kuanzisha viwango vya vigezo na masharti ya usambazaji wa bidhaa na huduma zinazodhibitiwa.

## SURA YA NNE

## 4.0 MAONI YA WADAU

### 4.1 Utangulizi

Tume ya Kurekebisha Sheria katika kukamilisha utafiti huu ilikutana na makundi ya wadau waliojumuisha Taasisi za Muungano zinazosimamia leseni, taasisi zinazotoa leseni Zanzibar, Mamlaka za Leseni ikiwemo Baraza la Leseni Zanzibar, Wizara ya Biashara, Viwanda na Masoko, wafanyabiashara wa sekta mbalimbali, wadau wengine pamoja na Asasi za kiraia. Lengo la vikao hivyo ni kupata maoni na mapendekezo ya wadau wa sekta ya leseni za biashara. Tume imeyagawa maoni katika maeneo ya Kisheria na Kiutendaji.

### 4.2 Maoni ya Kisheria

#### (a) Muundo wa taasisi/mamlaka

Wadau wameeleza kwamba Sheria ya Leseni za Biashara ya mwaka 1983 ina haja ya kuwekewa muundo maalum na mifumo ya usimamizi ili kuweza kuratibu shughuli za utoaji wa leseni. Aidha imependekezwa Sheria iangalie chombo maalum cha kusimamia masuala ya leseni pamoja na kuweka wazi mamlaka ya vyombo vya usimamizi akiwemo Waziri husika, Mamlaka za leseni, Maafisa leseni n.k.

#### (b) Utoaji wa leseni

Wadau wamependekeza kwamba mamlaka kuu ya utoaji wa leseni za biashara zilizoanzishwa kisheria zibakie na Mamlaka zilizopewa na wapewe miongozo ya jumla ya utoaji wa leseni; na kwa biashara ambazo hazina msimamizi maalum ziwekewe utaratibu na mamlaka ya usimamizi ya utoaji leseni.

### (c) Utaratibu wa kumaliza makosa

Wadau wamependekeza kuwekwa utaratibu wa kumaliza makosa au adhabu za papo kwa papo kwa makosa ya kawaida ambayo hayahitaji uchunguzi wa kina au kuhusisha udanganyifu. Makosa kama kutobandika leseni, kupitiliza muda wa leseni na mengine yanahitaji kumalizwa kwa muda mfupi ili wafanyabiashara wapate muda wa kusimamia na kuendesha biashara zao.

Wadau wametoa maoni juu ya suala la kufungiwa biashara pale watakaposhindwa kutimiza masharti, ni vyema utaratibu wa kumaliza makosa ukatumika ili aweza kufanya biashara yake na kuiwezesha Serikali kukusanya mapato.

### (d) Biashara ambazo hazina msimamizi maalum

Wadau walitoa maoni yao katika biashara ambazo ni mpya zinazoanzishwa au kuibuka kutokana na mazingira na utandawazi kwa sasa, biashara hizi zitambuliwe na kuwekewa utaratibu wa kuzisimamia.

Biashara zinazoibuka zinawapa fursa wafanyabiashara hao kutokufuata taratibu na kupata kipato zaidi kuliko wale walio sehemu za biashara, kutokana na asili ya biashara hizo kuwa katika mkificho au kujulikana na watu wa kundi maalum. Kuna biashara za “mobile business” na “wamachinga” ambazo zinawashawishiwa baadhi yao na wenye maduka makubwa kwa lengo la kukwepa kodi au kuficha uhalisia wa biashara zao zinapaswa kusimamiwa kikamilifu. Hivyo wadau wameshauri katika marekebisho ya sheria iliyopo yafanywe kwa kujumuisha makundi yote ya biashara.

### (e) Adhabu kwa makosa ya leseni

Wadau wameeleza kwamba kuna haja ya kuangaliwa adhabu zilizotajwa katika sheria kwakuwa nyingi ni za muda mtefu, na hazilingani na wakati wa sasa, kwa sasa kutokana na utandawazi biashara zimekuwa na makosa mengi na mbinu ambazo zinawadanya kukiuka utaratibu wa leseni.

### (f) Uwezo wa Waziri na mamlaka nyengine

Wadau wameonesha wasiwasi juu ya baadhi ya Mamlaka kuchukua maamuzi bila ya kusikiliza wafanyabishara wanaolalamikiwa, ni vyema kuweka wazi utaratibu wa kutumika katika kupokea malalamiko na kuchukua hatua ikiwemo kuwapa fursa za kujieleza kabla ya kuchukua hatua au kutoa maamuzi.

## 4.3 Maoni ya Kiutendaji

### (a) Kuwepo taasisi nyingi za kutoa leseni

Wadau wameeleza uwepo wa changamoto ya uanzishwaji wa mamlaka nyingi za kutoa leseni bila kutambua mipaka na mamlaka ya kila taasisi. Hali hii inafanya biashara mpoja kudhibitiwa na kusimamiwa na taasisi nyingi, na kila moja kuwa na mamlaka tafauti na hivyo kupoteza au kuathiri lengo la kuanzishwa biashara husika. Aidha uwepo wa taasisi nyingi kunaongeza gharama za uendeshaji kwa wafanyabiashara kutokana na kuwepo kwa ada nyingi, vibali, ruhusa, na urasimu katika kukamilisha hatua za upatikanaji wa leseni.

Wadau wameeleza kwamba hali hii inawasababishia usumbufu mkubwa, ambapo mfanyabiashara inabidi azifate leseni hizo katika taasisi hizo kwa

wakati tofauti na kupelekea kupoteza muda na rasilimali katika utafutaji wa leseni.

### (b) Leseni kama chanzo cha mapato

Wadau wameitaka Serikali kuhakikisha kwamba leseni za biashara zinatolewa kwa lengo la kuzitambua biashara na kuzisimamia. Kwa sasa imebainika kwamba taasisi nyingi zimefanya leseni kama chanzo cha mapato na hivyo kutokuzingatia viwango vya leseni, kutokusimamia uendeshaji na malengo ya biashara, kutokutathmini mwenedno wa biashara kisekta na kupandisha ada kiholela. Hali hii inaondoa msingi wa kutolewa leseni na kukosekana udhibiti na mashartyi yaliyowekwa katika leseni kwa kila biashara.

### (c) Leseni nyingi biashara moja

Imeelezwa kwamba kuna haja ya kuweka utaratibu maalum kwa leseni za wawekezaji na wafanyabiashara wenye biashara zaidi ya moja. Imependekezwa utaratibu ujumuishe eneo moja (one stop centre) la kusimamia na kutoa leseni, kuunganisha taarifa za biashara, na kuhakikisha utoaji wa leseni unachukua miuda mfupi baada ya kukidhi viwango na masharti yaliyowekwa kisheria.

### (d) Elimu kwa wafanyabiashara

Wadau wamesisitiza kutolewe elimu ya kutosha juu ya masuala ya leseni ili kuwaaaidia wafanyabishara kufahamu umuhimu wa kukata leseni kwa wakati, masharti ya leseni, wajibu na faida za kuwa na leseni, haki zao katika leseni, taratibu za kufuata wasiporidhika na utolewaji leseni, makossa na adhabu.

### (e) Uhamisho wa leseni kutoka kwa mfanyabiashara

Wadau wametaka kuwekwa utaratibu maalum iwapo mfanyabishara anahitaji kuhamisha biashara yake kwa mtu mwengine, kubadilisha eneo la biashara na kuongezeka kwa bidhaa au huduma tafauti kinyume na matakwa ya nleseni iliyotolewa. Imeelezwa kwamba maizngira yanayopelekea kuhamisha biashara yatambuliwe na kuwekewa utaratibu.

### (f) Rufaa

Wadau wamependekeza sheria izingatie utaratibu wa rufaa na taratibu za kufuatwa na wafanyabiashara na mamlaka za rufaa, kwa Sheria ya Leseni za Biashara na baadhi ya sheria nyengine zinazosimamia masuala ya leseni. Hivyo wamependekeza utaratibu huo uwe wazi zaidi, na hatua zibainishwe tokea mwanzo hadi mwisho ili kutoa uelewa kwa wafanyabishara na wananchi kwa ujumla.

### (g) Uwepo wa kumbukumbu maalum za wafanyabiashara

Wadau wamependekeza uwepo wa kumbukumbu maalum za wafanyabishara ili ziweze kutumika katika taasisi moja na nyengine na pia kwa shughuli za Serikali. Kwa sasa hakuna utaratibu maalum na taasisi zinaomba nyaraka mara kwa mar ahata kama wafanyabiashara wamewasilisha kabla, baadhi ya taasisi na mamlaka zinataka nyaraka hizo hizo kila wakati wa kulipia leseni mpya unapofika.

## SURA YA TANO

## 5.0 MIKATABA YA KIMATAIFA NA SHERIA ZA NCHI MBALIMBALI

### 5.1 Mikataba ya Kimataifa

#### (a) Shirika La Biashara Ulimwenguni (World Trade Organisation)

Shirika la Biashara Ulimwenguni lilianzishwa mnamo mwaka 1995. Shirika hilo ni mrithi wa Makubaliano ya Jumla ya Ushuru na Biashara (General Agreement on Tariff and Trade) ulioanzishwa (GATT) mwaka 1947.

WTO inawezesha kufanywa biashara ya bidhaa, huduma na mali miongoni mwa nchi wanachama kwa kutoa mfumo wa kujadili mikataba ya kibiashara, ambayo kwa kawaida hulenga kupunguza au kuondoa ushuru, upendeleo na vikwazo vyengine; makubaliano haya yanatiwa saini na wawakilishi wa Serikali wanachama.[90]

WTO pia inasimamia utatuzi huru wa migogoro kwa ajili ya kutekeleza makubaliano ya biashara na kutatua migogoro inayohusiana na biashara. Shirika linakataza ubaguzi kati ya washirika wa kibiashara, lakini hutoa vizuizi kwa ulinzi wa mazingira, usalama wa taifa, na malengo mengine muhimu.[91]

---

[90] Braithwaite J. & Drahos P. (2000) 'Global Business Regulation', Cambridge University

[91] Baldwin R. (2000) '*Regulatory Protectionism, Developing Nations and a Two –Tier World Trade System,*' International Trade and Regional Economic

Sheria zilizomo katika GATT na WTO hutumikia kwa kuzingatia malengo matatu. Kwanza, zinajaribu kulinda maslahi ya nchi ndogo na dhaifu dhidi ya mazoea ya kibaguzi ya biashara ya nchi kubwa na zenye nguvu. Vifungu vya WTO vinaeleza kwamba kila mwanachama wa WTO lazima atoe ufikiaji wa soko sawa kwa wanachama wengine wote na kwamba wasambazaji wa ndani na nje lazima wachukuliwe kwa usawa.

Pili, sheria zinawataka wanachama kuweka ukomo wa biashara kupitia ushuru pekee na kutoa ufikiaji wa soko usiofaa zaidi kuliko ule ulioainishwa katika ratiba zao (yaani, ahadi ambazo walikubali walipopewa uanachama wa WTO au baadaye). Tatu, sheria zimeundwa ili kusaidia Serikali kupinga juhudi za ushawishi za vikundi vya ndani vinavyotafuta upendeleo maalum.[92]

Hata hivyo baadhi ya tofauti na sheria zimewekwa, ingawa uwepo wao katika mikataba ya msingi ya WTO ulikusudiwa kuhakikisha kwamba unyanyasaji wa kibiashara unaepukwa, na kuleta uhakika zaidi na kutabirika kwa masoko ya kimataifa na kupunguza mivutano ya kisiasa.[93]

Mkataba wa Jumla wa Ushuru na Biashara siku zote ulishughulikia biashara ya bidhaa, na bado unafanya hivyo. Mkataba umefanyiwa marekebisho na kuingizwa katika mikataba mipya ya WTO.

---

[92] Sander H. and András I. ' World Trade After the Uruguay Round: Prospects and Policy Options for the Twenty-first Century' (1996) Routledge, at 17

[93] Hills C. A. (2007), '*How the WTO Fight Protectionism'* The International Trade Law Newsletter, Vol. 2 issue 1, March, 2009

GATT iliyofanyiwa marekebisho inasomwa pamoja na Makubaliano ya Jumla ya Biashara katika Huduma (GATS) na Makubaliano ya masuala yanayohusiana na Biashara ya Haki za Haki Miliki (Trade- Relates International Property Rights). WTO inawaleta watatu hao pamoja ndani ya shirika moja, seti moja ya sheria na mfumo mmoja wa kusuluhisha migogoro.

Tanzania ni mshirika wa mkataba wa matokeo ya Majadiliano ya Biashara ya Kimataifa (MTN the Multilateral Trade Negotiations) ambayo yalizinduliwa huko Punta Del Este nchini Uruguay mwishoni mwa 1986. Tanzania ilishiriki katika mazungumzo yaliyochukua miaka minane, na ushiriki wake kukamilika.[94]

Tanzania kwa sasa inanufaika kati ya nchi zilizochaguliwa duni na zilizoendelea na za Kiafrika katika Mpango wa Pamoja wa Msaada wa Kiufundi wa ITC/UNCTAD/WTO (JITAP), ambao unatokana na Azimio la Mawaziri la WTO la Singapore la mwaka 1996. Chini ya usaidizi huu wa kitaalam, Makubaliano ya pande zote ya Uruguay kwa uchumi wa Tanzania inachukuliwa kuwa hitaji la kipaumbele la maafisa wa sekta ya umma na watendaji wa sekta binafsi. Shughuli zinazolenga kuongeza uelewa wa Mikataba hiyo zinalenga watunga sera katika umma, wasomi na watendaji wa sekta binafsi.[95]

---

[94] Robert B. Mabele The Challenges of the Economic Partnership Agreements in Tanzania March 2007: https://library.fes.de/pdf-files/bueros/tanzania/04756.pdf

[95] UNCTAD/DITC/TNCD/7 4 October 2002 Original: United Nations Conference on Trade and Development Multilateral Trading System Impact on National Economy And External Trade Policy Adaptation United Republic Of Tanzania Report prepared by UNCTAD in the framework of the Joint ITC/UNCTAD/WTO Integrated Technical Assistance Programme to Selected Least Developed Countries and other African Countries (JITAP) Under cluster 9: MTS impact on national economy and trade policy adaptation inapatikana https://unctad.org/system/files/official-document/ditctncd7_en.pdf

### (b) GATT

GATT ilitokana na Mkutano wa Kimataifa wa Biashara na Ajira uliofanyika mwaka wa 1946 huko Havana, pendekezo la kuanzishwa kwa wakala unaoitwa Shirika la Biashara la Kimataifa (ITO) lilitolewa kwa malengo mbalimbali na ya jumla ya kuongeza na kudumisha biashara na ajira duniani.[96] Makubaliano ya Jumla ya Ushuru na Biashara (GATT) yalikuwa ni juu ya mambo mawili ambayo kuweka hati inayoweka kanuni za kufanya biashara za kimataifa, na kuundwa kwa shirika la kimataifa ili kuunga mkono makubaliano hayo.[97]

Ingawa Mkataba wa Havana wa ITO uliundwa kama aina ya katiba ya biashara ya kimataifa, haukufanikiwa kutokana na matatizo mbalimbali ikiwemo ukosefu wa makubaliano ya pamoja. Hata hivyo, baadhi ya nchi zilichukua moja ya masuala muhimu ya Mkataba wa Havana kuhusu kulegeza vikwazo vya kibiashara kwa kujumuisha katika Makubaliano ya Jumla ya Ushuru na Biashara (GATT). Hii ilitiwa saini mwaka wa 1947 na baadhi ya mataifa ishirini na tatu makubwa ya biashara. GATT ilikuzwa na kupanuliwa zaidi katika mazungumzo kadhaa baadae.[98]

Mfumo wa GATT ulibadilika zaidi ya miaka 47 na kuwa shirika la biashara la kimataifa ambalo hatimaye lilihusisha takriban nchi 130. Kupitia duru

---

[96] Understanding on the Interpretation of Article XXIV of the General Agreement on Tariffs and Trade 1994 (on regional agreements) Trade 1994

[97] World Bank '*Policy Response to Global Financial Crisis: Swimming against the Tide; How Developing Countries are coping with the Global Crisis*', World Bank Background paper prepared by World Bank Staff for the G20 Finance Ministers and Central Bank Governors meeting, Horsham, UK 13-14 March, 2009

[98] https://www.britannica.com/topic/General-Agreement-on-Tariffs-and-Trade

mbalimbali za mazungumzo, GATT ilipanuliwa au kurekebishwa kwa kanuni na mipangilio maalum.

Aidha juhudi zaidi zilizchukuliwa mwaka 1994 na mabadiliko ya awali ya GATT yaliyoanzishwa kabla ya Duru ya Uruguay yaliitwa GATT 1947 yalizingatiwa. Sehemu hii ya makubaliano ilitofautishwa na GATT 1994, ambayo inajumuisha marekebisho na ufafanuzi uliojadiliwa wakati wa Duru ya Uruguay pamoja na mikataba mengine kadhaa ya kimataifa kuhusu biashara ya bidhaa. GATT 1994 ikawa sehemu muhimu ya makubaliano yaliyoanzisha WTO. GATT na WTO zimesaidia kuunda mfumo wa biashara wenye nguvu na ustawi unaochangia ukuaji wa biashara kwa hali ya juu.[99]

Katika kuendeleza malengo ya GATT 1994 na kwa kuzingatia mahitaji ya biashara, maendeleo na fedha ya wanachama wa nchi zinazoendelea, suala la leseni lilitumika kudhibiti hatua kama zile zilizopitishwa kwa mujibu wa masharti husika ya GATT 1994, Wajumbe wa GATT waliazisha mkataba wa taratibu za leseni za kuagiza (Agreement on import licencing procedures).

Mkataba wa Taratibu za Leseni za Uagizaji unaelezea uagizaji wa leseni unapaswa kuwa rahisi, wazi na unaotabirika. Mkataba huo unatoa mwongozo wa jinsi Serikali zinapaswa kutathmini maombi ya leseni. Tanzania imefuata kikamilifu matakwa ya Duru ya Uruguay katika leseni za uagizaji na mambo ya tozo na ushuru.[100]

---

[99] Sander H. and András I. ‘ *World Trade After the Uruguay Round: Prospects and Policy Options for the Twenty-first Century’* (1996) Routledge

[100] https://www.wto.org/english/tratop_e/tpr_e/tp128_e.htm

### (c) GATS

GATS inafanya kazi ndani ya Shirika la Biashara Ulimwenguni na Sheria za GATS kuhusiana na Huduma za Utalii. Malengo ya mfumo wa WTO na GATS ni kuundwa kwa mfumo wa kimataifa wa sheria za biashara; kwa kuzingatia usawa wa wanachama wote; kukuza ukuaji wa uchumi kwa kufanya biashara huria. [101]

GATS ilianza kutumika mwaka wa 1995 na wanachama wote wa Shirika la Biashara Ulimwenguni ni wanachama wa GATS, ikiwa ni pamoja na Jamhuri ya Muungano Tanzania na ina sehemu kuu nne ikiwemo kanuni za jumla na wajibu na uhusiano wa kibiashara na nchi nyengine.

## 5.2 Mikataba ya Kikanda

### (a) East Africa community

Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) inaendelea kujumuisha mafanikio muhimu ya mashirikiano ya kikanda hususan utekelezaji wa Eneo Moja la Forodha la Jumuiya ya Afrika Mashariki, na matumizi ya Kanuni za Mwanzo za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2015.

Utaratibu wa Kuanzishwa kwa Umoja wa Forodha wa Jumuiya ya Afrika Mashariki ulitiwa saini na Wakuu watatu wa Nchi za Afrika Mashariki tarehe 2 Machi 2004 huko Arusha, Tanzania. Jamhuri za Rwanda na Burundi zilijiunga

[101] UNCTAD-ICTSD, Cambridge University Press, International Centre for Trade and Sustainable Development Cambridge University Press, 2005 ukurasa wa 130

na Umoja wa Forodha mwaka 2008 na kuanza kutumia rasmi mnamo mwaka 2009.[102]

Malengo ya Umoja wa Forodha wa EAC ni:

(a) Kuweka huru zaidi biashara ya bidhaa ndani ya EAC na kuweka misingi ya kibiashara yenye manufaa kati ya nchi wanachama;
(b) Kukuza ufanisi katika uzalishaji ndani ya Jumuiya;
(c) Kuimarisha uwekezaji wa ndani, mipakani na nje katika Jumuiya; na
(d) Kukuza maendeleo ya kiuchumi na mtawanyiko wa viwanda katika Jumuiya.

Utekelezaji wa Kanuni za Mwanzo za Jumuiya ya Afrika Mashariki, 2015, umerahisisha kufanya biashara katika eneo la EAC, kuondolewa kwa vizuizi vingi vya kodi na vizuizi visivyokuwa vya kodi katika biashara kumehamasisha usafirishaji wa bidhaa na huduma za biashara katika kila pembe ya EAC.[103]

Mwongozo wa Utumiaji wa Kanuni za Asili za Jumuiya ya Afrika Mashariki ni chapisho la Jumuiya ya Afrika Mashariki ambalo linaweka miongozo ya utekelezaji wa Kanuni za Asili za Jumuiya ya Afrika Mashariki ili kutoa upendeleo wa kodi wa jumuiya kwa bidhaa zinazokidhi vigezo vya asili na zinazouzwa kati ya Nchi Wanachama. Mwongozo unaeleza kwa kina matumizi ya vigezo vinne katika kubainisha hali ya asili ya bidhaa, taratibu za kusimamia

[102] Peter Walkenhorst "Trade Policy Developments in Tanzania: The Challenge of Global and Regional Integratio" February 2005, https://mpra.ub.uni-muenchen.de/23399/1/MPRA_paper_23399.pdf
[103] A Simplified Guide for Micro and Small-Scale Women Cross Border Traders and Service Providers within the East African Community (EAC)

sheria, taratibu za kuhudumia biashara ndogo ndogo za mipakani na mfumo wa kitaasisi wa utekelezaji wa Kanuni za Uasili.[104]

Mwongozo huu umeandaliwa ili kuwezesha tafsiri na matumizi sawa ya Kanuni za Asili katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Muongozo huu umeundwa ili kuwawezesha maofisa wa Forodha na maafisa wengine wanaohusika na uondoaji wa bidhaa kuelewa taratibu za utozaji ushuru wa Jumuiya kwa bidhaa zinazouzwa katika Jumuiya ya Afrika Mashariki. Pia ililenga kuwafanya wafanyabiashara na wadau wengine kuelewa taratibu na mahitaji ya bidhaa ili kustahiki kupewa leseni chini ya utaratibu wa biashara ya ndani.[105]

## 5.3 Sheria na uzoefu wa nchi mbalimbali

### 1. Sheria ya Leseni ya Tanzania Bara[106]

Sheria ya Leseni za Biashara ya Tanzania Bara inasimamiwa na Wizara ya Viwanda na Biashara na Mamlaka ya BRELA. Sheria hiyo ilifanyiwa marekebisho na sheria ya Fedha mnamo mwaka 2014, katika kifungu cha 8 ili kurekebisha viwango vya ada za leseni kwa biashara mbalimbali.

Wakala ya Usajili wa Biashara na Leseni (BRELA) ina mfumo wa usajili kwa Usajili wa Makampuni, Majina ya Biashara, Alama za Biashara na Huduma pamoja na huduma zote baada ya usajili kwa njia ya Mtandao. Aidha, Mfumo pia unatumika kwa utoaji wa Hati na Leseni za Biashara.

[104] Bheenick, R.M., 2003. "The EAC Customs Union Protocol: The Application of the Principle of Asymmetry." Study prepared for the East African Community Secretariat. Imani Development Consultants, Pretoria.
[105] https://www.eac.int/resources/11-document/472-710-653-manual-on-the-application-of-the-east-african-community-rules-of-origin
[106] Sheria Nam, 25 ya mwaka 1972

Miongoni mwa majukumu ya BRELA ni pamoja na kudhibiti biashara kwa kusimamia sheria za leseni za biashara na viwanda.

### *(a) Leseni za Muda kwa Wasiokua Wakaazi*

Leseni hizi zinatumika kwa watu walio katika taaluma maalum na wakandarasi majengo. Leseni hizo zinatolewa kwa watu hao baada ya kukamilisha malipo ambayo sheria hii imeweka na uhalali wa leseni hizo ni muda wa siku 30 kutoka tarehe ambayo imetolewa leseni hiyo au kwa muda mrefu zaidi kama kama Katibu Mkuu atakavyoona inafaa.[107]

### *(b) Mamlaka ya Rais*

Sheria katika kifungu cha 15, imetoa mamlaka kwa Rais, kwa msalahi ya umma kuzuia leseni za biashara za aina yoyote zilizotolewa katika eneo husika na kuweka ukomo wa kutoa leseni kwa Mashirika ya Serikali.

### *(c) Mamlaka ya Waziri*

Sheria katika kifungu cha 6, imetoa Mamlaka kwa Waziri anayesimamia biashara kuteua mtu yeyote au Mamlaka ya leseni; kutoa leseni kwa eneo maalum, biashara maalum au biashara kwa jumla. Aidha Waziri ataweka taratibu za maombi na utoaji wa leseni.

Kwa upande wa Mashirika na Serikali za Mitaa, Sheria hii imetoa pia mamlaka kwa Waziri wa Fedha kuweka utaratibu wa matumizi ya ada ikiwemo kuzuia malipo hayo kwa matumizi ya taasisi au kuingizwa katika Mfuko Mkuu wa Serikali.

[107] Kifungu cha 10

### *(d) Masharti ya kutoa leseni*

Sheria hii imeweka masharti maalum katika utoaji wa leseni za biashara ikiwemo anayepewa leseni asiwe chini ya umri wa mika 18, kukamilisha taratibu za Mamlaka au taasisi nyengine zinazotoa ruhusa ya biashara katika sheria zao, au mtu asiyekuwa raia ambaye anafanya biashara bila kukidhi masharti ya vibali alivyopewa au masharti ya Idara ya Uhamiaji.[108]

### *(e) Adhabu kwa kushindwa kukata leseni kwa wakati*

Sheria hii chini ya kifungu chake cha 10 kimetoa adhabu kwa mtu yoyote ambae atashindwa kukata leseni baada ya leseni yake ya mwanzo kupitwa na mda na zikapita siku 21 tangia leseni yake hiyo ipitiwe na muda au mtu ambae ameanza biashara na zikapita siku 21 bila kukata leseni, mbali ya malipo ya leseni atatakiwa alipe asilimia 50 ya malipo hayo kama ni adhabu

### *(f) Utaratibu wa kumaliza makosa "Compounding of offence"*

Sheria hii katika kifungu cha 22 kimeweka utaratibu wa kumaliza ikiwa kwa kuruhusu malipo ya adhabu kwa kiwango kisichopungua TZS 50,000 na kisichozidi TZS 100,000 na muombaji awe amekubali kwa maandishi kuhusu kosa lake hilo alilolifanya.

### *(g) Wajibu wa Kuthibitisha kosa*

Sheria katika kifungu cha 20 kimeeleza kwamba wajibu wa kuthibitisha kufanya au kutokufanya kosa utakuwa kwa aliyepewa leseni (mmiliki wa leseni ya biashara).

[108] Kifungu cha 14

***(h) Rufaa;***

Sheria hii katika kifungu cha 24 kinaelezea kuhusu rufaa kwa mtu ambaye amekataliwa kupewa leseni au kufutwa matumizi ya leseni ya biashara.

***(i) Makundi ya Leseni***

Sheria hii inatoa ada za leseni chini ya kifungu cha 8 kwa makundi mbalimbali ikiwemo Biashara ya wakala, (Agency business,), "Broker business", "Banking", "Financial institutions" and "capital markets", "Clearing and forwarding", "Cargo" "valuation and superintendence", "Shipping business", "Insuarance", "Manufactures representative", "Estate", "Commercial traveller", "Postal service", "Electricity power and energy supply", "Specified profession na makundi mengine ambayo yanahusisha biashara zinazosimamiwa na Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa.

**2. Jamhuri ya Vanuatu**

Kwa upande wa Jamhuri ya Vanuatu leseni za biashara zinaongozwa na Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 249 ya mwaka 1998. Kwa madhumuni ya sheria hii kifungu cha 3 kimeeleza utoaji wa leseni umewekwa katika mamlaka tatu. Mamlaka hizo ni:

(a) Waziri anaeshughulikia masuala ya fedha (kwa upande wa munispaa),
(b) Halmashauri za Serikali za mitaa (maeneo mengine ya Vanuatu) na
(c) Mkurugenzi (leseni za biashara chini ya kifungu cha 8, 9 na 10).

Leseni za biashara zinasimamiwa na mamlaka ya leseni ya biashara ya Vanuatu ambayo inaongozwa na Mkurugenzi.

Aidha sheria hii imeweka utaratibu kwa leseni za biashara kwa wawekezaji baada ya kuthibitisha na Mamlaka ya Uwekezaji;[109] na leseni za biashara ambazo hazijatajwa kwa wageni.[110]

### *(a) Maombi ya leseni*

Sheria chini ya kifungu cha 4 kimeeleza kuwa Kila maombi ya kutoa au kufanywa upya kwa leseni yatafanywa kwa Mamlaka ya utoaji leseni na mtu yeyote ambaye, bila sababu za msingi za kuamini kuwa ni kweli, akafanya au kusaidia na kuunga mkono kutoa taarifa yoyote ya uwongo katika maombi yoyote ya leseni atakuwa ametenda kosa na atalipa faini.

### *(b) Haki ya wawekezaji wa kigeni kupata leseni ya biashara*

Mwekezaji wa kigeni ambaye ameidhinishwa na mamlaka ya kukuza na kulinda Uwekezaji wa Vanuatu atakuwa na haki ya kupewa leseni ya biashara kama ilivyobainishwa katika cheti cha uwekezaji alichopewa.

### *(c) Punguzo la ada*

Kifungu cha 22 cha sheria kimeipa uwezo Mamlaka ya kutoa leseni kupunguza ada kwa zile biashara za mda maalum na biashara mpya iliyoanzishwa. Lakini hakuna punguzo litalozidi asilimia 50 ya ada iliyowekwa na kwa upande wa biashara mpya zilizoanzishwa punguzo hilo halitazidi miaka mitatu iliyofuatana.

### *(d) Madaraja ya leseni[111]*

[109] Kifungu cha 6 na 7
[110] Kifungu cha 8
[111] Kifungu cha 13

Sheria hii imezigawa leseni za biashara katika madaraja kumi na moja ambapo madaraja hayo yameainishwa kama ifuatavyo: -

(i) Uchimbaji wa madini, mchanga na kokoto;
(ii) Uzalishaji wa viwanda na biashara;
(iii) Viwanda vya ujenzi na biashara;
(iv) Biashara za jumla na rejareja;
(v) Usafirishaji, uhifadhi na huduma za kitalii;
(vi) Taasisi za kifedha, benki, bima, kampuni za makaazi, kampuni za kitaalamu na huduma za kibiashara;
(vii) Huduma za kijamii, burudani na huduma za ukarabati;
(viii) Nishati;
(ix) Sanaa na uchoraji;
(x) Biashara za upandaji, kilimo, masoko, ukamaji mazxiwa, mbogamboga, matunda na bustani; na
(xi) Uvuvi.

Madaraja hayo yameelezewa vizuri katika jaduweli la kwanza la sheria pamoja na kiwango cha ada zake.

### *(e) Baadhi ya biashara kulipa ada kila robo mwaka*

Sheria hii imetoa fursa kwa wamiliki wa leseni za Biashara za benki za biashara, taasisi nyingine za fedha, bima na huduma nyingine za kitaalamu na biashara kulipa kwa robo mwaka.

### (f) Utoaji wa leseni ya biashara

Katika kifungu cha 8 cha sheria hii ya Leseni za Biashara Sura ya 249 ya mwaka 1998 kinataka mwekezaji wa kigeni; kumkabidhi Mkurugenzi cheti cha kibali kinachobainisha leseni ya biashara kwa biashara haijaorodheshwa katika sehemu ya 13; kumpa Mkurugenzi fomu ya maombi iliyokamilika; na kulipa ada ya leseni ya biashara inayolipwa kwa leseni kwa mujibu wa kifungu cha 18.

**(g) Upya wa leseni za biashara**

Katika kifungu cha 9 ikiwa mtu (iwe mwekezaji wa kigeni au la) ambaye leseni ya biashara ilitolewa chini ya kifungu cha 5, 6, 7 au 8; na inatumika kwa ajili ya upyaji wa leseni; na kulipwa ada inayolipwa kwa leseni; Mkurugenzi au Baraza la Serikali za Mitaa, atatoa leseni mpya ya biashara.

**(h) Uhamisho wa leseni za biashara**

Katika kifungu cha 10 cha sheria kinaeleza utaratibu mzima wa uhamisho wa leseni; Kulingana na kifungu hiki, leseni ya biashara inaweza kuhamishwa na taarifa lazima ieleze namba ya leseni ya biashara; jina na anwani ya mmiliki; eneo na asili ya biashara; jina na anwani ya mhamishaji; na tarehe ya uhamisho.

**3. Seychelles**

Sheria ya biashara ya Seychelles Sura ya 113 ya mwaka 2010, imeanzisha mamlaka ambapo pamoja na kazi nyengine pia ina jukumu la kusimamia leseni zote za biashara. Mamlaka ya Utoaji Leseni ya Seychelles (SLA) ilianzishwa mnamo mwezi Septemba mwaka 1984 na ipo chini ya wizara inayoshughulikia mambo ya Fedha na imepewa majukumu yafuatayo: [112]

(a) kutoa leseni au kufanya upya leseni;

[112] Kifungu cha 9

(b) Kufuta leseni
(c) Kusitisha leseni
(d) Ambatanisha au kubadilisha masharti ya leseni

Jukumu la Mamlaka hiyo (SLA) limebadilika kwa miaka mingi kulingana na mageuzi ya kisiasa na kiuchumi ambayo yamefanyika nchini humo. Sheria ya Leseni, ya mwaka 2010 inatoa uwezo[113] kwa Mamlaka ya Leseni ya Seychelles katika mambo yafuatayo:

(a) Kutaka mtu kutoa taarifa juu ya jambo lolote linalohusiana na leseni;
(b) Kumwita mtu kuja katika mamlaka kujibu masuali au kuwailisha nyaraka;
(c) Kulisha kiapo au kusimamia;
(d) Kutoa ripoti.

Kazi za Mamlaka hii ni pamoja na kutoa leseni au leseni mpya, kubadilisha masharti ya leseni, kusitisha leseni na kufuta leseni.[114]aidha sheria imeanzisha Rejista maalum na imeweka hati maalum kwa lseni na maeneo ya leseni.[115]

### *(a)* Masharti ya *leseni*[116]

Kifungu cha 20 kimeweka masharti ya kupata leseni na bila kujali Sheria nyengine yoyote, hakuna mtu atakaye shiriki au kufanya shughuli yoyote ya biashara au taaluma, iliyoainishwa katika Jaduweli; kuweka au kusimamia

[113] Kifungu cha 10
[114] Kifungu cha 9
[115] Kifungu cha 20
[116] Kifungu cha 20

majengo yoyote yaliyotajwa katika Jaduweli isipokuwa iwe kwa mujibu wa leseni iliyotolewa na Mamlaka.

### *(b) Bodi na maamuzi ya Rufaa*

Kutakuwa na Bodi maalum ya Rufaa kwaajili ya kusikiliza na kuamua rufaa dhidi ya maamuzi ya Mamlaka. Hivyo mtu yoyote ambaye hajaridhika na uamuzi Mamlaka anaweza kuwasilisha rufaa kwa maandishi kwa Bodi ya Rufaa. Bodi ya Rufani inaweza, pale inapowasilisha notisi ya rufaa, kuamua rufaa kwa kuthibitisha uamuzi wa Mamlaka; kubatilisha uamuzi; na kuamuru Mamlaka kuangalia upya uamuzi wa Mamlaka kama ilivyoelekezwa na Bodi ya Rufani.

### *(c)* **Kumaliza kosa "Compounding of offence"**

kifungu cha 27 cha sheria hii kimempa mamlaka Afisa mtendaji mkuu wa Mamlaka kumtolesha faini isiyozidi kiwango kilichowekwa chini ya kifungu cha makosa cha sheria aliyetenda kosa chini ya sheria hii ikiwa tu mtu huyo atakubali kwa maandishi kosa lake hilo. Faini hiyo itachukuliwa kama imetolewa na Mahakama.

## 4. Botswana

Botswana inaongozwa na Sheria ya Biashara Sura ya 43:02 ya mwaka 2008 katika kusimamia leseni za biashara. Sheria hii mbali ya mambo mengine imeanzisha yafuatayo:

### *(a) Kuanzishwa kwa kamati za leseni*

Sheria katika kifungu cha 4 imeunda Kamati ya leseni kwa kila Halmashauri na wajumbe wa kamati hiyo watateuliwa na Waziri. Kila kamati ya leseni itakayoundwa itakuwa na wajumbe wafuatao:

(i) Afisa mkuu wa Halmashauri ambaye hatakuwa chini ya cheo cha C1;

(ii) Afisa Biashara kutoka Halmashauri;

(iii) Mjumbe wa sekta binafsi, ambaye atakuwa Mwenyekiti; na

(iv) Diwani.

***(b) Maombi ya Leseni***

Sheria katika kifungu cha 10 kimeelezea jinsi maombi ya leseni ya takavyopelekwa kwa kamati ambapo Mtu anatakiwa kuwasilisha maombi ya leseni kwa namna itakavyoelekezwa na atawasilisha maombi hayo kwa kamati ya leseni ya Halmashauri katika eneo analotaka kufanyia biashara. Kamati ya leseni itapeleka maombi hayo kwa Waziri.

***(c) Leseni zitakazotolewa chini ya Sheria***

Kamati ya leseni chini ya kifungu cha 11 imepewa uwezo wa kutoa leseni za biashara zifuatazo dalali, duka la vitabu, boutique, kuosha magari, huduma za usafishaji,curio shop, Maghala,msambazaji, dry-clean mazao mapya, jumba la mazishi, duka la samani, Duka la Nguo, na muuzaji jumla

Aidha leseni nyengine zilzioainishwa ni Saluni za kike, vifaa vya ujenzi, hire service, sehemu za kufulia nguo, vifaa vya magari, vituo vya mafuta, mgahawa, maduka yenye mchanganyiko wa bidhaa, “take away, wholesale, workshop, or miscellaneous trade or business”.

***(d) kutolewa na muda wa leseni***

Kifungu cha 13 cha sheria kimeweka wazi kuwa Kamati ya leseni baada ya kujiridhisha kuwa muombaji amekamilisha matakwa yote ya utoaji wa leseni itampa leseni yenye masharti kama itakavyoona ni muhimu, na leseni hiyo itatumika kwa kipindi cha miezi 12 isipokuwa kama ilifanywa upya au kufutwa hapo awali.

***(e) Bodi ya Rufaa ya Mkoa***

Sheria hii pia imeanzisha katika kifungu cha 21, bodi za rufaa kwa kila mkoa. Wajumbe wa bodi hizo wanachaguliwa na Waziri. Bodi hiyo itakua na wajumbe wafuatao akiwemo mjumbe kutoka sekta binafsi ambaye atakuwa Mwenyekiti; Katibu wa Baraza au Karani wa Mji; wawakilishi wawili kutoka sekta ya kibinafsi walioteuliwa kwa misingi ya kikanda; mwanachama wa Huduma ya Polisi ya Botswana wa cheo cha Sajenti au zaidi; mwakilishi wa Wizara ya Ardhi na Nyumba; mwakilishi wa Wizara ya Biashara na Viwanda; na Madiwani watatu kama Waziri atakavyoamua.

Bodi hii ya rufaa imeanzishwa kwa ajili ya kusikiliza rufaa ya Mtu ambaye hakuridhika na uamuzi wa kamati ya utoaji leseni katika mazingira ya kutotoa au kuhuisha leseni; kutohamisha leseni; kusimamisha leseni; au kubatilisha leseni.

Mtu anaweza kukata rufaa kwa maandishi kwa Bodi ya Rufani ya Mkoa ndani ya siku 30 baada ya taarifa ya uamuzi huo na ikitokea hakuridhika na uamuzi wa Bodi ya Rufani ya Mkoa anaweza kukata rufaa kwa Waziri kwa maandishi, ndani ya siku 30 baada ya taarifa ya uamuzi wa Bodi.

### *(f) Uhamisho wa leseni*

Kifungu cha 17 kimetoa fursa kwa mtu anayemiliki leseni ya biashara kuhamisha leseni yake kwa mtu mwengine kupitia maombi maalum. Kwa madhumuni ya kifungu hiki "kuhamisha leseni" maana yake ni kutoa tena leseni ya biashara kwa mtu mwingine mbali na mtu aliye na leseni biashara hiyo.

## 5. Tonga

Tonga inatumia Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 40:02 ya mwaka 2016 ambayo imezingatia yafuatayo:

### *(a) Mtu anaefanya biashara atashikilia leseni*

Kwa mujibu wa Sheria hii, kila mfanyabiashara katika Ufalme anajiehusisha na biashara ni lazima awe na leseni halali ya biashara.

### (b) Wakati leseni ya biashara haitatolewa

Katika sheria hii kifungu cha 5 kimetoa ufafanuzi juu ya mazingira ambayo yatapelekea mtu kunyimwa leseni ya biashara ikiwemo mtu anayejishuhulisha biashara iliyokatazwa; mtu aliye chini ya umri wa miaka 18; ubia ambapo mmoja wa washirika ni chini ya umri wa miaka 18; mwekezaji wa kigeni ambaye hana cheti halali cha uwekezaji au mfanyabiashara yeyote pekee ambaye katika kipindi cha miaka mitano iliyopita ameondolewa kuwa mkurugenzi wa kampuni chini ya Sheria ya Makampuni.

Aidha mazingira mengine yaliyowekwa ni ubia wowote ambapo mmoja wa washirika aliondolewa kuwa mkurugenzi wa kampuni miaka mitano iliyopita

chini ya Sheria ya Makampuni; mfanyabiashara yeyote au mfanyabiashara aliyependekezwa ambaye miaka mitatu kabla imepatikana na hatia ya kosa la jinai; mfanyabiashara yeyote au mfanya biashara aliyependekezwa ambaye ana hukumu dhidi ya kushindwa kulipa deni; Mtu ambaye kwa maoni ya Waziri, anaweza kuwa tishio kwa usalama wa taifa na usalama wa umma.

**(c) Afisa Leseni ya Biashara**

Katika sheria hii kifungu cha 6 cha sheria kinatoa mamlaka kwa Afisa Mtendaji Mkuu atakuwa Msajili mwenye dhamana ya kutoa leseni za biashara na utekelezaji wa masharti ya Sheria hii. Pia Msajili anaweza kukasimu madaraka yake hayo kwa mtu au watu wengine katika Wizara.

**(d) Masharti ya leseni**

Katika sheria hii kifungu cha 9 Leseni ya biashara inatowa masharti kupata leseni ambayo inaruhusu mtu wa biashara kushiriki katika jamii yoyote au makundi ya shughuli za biashara zilizowekwa katika kanuni kama shughuli zinazoruhusiwa, na kila aina hiyo au makundi yaliyoorodheshwa kwenye leseni moja; kwa mujibu wa kanuni na masharti yoyote yaliyoidhinishwa kwenye leseni ambazo zinaendana na Sheria hii.

**(e) Rufaa**

Katika sheria hii kifungu cha 12 ya leseni za biashara kinatoa ruhusa ya mfanyabiashara kukata rufaa kwa Mmiliki yeyote wa leseni ya biashara atakuwa na haki ya kukata rufaa uamuzi chini ya kifungu cha 11, kwa Waziri ambaye uamuzi wake utakuwa wa mwisho, Rufaa zote zitawasilishwa ndani ya

siku 10 za kazi za uamuzi, Mtu yeyote atakayeomba chini ya kifungu hiki atakuwa na haki ya kusikilizwa na Waziri.

**(f) kuhamishwa Leseni**

Katika sheria hii kifungu cha 13 kimeonesha kuwa leseni haiwezi kuhamishwa endapo mmiliki wa leseni ya biashara anataka kuuza au vinginevyo kuhamisha mali zake kwa mtu wa tatu, mtu kama huyo wa tatu anaweza kuwasilisha maombi kwa Msajili kwa leseni ya biashara kabla ya kukamilika kwa uuzaji au uhamisho wa mali, na Msajili anaweza, ikiwa programu iko katika kwa mujibu wa Sheria hii, kutoa leseni ya biashara kwa mtu wa tatu katika kabla ya uuzaji au uhamisho wa mali ili kuruhusu kuendelea uendeshaji wa biashara.

# SURA YA SITA

## 6.0 MATOKEO YA UTAFITI

### 6.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea matokeo yaliyopatikana katika utafiti huu unaohusiana na usimamizi na utoaji wa leseni za biashara. Sura hii imejumuisha yaliyojitokeza katika maoni ya wadau, maelezo ya Mipango ya nchi, Sera na sheria mbalimbali zinazohusiana na leseni, na uzoefu wan chi mbalimbali. Matokeo ya utafiti huu yanatokana na sehemu kubwa ya njia za utafiti ambazo zimetumika kukamilisha kazi hii.

### 6.2 Njia zilizotumika katika Utafiti

Njia zilizotumika kufanyia tafiti eneo hili la leseni za biashara limehusisha kwa asilimia kubwa utafiti wa ndani uliopitia sera, sheria mbalimbali, mikataba ya kimataifa, vitabu na maandiko mbalimbali yaliyozungumzia leseni za biashara.

Aidha njia nyengine ni kukutana na wadau wanaohusika na eneo hili la leseni za biashara na vyombo mbalimbali vinavyosaidia katika usimamizi wa mfumo wa leseni za biashara pamoja na mamlaka za kutoa leseni.

### 6.3 Upeo wa utafiti

Utafiti huu umelenga kuangalia utataribu uliopo katika usimamizi na utoaji wa leseni za biashara katika Sheria Nam. 3 ya mwaka 1983 na mapungufu yaliyopo katika usimamizi wa sekta hii kwa kuzingatia matakwa ya mikataba ya

kimataifa ambayo Tanzania imeiridhia, Sera mbalimbali, Dira 2050, ILANI ya CCM na MKUZA III.

## 6.4 Ukomo wa utafiti

Katika kufanya utafiti huu, mapungufu yafuatayo yamejitokeza:

(a) Kutokuwepo kwa utaratibu na miongozo mizuri inayohusiana na usimamizi na utoaji wa leseni kwa Mamlaka zilizopo;

(b) Kutokuwepo uelewa wa kutosha kwa jamii na taasisi za Serikali kuhusu taratibu za maombi ya leseni, masharti, sifa na uwezo wa mamlaka za leseni;

## 6.5 Hadidu rejea

Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imeandaa ripoti hii kwa kufuata hadidu rejea zifuatazo ambazo zitaiweka muelekeo mzuri wa matumizi ya leseni:

(a) Kufanya tathmini ya utaratibu uliowekwa katika sheria Nam. 3 ya mwaka 1983 katika utoaji wa leseni za biashara.

(b) Kuangalia uzoefu wa nchi mbalimbali kuhusiana na masuala ya usimamizi wa leseni za biashara na kwa namna gani uzoefu huo unaweza kuisaidia Zanzibar.

(c) Kuangalia Sera na sheria mbalimbali za Zanzibar zinazohusiana na usimamizi au utoaji wa leseni za biashara.

(d) Kupitia mikataba mbalimbali ya kikanda na kimataifa ambayo inahusiana na leseni za biashara na kuona ni kwa namna gani zinaweza kusaidia katika marekebisho ya sheria hii.

(e) Kutoa mapendekezo yanayofaa ya kisera na kisheria kwa lengo la kupunguza au kuondosha kabisa changamoto zilizopo kwenye leseni za biashara.

### 6.6 Sampuli za utafiti

Kufikia malengo ya utafiti huu, jumla ya makundi matano (5) yalihusishwa. Makundi hayo yalijumuisha Taasisi mbalimbali za Serikali, Taasisi za binafsi zinazohusiana na masuala ya Leseni za Biashara, maafisa wanaotoa leseni za biashara, Wadau wanaotoa Leseni za Biashara hapa nchini, wadau kutoka Taasisi za Muungano zinazotoa leseni, wanasheria na waandishi wa habari na wafanyabiashara. Wadau hao ni kama wafuatao:

1. Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda;
2. Baraza la Kusimamia Mfumo wa Leseni za Biashara;
3. Wakala wa Chakula, Dawa na Vipodozi;
4. Afisi ya Msajili wa Hakimiliki;
5. Bodi ya Mapato Zanzibar;
6. Bodi ya Ushauri na Udhibiti Vileo Zanzibar;
7. Tume ya Utangazaji Zanzibar;
8. Wakala wa Maabara ya Mkemia Mkuu wa Serikali;
9. Wakala wa Usajili wa Biashara na Mali;
10. Mamlaka ya Hifadhi na Uendelezaji Mji Mkongwe;
11. Baraza la Manispaa ya Mjini;
12. Mamlaka ya Usafiri Baharini;
13. Kamisheni ya Utalii Zanzibar;
14. Mrajis wa Elimu;
15. Idara ya Maendeleo ya Uvuvi na Mazao ya Baharini;

16. Idara ya Misitu;
17. Bodi ya Hospital Binafsi;
18. Mamlaka ya Usafiri wa Anga Tanzania;
19. Mamlaka ya Usimamizi wa Shughuli za Bima Tanzania;
20. Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu Tanzania;
21. Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania;
22. Benki Kuu ya Tanzania;
23. ZABCO; Wabadilishaji Fedha za Kigeni Zanzibar.
24. UKIAMWIMA
25. Zanzibar National Chamber Of Commerce;
26. ZMCL;
27. ZANZIBAR FREIGHT FORWARDERS BUREAU
28. ZEXA.

Vikao vya wadau vilifanyika katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Jumla ya wawakilishi wote walioshirikishwa ni 97. Katika idadi hii ya washiriki, wanawake walikuwa ni 31 na wanaume walikuwa ni 62.

Wawakilishi kutoka makundi mbali mbali ya wadau ambao wameshiriki katika utafiti huu wametoa mapendekezo tofauti kuhusu leseni za biashara na malengo yake. Hata hivyo, kila kundi lilikuwa na maslahi tofauti na kwa kila kundi wawakilishi walitofautiana sana na wawakilishi katika makundi mengine ya wadau.


Kwa baadhi ya makundi mengine, hakukuwa na tofauti kubwa katika maoni na mapendekezo. Matokeo yetu, hata hivyo, yanaweza kuwa na athari kwa Wadau

katika usimamizi wa leseni za biashara. Jadueli Nam. 1 linaonesha washiriki wote wa Zanzibar.

***Jadueli Nam. 1: Idadi ya washiriki wote wa Utafiti.***


| **Makundi** | **Waliohudhuria** | **Walioalikwa** | **Asilimia** |
|---|---|---|---|
| Taasisi za Serikali zinazotoa Leseni | 29 | 35 | 90.8 |
| Wafanyabishara na jumuiya za wafanyabiashara | 41 | 45 | 73.3 |
| Taasisi za Serikali ya Muungano zinazotoa Leseni | 7 | 7 | 100.0 |
| Wanasheria | 8 | 8 | 100.0 |
| Waandishi wa Habari | 2 | 2 | 100.0 |
| **Jumla** | **87** | **97** | 89.7 |

***Chati Nam.1: Mchanganuo wa washiriki kwa Jinsia***




Matokeo ya utafiti yanaonesha kuwa, asilimia 75.9% ya washiriki walikuwa wanaume wakati asilimia 24.1% walikuwa wanawake. Washiriki wanawake walikuwa wachache kutokana na ukweli kwamba masuala ya leseni imeshirikisha wanaume wengi kuliko wanawake.

*Chati Nam. 2:Idadi na Asilimia ya Washiriki kwa Mujibu wa Kiwango cha Elimu*




Matokeo yanaonesha kuwa asilimia (5.7%) ya washirki wana elimu ya sekondari na asilimia (56.3%) walikuwa na elimu baada ya sekondari, na asilimia ambao ni wasimamizi na watoaji wa leseni asilimia (35.6%) walikuwa na elimu ya juu kuanzia Digirii ya kwanza na kuendelea. Lengo kubwa la kufanya uchambuzi huu, ni kuonesha kwamba mbali ya watendaji wa Serikali waliotoa maoni, uhalisia unaonesha kwamba makundi yanayojishughulisha na masuala ya leseni za biashara yana elimu ya juu. Chati Nam. 2 linaonesha kuwa shughuli za leseni zinafanywa na wataalam.

## 6.7 Matokeo ya Utafiti

Baada ya utafiti huu na kuzingatia Mikataba ya Kimataifa na uzoefu wa sheria z anchi mbalimbali, maoni ya wadau na Mipango ya Nchi kama MKUZA, DIRA 2050, ILANI YA CCM na Sera mbalimbali zinazosimamia masuala ya biashara nchini, Utafiti huu umebaini yafuatayo:

## 1. Maoni ya Jumla

### (a) Uwepo wa Sheria nyingi zinazosimamia utoaji leseni

Utafiti huu umebaini uwepo wa sheria nyingi zinazosimamia leseni, vibali na ruhusa za biashara, na baadhi ya sheria zimeweka utaratibu wake wenyewe bila kuzingatia masharti ya sheria nyengine. Hali hii inaleta kikwazo katika udhibiti wa shughuli za biashara zinazosimamiwa Zanzibar.

Utafiti huu umechambua usimamizi wa leseni za biashara mbalimbali zinazosimamiwa na kubaini baadhi ya maeneo yenye usimamizi ni pamoja na kada za afya, Madaktari wa tiba mbadala na wafamasia; wasanifu majengo; madalali; wauzaji wa vitabu na maduka ya boutique; watangazaji, wajenzi na wakandarasi; wakulima, wavuvi; wafanyabiashara wa jumla; wenye hoteli; wawekezaji; wauzaji na wasambazaji wa vileo; wafanyakazi wa meli; wafua dhahabu na fedha; watembezaji na vyombo vya watalii; mawakala wa usafiri; wakataji miti; Chakula na vinywaji; maeneo huru ya kiuchumi; kumbi za burudani; usimamizi wa mazingira n.k.

Biashara hizi ni nyingi na bado kuna maeneo yanayohitaji kuratibiwa kwa pamoja kabla ya kutoa leseni za biashara.

### (b) Kukosekana utaratibu maalum wa utoaji leseni

Tume imebaini kwamba ingawa kuna leseni nyingi ambazo hutolewa chini ya Sheria ya Leseni ya Biashara ya mwaka 1983, kwa sasa kuna sheria nyengine zinazozungumzia utoaji wa leseni na kila sheria ina utaratibu wake, baadhi ya taasisi zinachanganya utoaji wa leseni na vibali katika ngazi ya Serikali kuu na

Serikali za mitaa. Tume inaona, bila ya kuwa na Sera madhubuti ya kusimamia utoaji wa leseni za biashara na kuhakikisha utekelezaji unaratibiwa, usimamizi wa biashara utashindwa kulenga mipango mikuu ya nchi na Sera ya Serikali katika usimamizi wa biashara nchini.

#### (c) Urasimu katika Maombi ya leseni za Biashara

Utafiti huu umebaini kuwepo kwa urasimu mkubwa katika taratibu za utoaji wa Leseni za Biashara kupitia taasisi mbalimbali na sheria zinazosimamia masuala ya leseni Zanzibar. Aidha imebainika kwamba urasimu huo unasababishwa na uwepo wa vyombo na taratibu nyingi zinazotakiwa kufuatwa kabla ya kupatiwa leseni hali inayosababisha usumbufu kwa wananchi na inayoshawishi uwepo wa rushwa katika utoaji wa leseni.

Kukosekana kwa utaratibu maalum na urasimu kunaleta mgongano kati ya taasisi za Serikali na malalamiko ya wananchi katika taasisi za leseni.

#### (d) Ugumu wa kukadiria gharama

Tume imebaini kuwepo kwa ugumu wa kukadiria gharama halisi za kusimamia taratibu za utoaji leseni Zanzibar. Hali hii imesababishwa na mgawanyiko wa kitaasisi na kiutawala wa mfumo wa udhibiti, hasa katika utoaji leseni. Wakati wa vikao vya wadau Tume imebaini Zanzibar ina wingi wa taasisi zenye majukumu mbalimbali ya kutoa leseni kwa namna ambayo kuna usumbufu, mwingiliano na kutofautiana, ikiwa ni pamoja na ukosefu wa utekelezaji madhubuti. Suala ambalo linawaongezea gharama wafanyabiashara.

### 2. Matokeo Kisheria

**(a) Muundo wa Mamlaka**

Utafiti huu umebaini kutokuwepo uwazi katika mamlaka za kusimamia leseni zinazotambulika na zilizoanzishwa katika sheria na jinsi mamlaka hizo zinavyofanyakazi. Katika sheria ya Leseni ya mwaka 1983 inatambua Kamati za Mapinduzi za Wilaya na Kamati ya Mapinduzi za Mikoa, Kamati ambazo kwa muundo wa sasa wa Serikali haziwezi kufanyakazi.

**(b) Utaratibu wa maombi ya leseni**

Tume imebaini kwamba sheria iliyopo haijaanisha wazi utaratibu wa maombi ya leseni, aina za biashara, watu wanaopaswa au kustahili kupatiwa leseni, muda wa leseni, kufutwa kwa leseni, utaratibu kwa biashara zinazohitaji zaidi ya leseni moja ili kumrahisishia mfanyabiashara kupata leseni hizo kwa urahisi na kwa utaratibu unaotambulika. Aidha viwango vya ada vilivyotajwa katika sheria ili kupata leseni, ni vya muda mrefu na vimepitwa na wakati.

**(c) Uhamisho wa leseni kutoka kwa mfanyabiashara**

Utafiti umebaini kwamba kifungu cha 17 cha Sheria ya Leseni za Biashara kimeeleza uhamisho wa leseni kwa kuzingatia biashara iliyohamishwa sehemu moja kwenda sehemu nyengine, baada ya kukamilisha taratibu za maombi na kulipa ada inayotakiwa. Hata hivyo, utafiti umebaini kuna haja ya kuweka mazingira na masharti ya uhamisho wa leseni ili uhamisho huo usitumike vibaya na kuwafanya baadhi ya wafanyabiashara kuficha biashara mpya wanazoanzisha.

**(d) Adhabu kwa makosa mbalimbali ya leseni**

Utafiti umebaini kwamba sheria hii imeweka adhabu kwa makosa mbalimbali ya leseni, ingawa kutokana na ukuaji wa biashara na kubadika kwa mfumo wa baishara, malengo ya Sera ya Biashara, mipango ya nchi, uzoefu wa nchi mbalimbali kuna haja ya kuainishwa adhabu kwa wakati wa sasa, adhabu ambazo zitasaidia kufikia malengo yaliyowekwa.

Aidha utafiti huu umebaini kutokuwepo kwa utaratibu wa kumaliza baadhi ya makosa (compounding of an offence) kwa kulipwa faini tu kwa makosa madogo madogo ambayo yana adhabu ndogo kisheria na kupunguza utitiri wa kupeleka mashauri mengi ya kiutawala mahakamani. Hatua hii itarahisisha usimamizi na utatuzi wa makosa hayo kwa muda mfupi na kuwafanya wafanyabiashra waendelee na shughuli zao za kiuchumi.

**(e) Rufaa**

Utafiti umeonesha kwamba utaratibu wa kukata rufaa haupo wazi kwa kutokuainisha taratibu na mamlaka za rufaa, kwa Sheria ya Leseni za Biashara na baadhi ya sheria nyengine zinazosimamia masuala ya leseni. Hivyo Tume inaona kuna haja ya kuweka utaratibu wa rufaa kwa makosa yanayohusiana na leseni, makosa yanayopaswa kukatiwa rufaa, mamlaka za rufaa, taratibu za kukata rufaa na utekelelezaji wa maamuzi ya rufaa.

**(f) Makundi ya leseni**

Utafiti huu umebaini kwamba utaratibu wa sheria mbalimbali na Sera ya Biashara inaainisha uwepo wa makundi mbalimbali ya leseni chini ya sheria, kutambuliwa biashara zinazokubalika na kuweka upeo wa mamlaka ya Serikali za mitaa na mamlaka nyengine zinazotoa leseni. Sheria iliyopo sasa imetambua

aina tatu za leseni ambazo ni wafanyabiashara wa kawaida, wafanyabiashara wa jumla na biashara za kibenki.

Tume imebaini kwamba leseni zilizotolewa chini ya Sheria ya mwaka 1983, na kukokotoa gharama za kufuata leseni za kawaida, zinahusiana na biashara ya jumla na rejareja na kuacha sekta nyingi za biashara ambazo zinahitaji kusimamiwa kwa sasa.

Kukua kwa uchumi na kuimarika kwa teknolojia kumeongeza kwa kiasi kikubwa wigo wa biashara nchini, na kupelekea uwepo wa aina nyingi za biashara zinazohitaji usimamizi na misingi mikuu ya kutoa leseni za biashara.

**(g) Kazi na uwezo wa mamlaka za leseni**

Utafiti umebaini kwamba kutokana na asili ya biashara za Zanzibar na kutanuka kwa biashara kuna haja ya kubainishwa na kutafautishwa kazi na uwezo wa mamlaka za leseni, mamlaka ya Waziri anayehusika katika masuala ya leseni, utaratibu wa kukasimu madaraka ya Mamlaka ya leseni na mambo mengine yanayohusu leseni.

**(h) Kutambuliwa aina za biashara**

Utafiti umebaini kwamba sheria ya Leseni yam waka 1983, imeeleza biashara ambazo hazipaswi kupewa leseni chini ya kifungu cha 5 ambazo ni masuala ya kilimo (agricultural selling) ambayo ni kwa matumizi ya mtu mwenyewe; fundi mwashi (handcraftsman) ambaye ameajiriwa au huduma zake zinahusisha "repair" za bidhaa na sio mauzo ya bidhaa moja kwa moja na mtu yeyote aliyepewa leseni chini ya Sheria nyengine.

Hivyo kutokana na kuwepo Mamlaka nyengine zinazotoa na kusimamia leseni kwa mujibu wa sheria, kuna haja ya kubainisha biashara zinazopaswa kusimamiwa chini ya sheria hii, ili kuepuka mgongano wa utendaji katika Mamlaka za leseni.

**(i) Utaratibu wa kuhamisha leseni**

Utafiti umebaini sheria haikuweka masharti yua kuhamisha leseni ikiwa mwenye biashara amefariki, kampuni imefilisika ya kwa sababu nyengine yoyote itakayositisha uendelezaji wa biashara iliyopo. Aidha umiliki taratibu, na masharti yaliyopo yanapaswa kuwekwa kisheria ili kuepuka udanganyifu na ukwepaji wa kodi katika eneo hili.

**(j) Usajili wa leseni**

Imebainika kwamba hakuna utaratibu wa usajili na utambuzi wa leseni zilizotolewa, biashara kwa mujibu wa sekta, kutambua malipo ya ada za leseni na matumizi yake. Uwepo wa usajili na rejista maalum utasaidia kutambua aina za biashara zilizopo, sekta zilizoguswa sana katika biashara Zanzibar na kuweza kufanya tathmini ya usimamizi wa leseni za biashara Zanzibar.

**(k) Utaratibu wa pingamizi za leseni**

Utafiti umeini kwamba sheria haijabainisha utaratibu wa kuweka pingamizi za biashara, mamlaka ya Waziri kuzuia aina ya biashara, na utaratibu wa kushughulikia malalamiko na hatua za kuchukuliwa kwa wafanyabiashara watakaoakata rufaa.

**(l) Leseni za wafanyabiashara wadogo wadogo**

Zanzibar ina wafanyabiashara wadogo wadogo wengi ambao baadhi yao wameqatiwa vitambulisho vya kufanyabiashara lakini hawajawekewa utaratibu wa kuzitambua biashara zao. Uzoefu wa nchi mbalimbali unaonesha ujumuishwaji wa wafanyabiashara wadogo wadogo katika sheria, aidha utaratibu wa usimamizi wa na miongozo mbalimbali ikiwemo ILANI ya CCM, Dira 2050 zinaeleza kutambuliwa na kuwekewa utaratibu mzuri wafanyabiashara wadogo wadogo wa Zanzibar.

**(m) Utaratibu wa kumaliza makosa**

Utafiti umeini kwamba sheria haijaweka utaratibu wa kumaliza makosa kwa makosa madogo madogo ambayo hayahitaji kupelekewa muhusika Mahkamani au kiumpeleka huko kutapelekea kupoteza muda na kusitisha biashara.

### 3. Kiutendaji

**(a) Kuwepo utitiri wa Mamlaka za leseni**

Utafiti umebaini kwamba kuna Mamlaka nyingi za leseni ambazo baadhi yake mamlaka zao zinaingiliana, aidha imebainika kuna mamlaka za Usimamizi (Regulators) ambazo sheria zao zinataka zisimamie utaalamu uliopo lakini zinatoa leseni za biashara na hivyo kufanya baadhi ya wafanyabiashara kuwa na leseni nyingi katika biashara moja inayofanywa.

**(b) Kutokukutana Mamlaka za leseni**

Imebainika kwamba mamlaka za leseni hazina mfumo wa kukutana ili kujadili changamoto zilizopo katika leseni ili kurahisisha mfumo wa biashara.

Imebanika kwamba kila Mamlaka inatumia uwezo wake kisheria na kiutendaji bila kuzingatia uwezo na utendaji wa mamlaka nyengine ya Serikali.

### (c) Kushughulikia baadhi ya leseni katika sehemu moja "One stop centre"

Tume imebaini kwamba kuna baadhi ya biashara zinashindwa au zinachelewa kuanzishwa kutokana urasimu na mlolongo mrefu wa taratibu za mamlaka mbalimbali Zanzibar, hali inayolalamikiwa na wawekezaji na wafanyabiashara wenye sekta nyingi za biashara.

Kwa lengo la kuimarisha biashara na uwekezaji Zanzibar, Tume imeona ipo haja ya kuanisha kituo maalum cha kurahisisha upatikanaji wa leseni au taratibu zilizopo hasa kwa wawekezaji, wafanyabishara wakubwa na wenye biashara nyingi ili kuweza kuziunganisha biashara zao.

## SURA YA SABA

## 1.0 MAPENDEKEZO YA TUME NA HITIMISHO

### 1.1 Utangulizi

Katika kufanya mapitio ya Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983, Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar imefanya vikao mbali mbali vya wadau ikiwemo taasisi na Mamlaka za leseni za Zanzibar na Muungano zinazotoa leseni kwa biashara Zanzibar ili kupata maoni na mapendekezo ya utaratibu wa utoaji wa leseni Zanzibar. Hatua hiyo imebainisha uwepo wa utitiri wa mamlaka za utoaji wa leseni ambazo zinapelekea wafanyabiashara wa Zanzibar kutokufurahia utaratibu uliopo na kupelekea usumbufu.

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imechukua hatua mbalimbali kuhakikisha mazingira mazuri, shirikishi na salama kwa wafanyabiashara wa ndani na nje ya Zanzibar. Juhudi hizo zinapaswa kutekelezwa katika hatua mbalimbali ikiwemo kupitia Sheria zinazohusiana na leseni za biashara Zanzibar ili kuwa na utaratibu unaokubalika.

### 1.2 Uchambuzi na Changamoto za Mfumo wa Leseni za Biashara Zanzibar

#### (a) Kutokutekelezeka kwa vifungu vingi vya sheria

Kutokutekelezeka kwa vifungu vingi vilivyomo ndani ya sheria hii na hivyo kuleta ugumu katika utekelezaji wake; na kutokuainishwa wazi utaratibu mzuri wa usimamizi wa leseni kupitia Mamlaka mbalimbali zinazotoa leseni Zanzibar.

Inapendekezwa kuandaliwa sheria mpya itakayoweka mfumo mzuri zaidi wa biashara na kuunganisha biashara mbalimbali zinazohusiana na kumilikiwa na mtu mmoja.

**(b) Taratibu za Kudhibiti**

Kuna aina mbalimbali za taratibu katika sheria na kanuni zinazotumika kusimamia na kudhibiti biashara. Kuna usajili, vyeti, vibali, leseni, uidhinishaji, viwango, n.k. Maneno haya yanatumika kwa kuyachanganya na hakuna upeo wa kila moja ili kutoa uelewa kwa wananchi na Mamlaka zinazohusika kisheria. Hivyo, ni muhimu kuzingatia njia hizi maana zake na jinsi zinavyoweza kutumika katika usimamizi wa biashara.

**(c)Ufafanuzi**

Katika kifungu cha 2, sehemu ya tafsiri kuna tafsiri nyingi hazipo wazi na kuonekana kuwa ni kikwazo na baadhi ya tafsiri zinazohusiana na usimamizi wa leseni hazijajumuishwa kwa mazingira yaliyopo sasa kama vile tafsiri ya biashara, leseni, mamlaka za leseni n.k.

Ufafanuzi uliopo unathibitisha kuwa leseni hutolewa kwa biashara moja na kukosekana utaratibu wa kusajili biashara nyingi zilizo katika eneo moja la biashara leseni, hivyo kuna haja ya kuhusishwa leseni na eneo la kufanyia biashara kama biashara za usafiri zinazohitaji idhini ya IATA, mikahawa, usindikaji wa chakula na majengo n.k. sheria inapaswa ieleze wazi uhusianao wa sheria hii na sheria za mamlaka nyengine zinazotoa leseni.

**(d) Kuweka ukomo kwa baadhi ya biashara**

Sheria imeweka ukomo kwa baadhi ya biashara kwa kutoa ruhusa za biashara za uwakala katika kifungu cha 4, biashara za kufanywa na madalali (brokers) na mashirika ya umma. Uzoefu wa sasa unaonesha kunahitajika kuweka mifumo inayoonana katika taasisi zinazosimamia biashara ili kuhakiki na kuthibitisha taarifa za wafanyabiashara.

### (e) Katazo la biashara

Sheria imeeleza biashara mbalimbali ambazo hazipaswi kukatiwa leseni ikiwemo mkulima yeyote anayeuza mazao ambayo amezalisha kwa umiliki wake mwenyewe, suala ambalo halijabainisha wazi; fundi yeyote ambaye ni mfanyakazi au mwanafunzi wa fundi mwengine au ambaye kazi yake ni kutengeneza kwa mteja anayemiliki bidhaa; na mtu yeyote ambaye tayari ana leseni au idhini nyengine chini ya sheria nyengine yoyote kutekeleza biashara au tasnia yoyote, ili mradi tu biashara hiyo iwe na biashara au tasnia yenye leseni au iliyoidhinishwa.

Makatazo haya yanatakiwa kuzingatia iwapo waliotajwa hawapati kipato katika biashara zao, udhibiti ili wakulima au mafundi wengine wasitumie vibaya fursa hii kisheria, na mwisho malengo ya Serikali yanapaswa kuzingatiwa kwa kuainisha maeneo au wafanyabishara maalum wenye kipato cha chini ambao Serikali imekusudia kuwawekea mazingira rafiki ya biashara zao na kuwapunguzia gharama.

### (f) Taratibu za rufaa

Sheria katika kifungu cha 6 (1) kinatoa mamlaka ya kuteuliwa Bodi ya Leseni za Biashara ili kusimamia mchakato wa utoaji leseni, na wajumbe wasiozidi.

Bodi imepewa katika kifungu cha 7 (1) imepewa mamlaka ya kuwaelekeza maafisa wa leseni katika uendeshaji wa majukumu yao na mwombaji yeyote ambaye hakuridhika na maamuzi ya afisa anayetoa leseni anaweza kukata rufaa kwa Bodi. Sheria ipo kimya juu ya mchakato wa kukata rufaa, mamlaka zinazowajibika kuwa chini ya Bodi hii na haijatoa mbadala iwapo Bodi ya Leseni haitakuwepo.

### (g) Mchakato wa Utoaji Leseni

Vifungu vya 9 na 10 vinaeleza aina za leseni, mahitaji ya ada ya kila mwaka au nusu ya mwaka na mchakato wa maombi ya leseni. Sheria imeweka aina za leseni za wafanyabiashara wa jumla, mfanyabiashara wa rejareja na benki. Kuna haja ya kujumuishwa makundi na aina nyingi zaidi za biashara kutokana na mabadiliko ya uchumi na mifumo ya biashara iliyopo sasa.

Aidha ngazi zilizoelezwa katika kifungu cha 10, zinajumuisha muda wa maombi (kesi ya leseni za miezi sita) na kwamba maombi lazima yapokewe kabla ya miezi miwili (au mwezi mmoja kwa upande wa leseni ya nusu mwaka) baada ya kuanza kwa muda wa leseni.

Kifungu cha 10 (2) kinaeleza kuwa afisa leseni apeleke maombi ya uchunguzi kwa Kamati ya Mapinduzi ya Wilaya ambayo biashara hiyo ipo. Kamati hizi kwa sasa hazipo katika Mfumo wa KiSerikali na Mamlaka za Miji na Mabaraza zimekuwa na mamlaka yao kisheria yanayopaswa kutekelezwa bila kupitia katika Kamati.

### (h) Makosa na Adhabu

Kifungu cha 21 kinaweka makosa manne ya jumla: kufanya biashara bila leseni halali; kutoa maelezo yasiyo sahihi; kushindwa kutoa taarifa sahihi; na kujaribu kukiuka masharti ya Sheria. Kuna haja ya kuongeza idadi ya makosa yanayohusiana na utolewaji leseni za biashara kwa kuzingatia Sera ya Biashara na Mipango ya Serikali iliyopo.

Kifungu cha 22 kinampa mamlaka Waziri, baada ya kushauriana na Mwanasheria Mkuu wa Serikali na Kwa idhini ya Rais, kufuta leseni yoyote ya biashara na kutostahiki mtu yeyote, ikiwa ni, katika maoni ya Waziri, haina maslahi ya umma. Uzoefu unaonesha kuwa utaratibu huu kwa sasa unatekelezwa na Waziri tu na hakuna haja ya kumjumuisha Mwanasheria Mkuu au Mheshimiwa Rais katika maamuzi haya.

## 1.3 Mapendekezo ya Tume

Tume baada ya kufanya utafiti na tathmini ya kina katika usimamizi wa leseni Zanzibar imebaini kuwepo mapendekezo ya Kisera, Kisheria na Kiutendaji, kwa lengo la kuimarisha misingi na mifumo ya biashara Zanzibar.

### 1.3.1 Mapendekezo ya Jumla

Tume inapendekeza mfumo wa leseni Zanzibar uwekewe utaratibu maalum na utoe vipaumbele vya maendeleo na mageuzi ya Serikali. Mpango wa Maendeleo ya Sekta Binafsi Zanzibar (PSDP), unasisitiza kuwa vikwazo katika ushindani wa biashara vinapaswa kuondolewa ili kuleta mabadiliko ya kiuchumi na kwamba mazingira ya udhibiti na ya gharama nafuu ni muhimu kwa uchumi imara na mahiri unaoendeshwa na sekta binafsi na kuweza kushindana katika masoko ya kikanda na kimataifa.

Inapendekezwa Sheria kuweka wazi usimamizi wa sheria hii kupitia Wizara husika inayosimamia biashara kwa kujumuisha upatikanaji wa takwimu za biashara zilizopo, kiwango cha uzingatiaji, na hatua za kuchukuliwa kisheria; taasisi na mamlaka zinazohusika chini ya sheria hii; mfumo na muda wa kusimamia leseni; Bodi zinazotambuliwa na mamlaka zao; makadirio ya leseni na taarifa kuhusu gharama za kuendesha mfumo ya biashara; uhusiano gani wa kitaasisi kati ya Idara ya Biashara na Bodi za leseni au maafisa wa leseni; ukubwa wa mapato ya kila mwaka yanayokusanywa kupitia mfumo wa leseni za biashara na uchangiaji katika Pato la Taifa (GDP).

### 1.3.2 Kisera

Tume inapendekezwa kuanzishwa katika Sera ya Biashara ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na kuweka udhibiti na usimamizi wa leseni za wafanyabiashara wa kati na wadogo (MSMEs). Hatua hii ni muhimu sana kwa ukuaji na maendeleo ya uchumi wa Zanzibar na juhudi za Serikali za kupunguza umasikini na kuboresha maisha ya wananchi wake.

Tume ya kurekebisha Sheria inapendekeza Sera ya Biashara ifanyiwe marekebisho ili ijumuishe na kubainisha kwa uwazi usimamizi wa leseni za biashara kwa Mamlaka zinazotoa leseni. Hatua hii itaweka mwongozo mzuri, itaeleza lengo la leseni za biashara na kuondoa utaratibu uliopo sasa wa kila mamlaka kuweka masharti ya leseni ambayo, baadhi yake, badala ya kumrahisishia mfanyabiashara na mwekezaji kufanya biashara, inakuwa kikwazo cha kuendeleza au kuanzisha biashara Zanzibar. Inapendekezwa maeneo ya Sera yajumuishe:

(a) kulenga na kuhakikisha kunawekwa mwongozo wa utoaji leseni Zanzibar na kusaidia maafisa leseni na wafanyabiashara kufikia maamuzi ya utaratibu wa maombi na utoaji wa leseni na masharti ya kuzingatiwa,

(b) kuangalia mfumo mzima wa kisheria kuhusu utaratibu na utoaji wa leseni kwa wawekezaji waliopo ndani na nje ya Zanzibar,

(c) kuainisha na kutoa miongozo juu ya uanzishwaji wa kituo cha "One Stop Center" katika eneo ambalo litakuwa ni rahisi kupata leseni kwa watu ambao wana biashara zaidi ya moja au wanahitaji vibali vya taasisi nyingi,

(d) Kuweka utaratibu wa kutoa leseni za biashara kwa mfumo wa kielektroniki,

(e) Kutambua na kuweka rejista maalum ya wafanyabiashara wenye leseni,

(f) kutoa ufafanuzi wa dhana za leseni kwa waombaji na maafisa katika utoaji na usimamizi wa leseni,

(g) kueleza biashara na shughuli mbalimbali za utoaji leseni zinazopaswa kuzingatiwa kwa mujibu wa sheria, utamaduni na silka za Zanzibar,

(h) kueleza Mamlaka zinazowajibika kusimamia masuala ya leseni ikiwemo Serikali za Mitaa, Mashirika ya umma ambayo yanalazimika kutoa leseni moja kwa moja kwa kuzingatia sheria zao, mamlaka za usimamizi (regulators) ikiwemo udhibiti, afya, Usalama, Viwango vya Biashara n.k na masharti yao,

(i) Kueleza Mamlaka za Rufaa na mamlaka ya kukasimu madaraka ya utoaji leseni; na utaratibu wa malalamiko na Rufaa kwa wenye malalamiko ya kupatiwa leseni, na

(j) Kuweka mazingira ya ushirikiano wa taasisi, Serikali za Mitaa, Wakala, Mashirika ya Umma na taasisi nyengine ili zifanye kazi kwa karibu katika kusimamia masuala yanayohusiana na utaratibu wa utoaji leseni.

### 1.3.3 Mapendekezo ya Kisheria

### 1. Mapendekezo ya Jumla

#### (a) Kutungwa kwa sheria mpya

Katika mapendekezo ya kisheria, Tume ya kurekebisha Sheria inapendekeza kufutwa kwa Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983 kutokana na sababu zifuatazo:

(ii) Kutokutekelezeka kwa vifungu vingi vilivyomo ndani ya sheria hii na hivyo kuleta ugumu katika utekelezaji wake;

(iii) Kutokuainishwa wazi utaratibu mzuri wa usimamizi wa leseni kupitia Mamlaka mbalimbali zinazotoa leseni Zanzibar;

(iv) Kutokuwepo kwa Mfumo wa leseni unaosimamia mamlaka zote zilizopo Zanzibar; na

(v) Kutokujumuishwa maeneo muhimu katika sheria.

#### (b) Mambo ya Kuzingatia

Inapendekezwa katika kutoa leseni za biashara yafuatayo yazingatiwe:

(i) utaratibu bora na wa gharama nafuu zaidi wa kuhakikisha mazingira mazuri ya biashara;

(ii) Kubainishwa wazi jukumu la Serikali;

(iii) Kuhakikisha hakuna utata katika matumizi ya taratibu za utoaji leseni za biashara;

(iv) viwango vya uwajibikaji; na

(v) Kutekeleza wajibu wa wafanyabiashara.

**(c) Utaratibu wa Udhibiti.**

Tume inapendekeza kuweka utaratibu mzuri wa udhibiti, ukusanyaji wa taarifa za usajili, hesabu na usajili wa leseni zinazotumika katika uchumi wa Zanzibar au ukokotoaji wowote wa gharama za mfumo wa utoaji leseni kwa jumuiya ya wafanyabiashara au mashirika ya sekta ya umma yanayohusika na utekelezaji wa mifumo ya leseni.

**(d) Mifumo ya Utoaji leseni**

Tume inapendekeza kubainishwa wazi mifumo ya utoaji wa leseni katika ngazi zote za Serikali kuu na Serikali za mitaa; pamoja na kuweka utaratibu wa kutambua leseni zinazotolewa chini ya mamlaka ya sheria ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Tume inapendekeza kuwekwa utaratibu maalum wa kisheria ili kurahisisha upatikanaji wa leseni leseni muhimu ikiwemo leseni ya biashara (ambayo inatumika kwa takriban makampuni yote), na leseni muhimu katika utalii, kilimo na usafiri. Makundi haya ni muhimu kwa kuwa hayana uwezo wa kuchukua fursa ya uchumi wa kiwango ili kupunguza athari za kibiashara.

**2. Mapendekezo ya Mswada**

Pamoja na Rasimu ya Mswada inayoambatanishwa na Utafiti huu, Tume inapendekezwa Sheria mpya ijumuishe maeneo yafuatayo:

**1. Kuweka wazi zaidi ufafanuzi wa vifungu**

Tume inapendekeza kuwekwe ufafanuzi wa maneno mengine zaidi ili kutoa uelewa na kuweka mwongozo ulio wazi kwa Mamlaka zinazotoa leseni za

biashara, ikiwemo tafsiri za leseni, biashara, leseni za biashara, bidhaa, mamlaka za leseni, mmiliki wa leseni n.k.

**2. Muundo wa taasisi**

Tume inapendekeza Baraza la Leseni lilioanzishwa chini ya Sheria ya Udhibiti wa Mfumo wa Utozaji Leseni za Biashara Nam. 13 ya mwaka 2013 liimarishwe zaidi na lipewe jukumu la kusimamia Sheria hii na kudhibiti Mamlaka za leseni zote zinazotolewa Zanzibar. Mamlaka hii iweke kumbukumbu zote za biashara, rejista, na kuunganisha Mamlaka za utoaji leseni katika Mfumo maalum.

Kuimarishwa kwa chombo hiki kutasaidia kusimamia utekelezaji wa uendeshaji wa Leseni za Biashara, Chombo hicho kipewe nguvu ya kisheria ya kusimamia taasisi nyengine za Serikali na kitambulike kama Mamlaka ya Leseni za Biashara.

**3. Utaratibu wa utoaji leseni**

Tume inapendekeza sheria iweke vizuri zaidi mfumo wa utoaji wa leseni na mfumo huo ujumuishe:

**(a) Masharti ya kufanya biashara baada ya kupata leseni**

Sheria ieleze marufuku kwa mfanyabiashara kufanya biashara bila kukata leseni halali, leseni hiyo iwe na masharti na mambo ya msingi ya kuzingatiwa kabla ya kutolewa.

**(b) Mamlaka ya leseni**

Sheria ieleze Mamlaka za leseni, na uteuzi wa mamlaka nyengine zinazotambuliwa kisheria. Aidha utaratibu wa kukasimu madaraka kwa mamlaka au taasisi ubainishwe wazi katika sheria.

**(c) Aina za leseni zitazotolewa**

Sheria iweke aina za leseni na biashara zitakazimamiwa chini ya sheria inayopendekezwa.

**(d) Utaratibu wa maombi**

Sheria hii iainishe utaratibu wa maombi ya wa leseni chini na namna Mamlaka inavyoweza kushughulikia maombi hayo. Utaratibu ujumuishe vielezo vinavyohitajika, muda wa leseni, ada na masharti mengine.

**(e) Taratibu za leseni kwa wageni /wawekezaji**

Inapendekezwa sheria ieleze masharti na utaratibu wa maombi ya leseni kwa wawekezaji na jinsi wanavyoweza kupata leseni kupitia uhusiano wa taasisi mbalimbali (One Stop Centre).

**(f) Kufutwa kwa leseni ya biashara**

Sheria iweke wazi Leseni ya biashara inaweza kufutwa na Mamlaka ya leseni chini ya masharti ya sheria. Aidha mambo yanayoweza kupelekea kufutwa kwa leseni yawekwe wazi.

**(g) Uhamisho wa leseni za biashara**

Sheria ieleze utaratibu wa kuhamishwa leseni na mmiliki wa leseni ya biashara na sababu na mazingira yanayoweza kufanya leseni hiyo ihamishwe.

**4. Masharti mengine ya leseni**

**b. Kutolewa nakala au leseni nyengine**

Sheria iweke utaratibu na mamlaka ya kutoa nakala ya leseni iwapo itathibitika kuwa leseni ya biashara imepotea, imeharibiwa au katika hali yoyote haiwezi kubandikwa au kupatikana katika uhalisia wake.

**c. Uwekaji wa kumbukumbu**

Sheria itambue kumbukumbu zinazohitajika, utaratibu wa kumbukumbu, masharti ya kuwasilisha kumbukumbu inapohitajika, na upatikanaji wa taarifa za kifedha.

**d. Leseni za wafayabishara wasio na maeneo maalum**

Ili kuweza kudhibiti kundi hili na kuweka mazingira bora ya biashara, Sheria itambue uwepo wa leseni za biashara kwa wafanyabiashara wasio na maeneo maalum na utaratibu wao wa maombi ya leseni uelezwe.

**e. kutoa au kukataa leseni ya biashara**

Sheria iweke wazi muda wa kushughulikia maombi ya leseni na sababu za kukataa kutoa leseni iwapo leseni itakataliwa.

**f. Ukaguzi wa leseni ya biashara**

Sheria ibainishe maafisa walioidhinishwa na mamlaka ya leseni, na muda unaotakiwa kufanya ukaguzi na kuingia katika majengo yoyote ya biashara kwa lengo la kukagua leseni ya biashara na kujiridhisha kwamba masharti ya leseni yanafuatwa.

## 5. Taratibu na mamlaka za maamuzi

Sheria inayopendekezwa ieleze uwezo na mamlaka za Waziri katika usimamizi na ufutaji wa leseni, Mamlaka za leseni na maafisa wa leseni katika usimamizi, ukaguzi na ufutaji leseni na uhifadhi wa taarifa za leseni.

## 6. Uwasilishaji wa malalamiko na Rufaa

Sheria iweke utaratibu wa kuwasilisha malalamiko, pingamizi kwa kukataliwa au kukiukwa taratibu za utoaji leseni, taratibu za kushughulikia malalamiko na pingamizi pamoja na muda na utaratibu na mamlaka za rufaa, pamoja na wajibu wa kuthibitisha kosa.

## 7. Marekebisho au mabadiliko ya taarifa za Leseni

Sheria iweke wazi taratibu za kufuatwa iwapo mfanyabiashara anataka kufanya mabadiliko au marekebisho ya taarifa zilizo katika leseni yake na taratibu za kufuatwa na afisa leseni kabla ya kufanya mabadiliko kwa taarifa na maandishi.

## 8. Mamlaka ya Waziri

Inapendekezwa sheria iweke mamlaka ya Waziri husika katika kutunga Kanuni, kubadilisha viwango vya Ada au kuweka utaratibu na mfumo mbadala wa utoaji leseni.

## 9. Makosa na adhabu

Inapendekezwa Sheria iweke adhabu kwa yeyote anayekiuka au kushindwa kufuata masharti ya utoaji wa leseni kwa kujumuisha makosa mengi zaidi ili

wafanyabiashara waweze kufuata taratibu zinazotakiwa. Aidha inapendekezwa Sheria iweke mazingira ya utaratibu wa kumaliza makosa (compounding of offences) kwa mtu ambaye atafanya kosa ambalo si la kijinai, chini ya sheria na kama atakubali kosa lake basi kesi hiyo iweze kumalizwa kupitia makubaliano badala ya kwenda Mahakamani.

### 1.3.4 Mapendekezo ya Kikanuni.

Baada ya kupitishwa kwa Sheria inayopendekezwa, Tume ya Kurekebisha Sheria inapendekeza mamlaka husika kuharakisha kutungwa kwa Kanuni za Sheria hii ili zitoe ufafanuzi wa vifungu vya Sheria na Sheria hii iweze kutekelezeka kwa urahisi.

Aidha, inapendekezwa utungaji wa Kanuni hizo uzingatie masharti muhimu katika kutunga Kanuni ili kuepuka kucheleweshwa kwa hatua za kutumika kwa Kanuni hizo.

### 1.3.5 Mapendekezo ya Kiutendaji

Tume inapendekeza mbali ya masuala ya Kisera, Kisheria na Kikanuni, yafuatayo yawekewe utaratibu ili kutimiza azma ya Serikali ya kuipa nguvu taasisi ya Leseni za Biashara na kuweka utaratibu mzuri wa taarifa kwa taasisi za umma.

(a) Kuandaliwe Mpango Mkakati kwa ajili ya utekelezaji wa utoaji wa leseni kwa taasisi za Serikali na zisizo za kiserikali: Taratibu nyingi za utoaji wa leseni zina vikwazo visivyo vya lazima kwa biashara, uwekezaji na ufanisi wa kiuchumi; kupunguza kasi ya mwitikio wa biashara kwa

mabadiliko katika soko, na kupunguza ubunifu na upatikanaji wa nafasi za ajira, hali inayokatisha tamaa wafanyabiashara na wajasiriamali.

(b) kuwekwa mazingira ambayo yanakuza ushindani mzuri wa biashara na kupunguza gharama, ili kusaidia utekelezaji wa sera ya umma, katika maeneo kodi, usalama na ulinzi wa mazingira. Hata hivyo, utaratibu wa sasa unapelekea gharama kubwa kwa biashara, na uchumi kwa ujumla.

(c) Kutolewa mafunzo zaidi kwa watendaji wa taasisi zinazotoa na kusimamia leseni za biashara.

(d) Kutoa elimu kwa wajasiriamali wadogo na wafanyabiashara juu ya umuhimu na faida za ukataji wa leseni kwa wakati na kuwashirikisha kwa karibu ili waweze kupunguza usumbufu wa kulipa faini pindi utakapochelewa kukata leseni.

(e) Kuwekwa ushirikiano mzuri baina ya taasisi ya leseni za biashara na Taasisi za umma, ambao utalenga katika mafunzo na programu ambazo zinaweka wazi utumiaji wa leseni kwa wafanyabiashara.

## 7.4 Hitimisho

Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983 ni sheria mama ya leseni ya biashara na ni ya muda mrefu. Aidha, mbali ya kuwepo kwa mabadiliko ya mifumo ya kibiashara, mabadiliko ya uchumi na utandawazi, sheria hii haijafanyiwa marekebisho au mapitio ili kwenda sambamba na mabadiliko hayo.

Tatizo jengine lililobainika ni uwepo wa Mamlaka nyingi zilizoanzishwa kisheria na kufanya usimamizi wa leseni kujumuisha taasisi nyingi, na hivyo kupelekea mkanganyiko wa matumizi ya sheria sahihi kwa wafanyabiahsara na

kuleta usumbufu katika usimamizi na ufuatiliaji wa wafanyabiashara wa Zanzibar.

Baadhi ya Mamlaka zimekuwa zikichanganya utolewaji wa leseni, usajili, ruhusa na vibali na nyengine kuchukua mamlaka ya leseni za biashara kutokana na Sheria hii kutokuweka wazi ukomo na matumizi halisi ya sheria. Tume inaamini kwamba kuwekwa kwa Mfumo mzuri unaofahamika katika utoaji wa leseni na usimamizi wa mamlaka zinazotoa leseni, utasaidia kuimarisha mfumo wa biashara uliopo, kuweka mifumo rafiki ya kufanya biashara, na hatimaye kusaidia kukuza uchumi wa Zanzibar.

Tume inapendekeza Mfumo wa leseni utakaowekwa kwa ajili ya udhibiti wa leseni za biashara katika sekta mbalimbali za kiuchumi na sekta ndogo na ngazi zote za Serikali kuanzia Serikali ya kitaifa hadi ya mitaa.

Mifumo hii iwe ya uwazi, na ubora; iunganishe kazi za udhibiti wa kitaasisi na kurahisisha michakato ya udhibiti; kupunguza mzigo wa kiutawala na gharama za jumla za shughuli kwa biashara; kuondoa matumizi ya leseni kama njia ya kuzalisha mapato; kuchangia katika lengo pana la kujenga utamaduni wa utoaji huduma ndani Zanzibar.

## REJEA

### VITABU NA MAKALA

Abdul Sheriff, "The Peasantry Under Imperialism, 1873 - 1963" in Abdul Sheriff and Ed Ferguson (eds.) Zanzibar Under Colonial Rule (London: James Currey, 1991), p.112 and Abdul Sheriff, "The Spatial Dichotomy of Swahili Towns: The Case of Zanzibar in the nineteenth Century" in AZANIA: Journal of the British institute in Eastern Africa, Volume XXXVI-XXXVII 2001-2002, (Nairobi: The British Institute in Eastern Africa), 2002

Akman Pinar, *The Concept of Abuse in EU Competition Law: Law and Economic Approaches*, 2012, Hart Publishing, Oxford

Antoniak M (1995). 21st Century Entrepreneur: How to Start a Home Business. New York: Avon

Anderman, Steven & Schmidt Hedvig, *EU Competition Law and Intellectual Property Rights: The Regulation of Innovation, 2011*, 2nd edition, Oxford University Press, Oxford.

Baldwin R. (2000) '*Regulatory Protectionism, Developing Nations and a Two –Tier World Trade System,*' International Trade and Regional Economic

Bheenick, R.M., 2003. "The EAC Customs Union Protocol: The Application of the Principle of Asymmetry." Study prepared for the East African Community Secretariat. Imani Development Consultants, Pretoria.

Booth, D., Cooksey, B., Golooba-Mutebi, F., & Kanyinga, K. (2014). East African prospects: an update on the political economy of Kenya, Rwanda, Tanzania, and Uganda. Overseas Development Institute. https://www.odi.org/publications/8383-east-african-prospectsupdate-political-economy-kenya-rwanda-tanzania-and-uga

Braithwaite J. & Drahos P. (2000) 'Global Business Regulation', Cambridge University

Cichocki KM, "Unlocking the Future of Public Libraries: Digital Licensing that Preserves Access" (2007-2008) 16 University of Baltimore Intellectual Property Law Journal

Cross W M, (2012) "Restoring the Public Library Ethos: Copyright, E-Licensing, and the Future of Librarianship," Law Library Journal 104:2

David McKitterick (1992) *A History of Cambridge University Press*: Volume 1, Printing and the Book Trade in Cambridge, 1534 -1698 printed by the Syndicate of the University of Cambridge

Dreschle B (2001). Small-Scale Mining and Sustainable Development within the SADC Region, MMSD project of IIED, International Institute for Environment and development. Available at: https://www.scribd.com/document/91701845/Small-Scale-Miningand-Sustainable-Development-Within-the-SADC-Region

Fred H. Cate, (2002). "The commodification of information and the control of expression," *Amicus Curiae* (Journal of the Institute of Advanced Legal Studies, School of Advanced Studies, University of London), volume 43, pp.. 3–7.

Gellhorn W (1956) "Individual Freedom and Governmental Restraints."Baton Rouge: Louisiana State University Press

Gervais D, Maurushat A, "Fragmented Copyright, Fragmented Management: Proposals to Defrag Copyright Management" (2003) Canadian Journal of Law and Technology 2, 15

Hills C. A. (2007), '*How the WTO Fight Protectionism'* The International Trade Law Newsletter, Vol. 2 issue 1, March, 2009

Hinkes, 2007:709 Hinkes E M, "Access Controls in the Digital Era and the Fair Use/First Sale Doctrines" (2006-2007) 23 Santa Clara High Technology Law Journal 685

Hildebrand, Doris, *The Role of Economic Analysis in the EC Competition Rules, 2009*, 3rd edition, Kluwer Law International

John Willey & Sons Australia Ltd, *Mohan Dhall (contributing author)*; *Business Studies in Action, Preliminary Course*; Stephen Chapman, Natalie Devenish 3rd Edition

Kampala Capital City Authority (KCCA) (2017), Trading Licence (Assessment, Payment & Issuance). Available at: https://www.kcca.go.ug/uDocs/Trade_Licence_FAQs.pdf

Khadija Shamte Mzee "Setting up A Business in Zanzibar: The Legal Requirements," LYBL Volume 8 -2018

Paul Dobson and Rob Stokes: (2012) *Commercial Law*, Sweet and Maxwell London,

*Protecting Your Trademark; Enhancing Your Rights through Federal Registration*, BASIC Facts About Trade mark, United States Patent ND Trademark Office; available at https://www.uspto.gov/sites/default/files/documents/BasicFacts.pdf

Pedro A. De Miguel Asensio: *The Law Governing International Intellectual Property Licensing Agreements (A Conflict of Laws Analysis)*, Research Handbook on Intellectual Property Licensing Cheltenham, Edward Elgar Publishing, 2013

Peter Stimpson and Alex Smith *Business Management for the IB Diploma 978-1-107-46437-7*, Second Edition, Cambridge University Press 2015

Peter Walkenhorst "Trade Policy Developments in Tanzania: The Challenge of Global and Regional Integratio" February 2005, https://mpra.ub.uni-muenchen.de/23399/1/MPRA_paper_23399.pdf

Robert B. Mabele The Challenges of the Economic Partnership Agreements in Tanzania March 2007: https://library.fes.de/pdf-files/bueros/tanzania/04756.pdf

Sander H. and András I. (1996) "World Trade After the Uruguay Round: Prospects and Policy Options for the Twenty-first Century" Routledge

Robert Goldscheider and Alan H. Gordon Editors, (2006) *Licensing Best Practices, Strategic, Territorial, and Technology Issues*, John Wiley & Sons, Inc, Wiley

Squitieri, Mauro (2012) *Refusals to License Under European Union Competition Law After Microsoft*, Journal of International Business and Law: Vol. 11: Issue. 1, Article 4.

Steve Suranovic (2010): *International Trade: Theory and Policy*; George Washington University Saylor Foundation

Tilley, H. (2014). The political economy of aid and accountability: the rise and fall of budget support in Tanzania. New York: Routledge

UNCTAD-ICTSD, Cambridge University Press, International Centre for Trade and Sustainable Development Cambridge University Press, 2005

World Bank (2010) "Doing Business in Zanzibar 2010" A Co publication of the World Bank and the International Finance Corporation, inapatikana https://openknowledge.worldbank.org/bitstream/handle/10986/13439/74678.pdf?sequence=1&isAllowed=y

*World Bank "Doing Business 2016 Measuring Regulatory Quality and Efficiency*, 3rd edition," World Bank Group Comparing Business Regulation for Domestic Firms in 189 Economies

World Bank Group *Doing Business 2016 Measuring Regulatory Quality and Efficiency*, 13th edition, Comparing Business Regulation for Domestic Firms in 189 Economies, World Bank Group

World Bank '*Policy Response to Global Financial Crisis: Swimming against the Tide; How Developing Countries are coping with the Global Crisis*', World Bank Background paper prepared by World Bank Staff for the G20 Finance Ministers and Central Bank Governors meeting, Horsham, UK 13-14 March, 2009

**TOVUTI**

https://ij.org/activism/legislation/model-legislation/model-economic-liberty-law-1/

https://www.andrewsarbenz.com/business-attorney-tacoma-business-licsense

https://www.investopedia.com/terms/t/trade.asp

https://www.dictionary.com/browse/trade

Trade License- Category, Eligibility, Registration, FAQs (taxguru.in)

https://www.lendingkart.com/blog/trade-licens

https://mn.gov/deed/business/starting-business/legal-regulatory/

https://en.wikipedia.org/wiki/Essential_facilities_doctrine

https://www.britannica.com/topic/General-Agreement-on-Tariffs-and-Trade

https://www.eac.int/resources/11-document/472-710-653-manual-on-the-application-of-the-east-african-community-rules-of-origin

https://www.wto.org/english/tratop_e/tpr_e/tp128_e.htm

**KESI**

MCI v. AT&T, 708 F.2d1081, 1132 (7th Cir. 1983);

Hecht v. Pro-Football, Inc., 570 F.2d 982, 992-93 (D.C. Cir. 1977),

CommissionDecision 92/213/EEC, 1992 O.J. (L 96) 34 (British Midland v. Aer Lingus

*Inc. v.Trinko*, 124 Ct. 872, 881 (2004)

*In the Heart of Atlanta Motel v. United Sates* 379 U.S. 241, 85 S.Ct.348 13 L.Ed.2d 258 (1964)

**MIKATABA NA RIPOTI**

UNCTAD/DITC/TNCD/7 4 October 2002 Original: United Nations Conference on Trade and Development Multilateral Trading System Impact on National Economy And External Trade Policy Adaptation United Republic Of Tanzania Report prepared by UNCTAD in the framework of the Joint ITC/UNCTAD/WTO Integrated Technical Assistance Programme to Selected Least Developed Countries and other African Countries (JITAP) Under cluster 9: MTS impact on national economy and trade policy adaptation inapatikana https://unctad.org/system/files/official-document/ditctncd7_en.pdf

Understanding on the Interpretation of Article XXIV of the General Agreement on Tariffs and Trade 1994 (on regional agreements) Trade 1994

A Simplified Guide for Micro and Small-Scale Women Cross Border Traders and Service Providers within the East African Community (EAC)

Programme Management Unit, 'Property and Business Formalisation Programme, Vol. 5, Business Formalisation Reform Packages and Outline for Zanzibar'.

Report Analysis of the Business Licensing Regime in Zanzibar Project 6036 Revolutionary Government of Zanzibar April 2011, Maxwell Stamp PLC : Phase 1

General Agreement on Tariff and Trade) ulioanzishwa (GATT) mwaka 1947.

**MIPANGO YA NCHI**

Dira ya Maendeleo ya 2050- 2050

ILANI YA CCM 2020-2015

**SERA**

Sera ya Biashara ya mwaka 2006

Sera ya Uwekezaji ya mwaka 2005

Sera ya Wajasiriamali Wadogo na wa kati Zanzibar ya mwaka 2005

Sera ya Ajira Zanzibar 2009

Sera ya Serikali za Mitaa Zanzibar ya mwaka 2012

Sera ya Mazingira ya mwaka 2014

Sera ya Mafuta na Gesi Zanzibar (Upstream) ya mwaka 2016

Sera ya Afya Zanzibar ya mwaka 2010

Sera ya Kilimo Zanzibar ya mwaka 2000

Sera ya Uvuvi Zanzibar ya mwaka 2000

Sera ya Usalama wa Chakula Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Usafiri Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Asasi za Kiraia Zanzibar ya mwaka 2008

Sera ya Elimu Zanzibar ya mwaka 2006

Sera ya Habari na Mawasiliano ya mwaka 2013

Sera ya Jinsia Zanzibar ya mwaka 2005

Sera ya Usimamizi wa Maafa Zanzibar ya mwaka 2011

Sera ya Hifadhi ya Jamii ya mwaka 2014

**SHERIA**

Sheria ya Tume ya Kurekebisha Sheria Zanzibar namba 16 ya mwaka1986

Sheria ya Leseni za Biashara Nam. 3 ya mwaka 1983

Sheria ya Biashara Nam. 14 ya mwaka 2013

Sheria ya Usimamizi Mfumo wa Leseni za Biashara Nam. 13 ya 2013

Sheria ya Utalii Zanzibar Nam. 6 ya mwaka 2009

Sheria ya Misitu na Mali zisizohamishika Nam. 10 ya 1996.

Sheria ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa Zanzibar Nam. 7 ya 2014

Sheria ya Uvuvi Nam. 7 ya mwaka 2010

Sheria ya Mamlaka ya Bahari Zanzibar Nam. 3 ya mwaka 2009.

Mamlaka ya Udhibiti wa Huduma za Maji na Nishati Zanzibar Nam. 7 ya 2013.

Sheria ya Vileo Nam. 9 ya mwaka 2020

Sheria ya Chakula, Dawa na Vipodozi Nam. 2 ya mwaka 2006

Sheria Ya Tume ya Utangazaji Zanzibar Nam. 7 ya 1997

Kanuni ya Usafiri wa Baharini (Usajili na Leseni za Vyombo) ya mwaka 2007

Zanzibar Industrial Property Act, Nam. 4 ya mwaka 2008

Sheria ya Usajili wa Makandarasi Nam. 6 ya mwaka 2008

Sheria ya Benki ya Tanzania (BOT) Nam. 4 ya mwaka 2006

Sheria ya Usimamizi wa Mabenki na Taasisi nyengine za Kifedha Nam. 5 ya mwaka 2006

Sheria ya Kusimamia Maendeleo ya Uvuvi wa Bahari kuu Nam. 5 ya mwaka 2020

Sheria ya Bima Nam. 10 ya mwaka 2009

Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania Nam. 12 ya mwaka 2003 "TCRA"

Sheria ya Leseni ya Tanzania Bara Sheria Nam, 25 ya mwaka 1972, Sura ya 208 Sheria za Tanzania

Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 249 ya mwaka 1998 Vanuatu

Sheria ya biashara ya Seychelles Sura ya 113 ya mwaka 2010

Sheria ya Biashara Sura ya 43:02 ya mwaka 2008 Botswana

Sheria ya Leseni za Biashara Sura ya 40:02 ya mwaka 2016 Tonga